**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Nne - Tarehe 10 Februari, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):**

Taarifa ya Mwaka wa Hesabu za Mfuko wa Fedha za Barabara kwa mwaka 2003/2004 *(The Annual Report and Accounts of the Roads Fund Board for the Year 2003/2004)*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 36

**Makao Makuu ya Serikali**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE (k.n.y MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA):** Kwa kuwa zoezi la kuhamishia Makao Makuu ya Serikali Dodoma limechukua miaka mingi bila kukamilika; na kwa kuwa hata nyumba za Mawaziri zimejengwa Dar es Salaam:-

Je, isingekuwa jambo bora kutamka rasmi kuwa Bunge liendelee kukutana Dodoma na Serikali iendelee kuendeshea shughuli zake Dar es Salaam, kwa kuzingatia kuwa gharama za kujenga zinapanda sana na je, kuna ubaya gani kubadilisha uamuzi huo ili kujenga heshima ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kuhamishia Serikali Dodoma ulipitishwa na kuanza kutekelezwa kuanzia mwaka 1974 ambapo hadi sasa imechukua takribani miaka 31. Kama usemi wa kale usemao Roma haikujengwa siku moja, muda huo ni mfupi sana kwa nchi inayoendelea kama ya kwetu na ambayo tangu Uhuru imedhamiria kupambana na maadui ujinga, maradhi na umaskini. Mtakumbuka kwamba nchi kama Australia mbayo imeendelea sana kiuchumi iliweza kuhamisha Makao ya Serikali yake kutoka Melbourne kwenda Canberra kwa takriban miaka 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi cha miaka thelathini ya utekelezaji wa uamuzi huo kwa hali ya nchi yetu ni kifupi sana ukizingatia matukio mbalimbali yaliyojitokeza na kuathiri jitihada zetu za kuinua uchumi katika kipindi kipindi hicho chote cha utekelezaji. Kwa mfano, utekelezaji ulianza na kuendelea vizuri mwaka 1974 hadi 1978 nchi yetu ilipoingia vitani dhidi ya Nduli Iddi Amin. Mwaka 1980 hadi 1985 nchi yetu iliingia katika kipindi kigumu kifedha ambayo tulikosa hata misaada ya wahisani ikiwemo ile kutoka Taasisi za Fedha Duniani mfano, *World Bank* na *IMF).* Miaka ya 1986 hadi 1995 Serikali ilirejea katika makubaliano na Taasisi za Fedha Duniani ili kuweza kujikwamua kiuchumi. Katika kipindi cha Awamu ya Tatu, jitihada kubwa zilifanywa na kuwezesha hali ya uchumi kuanza kutengemaa. Makusanyo ya mapato yameongezeka zaidi ya mara tano na hivi karibuni tumefutiwa madeni ya nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kutengemaa kwa uchumi wetu, Serikali imeweza kuendeleza mipango mbalimbali ya maendeleo nchini ikiwa ni pamoja na usanifu, ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya barabara zikiwemo za zile za Dar es Salaam - Dodoma - Mwanza na Arusha - Babati - Dodoma. Aidha, kwa mafanikio hayo ya uchumi, zinajengwa nyumba Jijini Dar es Salaam na Dodoma kwa ajili ya viongozi mbalimbali wa umma ambapo Dodoma pekee nyumba mpya 300 za daraja la kwanza ziko katika hatua ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama cha Mapinduzi kupitia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 kimeahidi kuongeza kasi kupitia Serikali yake ya Awamu ya Nne kwa kusimamia kwa karibu utekelezaji wa uamuzi huo katika kipindi cha awamu ya mwaka 2005 - 2010. Mambo muhimu yatakayotekelezwa na Serikali ni haya yafuatayo:-

(a) Kuitambua rasmi Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali kisheria na kuweka utaratibu wa Serikali kuhamia.

(b) Kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Iringa - Arusha - Dodoma na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Dodoma - Mwanza kama mkakati wa kuendeleza Mji wa Dodoma ili uweze kuvutia vitega uchumi. *(Makofi)*

(c) Kuweka vivutio kwa sekta binafsi ili ishiriki uwezekezaji kwenye ujenzi wa miundombinu inayohitajika katika ukuaji wa mji na katika uwekaji wa huduma mbalimbali zinazokidhi mahitaji ya watumishi wa Serikali na wananchi kwa ujumla.

(d) Kuongeza kasi ya Wizara za Serikali kuhamia Dodoma, kwa kuwa sasa Serikali inajenga nyumba nyingi za kuishi watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ufafanuzi huo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maelezo niliyotoa hapo juu, zoezi la kuhamishia Makao Makuu ya Serikali Dodoma halijachukua miaka mingi na hivyo siyo jambo la busara kwa wakati huu kutamka rasmi kuwa Bunge litakutana Dodoma na Serikali itaendelea kuendesha shughuli zake Dar es Salaam. Ili kujenga heshima ya Serikali tunapenda kusisitiza kuwa Serikali itaendelea na utekelezaji wa uamuzi huo hatua kwa hatua kadri uwezo utakavyoruhusu. *(Makofi)*

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Serikali zote tangu Awamu ya Kwanza hadi Awamu ya Tatu zimeshindwa, hatua zipi za dhati zitafuatwa na Awamu ya Nne ili kuhamia Dodoma? *(Makofi)*

(b) Je, ni gharama kiasi gani kilichobaki ili kukamilisha ujenzi wa Serikali kuhamia Dodoma? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwenye macho haambiwi tazama na mwenye masikio haambiwi sikia. Jana Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, amethibitishia umma wa Dodoma ikiwa ni pamoja na Mbunge kuwa Serikali imedhamiria kwa dhati kuhakikisha kwamba Makao Makuu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yatakuwa Dodoma na akasema hali hiyo itatekelezwa hatua kwa hatua kufuatana na uchumi wetu. Kwa sababu tumesema hii ni *process* hatuwezi kusema kwamba kiasi kadhaa cha fedha zimebakia kwa sababu uchumi unabadilika na bei za vitu jinsi siku zinavyokwenda zinabadilika. Kwa hiyo, tutakuwa tuna-*review in a rolling plan* ambayo itatekelezwa awamu kwa awamu. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize swali kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Rais jana alipokuwa anahutubia wananchi wa Mkoa wa Dodoma, alithibitisha kwamba msimamo wa Serikali kuhamia Dodoma uko pale na hauna mjadala, je, Serikali haioni umuhimu wa kupanga ratiba ya kuhamia Dodoma? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Degera, kama ifuatavyo:-

Kama tulivyokwisha kusema kwamba upangaji wa ratiba yetu utategemea hali ya uchumi wetu na sisi tutaendelea kupanga kwa utaratibu huo huo kwamba hali itakavyotuwezesha ndiyo hivyo tutakavyohamia na maadamu Rais kasema tutahamia, Mheshimiwa Mbunge awe na uhakika tutahamia. *(Makofi)*

Na. 37

**Kibali cha Kuundwa kwa Wilaya ya Iramba Mashariki**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa ni muda mrefu sasa umepita tangu Serikali iahidi uundwaji wa Wilaya ya Iramba Mashariki na kwa kuwa tatizo kubwa lililokuwa likicheleweshwa utekelezaji huo ni hali mbaya ya uchumi uliokuwepo, lakini sasa inafahamika kuwa uchumi wetu ni mzuri na kwa kuwa tarehe 23 Septemba, 2005 Mheshimiwa Rais alipotembelea Iguguno wakati wa kampeni aliahidi kuunda Wilaya kwa wananchi wa Iramba Mashariki na kwa kuwa Iramba Mashariki ilishatimiza vigezo vyote vya kuwa Wilaya na awali ilikuwa iundwe Wilaya ya Basuto ambayo ingechukua eneo la Iramba Mashariki, Mbulu na Babati jambo ambalo lilishindikana na badala yake ikaundwa Wilaya ya Hanang:-

(a) Je, Serikali, haioni kwamba sasa umefika wakati muafaka wa kuunda Wilaya mpya ya Iramba Mashariki?

(b) Kwa kuwa Serikali inawataka wananchi wake waanzishe miradi yao ya maendeleo na yenyewe isaidie kuchangia nguvu zao na kwa kuwa wananchi wapo tayari kuanza kujenga Makao Makuu ya Wilaya, Halmashauri, nyumba za watumishi na kadhalika. Je, Serikali inasema nini juu ya jitihada hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, uundaji au ugawaji wa maeneo mapya ya kiutawala hapa nchini unatawaliwa na Sheria za Serikali za Mitaa Na. 7, Mamlaka za Wilaya na Sheria Na. 8, Mamlaka za Miji za mwaka 1982 pia Sheria za Uanzishwaji Mikoa na Wilaya Na. 12 ya mwaka 1994. Aidha, viko vigezo ambavyo vinahitajika ili kuunda Wilaya mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa Wilaya ya Iramba inavyo baadhi ya vigezo vinavyostahili kuifanya igawanywe kwani inao wakazi wapatao 161,050 na jumla ya vijiji 58 na bonde la ufa linalowafanya wananchi wapate shida kufuata huduma muhimu Makao Makuu ya Wilaya yaliyopo Kiomboi na Iramba Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuongezeka kwa maombi ya kuanzishwa kwa Wilaya mpya ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Iramba, Ofisi yangu inaendelea kufanya uchambuzi wa kina juu ya suala la maeneo ya Mikoa na Wilaya mbalimbali ili kupata

ufumbuzi wa namna ya kulishughulikia kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa maeneo husika kupata huduma muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugawaji wa Wilaya au maeneo mapya unategemea uwezo wa Serikali kuyajenga Makao Makuu ya Wilaya, kugharamia gharama mbalimbali. Gharama hizo ni pamoja na kuanzishwa kwa Wilaya ambako inakisiwa kiasi cha shilingi bilioni moja kwa kuanzisha Wilaya moja na kuanzisha Mkoa ni shilingi bilioni 4 hadi 6. Hivyo Serikali hugawa maeneo ya utawala kwa awamu kulingana na uwezo wake kifedha.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wananchi wanapoanzisha miradi yao mara nyingi Serikali huwaunga mkono, ijapokuwa ni vema zaidi kuishirikisha Serikali mapema kabla ya kuanza kutekeleza miradi hiyo ili Serikali nayo iweke mipango yake vizuri. Tunafahamu kuwa hivi sasa ziko Wilaya mpya nyingi ambazo zilianzishwa na hazijaweza kukamilisha miundombinu inayokuwa inatakiwa ikiwa ni pamoja na majengo ya Ofisi, nyumba za watumishi na miundombinu mingine. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Iramba wavute subira wakati huu Serikali iendelee na zoezi la kuainisha Wilaya zote zinazohitaji kugawanywa ili kuandaa mkakati na kuangalia uwezo wa kifedha. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hii ni ahadi iliyotolewa na Mkuu wa nchi, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alipohutubia wananchi wa Iramba Mashariki tarehe 23 Septemba, 2005 na jana wakati akihutubia wananchi wa Dodoma alisema kwamba atahakikisha ahadi zote zilizotolewa zinatekelezwe. Je, hii itakuwa miongoni mwa ahadi zile muhimu za kwanza kutekelezwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais kwamba ahadi zote ambazo tumeahidi sisi Wabunge pamoja na yeye zitatekelezwa kwa awamu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira nalo hilo litapewe kipaumbele wakati wa kutekeleza hizo ahadi zetu kwa mwaka wa 2005 mpaka 2010. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vigezo vya kuanzishwa Wilaya mbalimbali kama alivyotaja Naibu Waziri ni vigumu kwa Wilaya nyingi kuvifikia ikiwemo na majengo na maeneo mbalimbali ili Wilaya hizo zianzishwe. Lakini kwa kuwa Wilaya ya Nzega imeomba kuwa Mji kwa muda mrefu na majengo yapo. Je, Waziri yupo tayari kutamka ni lini kwa kuwa kigezo cha majengo yapo, Mji wa Nzega utapata hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji kwa kuwa sasa hivi ni kijiji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa hivi sasa inafanya tathmini mbalimbali ya kuangalia Halmashauri za Miji, ambazo zitaanzishwa mojawapo ni Halmashauri ya

Wilaya ya Nzega nayo inafanyiwa tathmini. Tukishafanya tathmini namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba yale ambayo tutayaweza tutatekeleza kwa awamu kama nilivyosema kwenye swali la awali. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali linalotokana na swali la msingi aliloluliza Mheshimiwa Mgana Msindai.*(Makofi)*

Wakati akitoa majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri, takwimu aliyoitoa anasema Wilaya ya Iramba ina vijiji 58. Hivyo vijiji vinavyosema 58 si takwimu sahihi kwa sababu Iramba tayari ina vijiji vinavyopata karibu 102 kwa sababu Iramba Magharibi, peke yake ina 67 na wakazi waliotaja ni 160,000.

Sasa naomba Mheshimiwa Waziri anieleze kwamba hili tatizo linalozungumzwa la kuigawa Wilaya linatupa kero sana kwa sababu tunayo maeneo kwa Iramba Mashariki, ambayo yanaweza yakahimili na kufanya Wilaya ikaundwa. Kwa hiyo, naomba atueleze ni muda gani Wilaya itapatikana Iramba Mashariki?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoahidi na kama tulivyojibu kwenye swali la awali kwamba hayo masuala ya kugawa Wilaya yatakwenda kwa awamu na baada ya kufanya tathimini, Rais kuridhia na kutangazwa kwenye gazeti na kuwekwa kwenye mipango yetu ya Bajeti. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge hatuwezi kusema tutafanya lini, lakini baada ya tathimini tutahakikisha kwamba hili suala tunalitatua. Ahsante. *(Makofi)*

N. 38

**Sekta ya Uvuvi**

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa sekta ya uvuvi ni chanzo kikubwa cha mapato ya wavuvi waishio kandokando ya Ziwa Tanganyika; na kwa kuwa wavuvi hao huvua kwa nyenzo zilizopitwa na wakati na hawana uhakika wa soko la samaki wanaovuliwa:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kuwa wavuvi hao wanapata nyenzo za kisasa za uvuvi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani katika kuhakikisha wavuvi hao wanapata soko la uhakika kwa bidhaa zinazovuliwa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Mradi wa Uwiano wa kuhifadhi Mazingira ya Ukanda wa Ziwa Tanganyika, mradi huo utahusisha nchi nne za Burundi, Zambia, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo na Tanzania mradi unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Mkopo huo ni wa *USD 7.4 million* na mchango wa Serikali ni *USD 88,786.*

Mradi huo uliowekwa sahihi Novemba, 2004 na utekelezaji wake utaanza rasmi mwezi Mei, 2006 baada ya taratibu za msingi kukamilika. Mradi huo ni pamoja na wa uhifadhi wa mazingira ya Ziwa Tanganyika, mafunzo kwa wavuvi, miundombinu, huduma ya ushauri na maendeleo ya uvuvi ambapo mikopo itatolewa kwa wavuvi wadogo wadogo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, soko la samaki nchini bado ni kubwa sasa ikizingatiwa kuwa kiasi cha samaki kinachovuliwa ni kidogo ikilinganishwa na kasi ya kuongezeka kwa idadi ya watu nchini. Hata hivyo kiasi kikubwa cha samaki kinachovuliwa ni dagaa ambao wana soko zuri nchini na nje ya nchi. *(Makofi)*

Katika kipindi cha mwaka 2003 - 2005 jumla ya kilo 109,229.20 za dagaa na samaki wa mapambo 14,456 viliuzwa nje ya nchi kwenye nchi za Burundi, Jamhuri ya Kongo, Rwanda na Zambia kwa thamani ya jumla ya shilingi 1,553,414,810.50 na kuliingizia Taifa ushuru wa shilingi 93,204,699.05.

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 wavuvi walipatiwa mafunzo juu ya uhifadhi bora wa samaki ili kuboresha kiwango cha ubora wa samaki hao jambo ambalo litawapatia wavuvi soko na bei nzuri zaidi. Mafunzo hayo pia yatasaidia katika kupunguza kiwango cha samaki wanaopotea kwa kuharibika. Pia Serikali itahamasisha wawekezaji watakaochakata samaki ili kupata bidhaa zinazoongezewa thamani na hivyo kuwaongezea wavuvi soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutangaza soko la samaki na mazao mengine ya uvuvi, Serikali imeanzisha tovuti ya sekta ya uvuvi *www.fisheries.go.tz* ambayo itatumika kutoa taarifa mbalimbali za sekta ikiwemo taarifa za uzalishaji wa samaki na mazao yake. Kuweko kwa tovuti hii kutawezesha kutangazwa kwa samaki wanaovuliwa nchini ikiwemo samaki wa Ziwa Tanganyika na hivyo kupanua wigo wa soko. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kuwa Serikali inapata mapato kutokana na dagaa. Je, haoni kama kuna umuhimu wa kujenga kiwanda cha samaki na dagaa Mkoani Kigoma ili kiweze kuwaongezea kipato zaidi wavuvi wa Mkoa wa Kigoma? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu msingi nimesema kuwa kuna mkakati ambao Serikali itahamasisha wawezekaji watakaochakata samaki ili kupata bidhaa zitakazoongezewa thamani na hivyo kuongeza wavuvi wa soko. Hii ina maana kwamba Serikali pia itatafuta wawezekaji ambao wataweza kufanya shughuli hiyo. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, katika swali la msingi ambalo linazungumzia wavuvi wa Ziwa Tanganyika matatizo yao yako sawa kabisa na wavuvi wa Ziwa Victoria. Kwa kuwa wavuvi walioko katika Ziwa Victoria, wanapambana na tatizo kutosaidiwa nyenzo za kuvulia na kupewa bei ambayo haiendani na gharama ya uzalishaji na kwa kuwa baadhi ya wafanyabiashara wenye viwanda vya samaki wamekuwa wakitumia nafasi ya kufanya biashara kwao kuwanyanyasa wavuvi wadogo. Je, Serikali inaweza ikawasaidiaje wavuvi hawa wa Ziwa Victoria ambao wanapata matatizo kama hayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la nyenzo za kuvulia kwa wavuvi wa Ziwa Victoria, kwa kweli linafanana na wavuvi wa Ziwa Tanganyika. Tatizo kubwa lililopo ni kwamba wavuvi kwa kawaida huwa wana utamaduni wa kila mmoja kuvua peke yake. Hivyo Serikali inapendekeza kuwa wavuvi wakati umefika sasa ni bora waungane wawe katika vikundi ili waweze kusaidiwa kupata mikopo mbalimbali. Kwa kuungana kuwa katika vikundi hawatanyanyaswa na wale wavuvi wakubwa. *(Makofi)*

Na. 39

**Vivutio vya Utalii**

**MHE. KABWE Z. ZITTO** aliuliza:-

Kwa kuwa utalii ni sekta muhimu katika uchumi wa Tanzania na kwa kuwa Mkoa wa Kigoma ni moja kati ya Mikoa yenye vivutio vya utalii na hasa kupitia Mbuga ya Gombe:-

(a) Je, ni watalii wangapi walitembelea Mkoa wa Kigoma katika kipindi cha mwaka 2000 - 2005?

(b) Je, ni watalii wangapi walitembelea Mbuga ya Gombe katika kipindi hicho hicho nilichotaja?

(c) Je, wananchi wa Kijiji cha Mwangongo, Bubago na Mtanga Mkoani Kigoma wanafaidika vipi na utalii huo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya watalii wanaotembelea Mkoa wa Kigoma, imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka watalii 2,391 mwaka 2000 hadi Septemba, 2005 jumla ya watalii 22,701 walikuwa wametembelea vivutio vilivyopo

Mkoani Kigoma kupitia vituo vya Bandari za Kigoma, Kibirizi, Manyovu, Mabamba, Ujiji, Kagunga na uwanja wa ndege wa Kigoma.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya watalii 3,926 walitembelea Hifadhi za Taifa ya Gombe katika kipindi cha kuanzia mwaka 2000 mpaka mwaka 2005. Kati ya hao, watalii wageni walikuwa 2,868 na watalii wenyeji walikuwa 1,058.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kuwa mapato yamekuwa yakiongezeka kutoka shilingi 80,900,325.00 mwaka 2003 hadi kufikia shilingi 123,037,750.00 mwaka wa 2005.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia utekelezaji wa Mpango wa Ujirani Mwema *(outreach programme)* katika kipindi kilichoanzia mwaka 1998/1999 hadi mwaka 2003/2004, kijiji cha Mtanga kilipatiwa msaada wa shilingi 4,502,780.00 na Mwamgongo walipatiwa shilingi 2,727,000.00 kwa ajili ya kujenga madarasa. Mwaka 2001 mpaka 2002 kijiji cha Bubango kilipewa jumla ya shilingi 8,553,440.00 na mwaka 2005/2006 kijiji cha Mgongo kilipewa shilingi milioni 11,263,000.00. Fedha hizo zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu katika vijiji vyote viwili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika kipindi hicho, Shirika lilichangia jumla ya shilingi 27,046,220.00 kwa ajili ya kusaidia miradi ya wananchi katika vijiji vya Mtanga, Mwamgongo na Bubango katika mkoa wa Kigoma.

Aidha, wananchi na viongozi wa vijiji hivyo kwa nyakati tofauti wamekuwa wakipewa fursa ya kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Gombe na kupata elimu kuhusu umuhimu wa kuhifadhi wanyapori na kuhifadhi mazingira kwa jumla.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ambayo yamefanyiwa utafiti, majibu mazuri sana na pia kwa mujibu wa taarifa za vyombo vya habari nimepata taarifa kwamba tayari umeshatembelea Mkoa wa Kigoma na Mbuga ya Gombe, nakupongeza sana kwa hili. Lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kufahamu Mbuga ya Gombe inaajiri Watanzania wangapi kutoka katika vijiji vya Mwamgongo, Bubango, Mtanga na Chankele?

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali langu la pili ni kwamba, sasa hivi tunafahamu kwamba utalii una *product* nyingi na moja ya *product* ni *community base tourism,* Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wanavijiji wa vijiji hivi vya Mtanga, Chankele, Bubangwa na Mwamgongo wanashirikishwa katika *community base tourism* ili pesa zinazotokana na utalii ziweze kubaki Mkoani Kigoma na kuondoa umaskini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kabwe Zitto, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoeleza mwenyewe Mheshimiwa Mbunge kwamba nilitembelea Hifadhi ya Gombe na katika mambo ambayo nilikuwa nimependa kuyafahamu ni kuhusu ajira za wafanyakazi ambao wapo Gombe kwa kuwa hiyo ni moja ya maagizo ambayo yako katika sera ya Utalii ya Taifa. Taarifa niliyokuwa nayo ni kwamba Hifadhi ya Gombe inashirikisha sana wananchi ambao wanaishi katika vijiji jirani. Gombe kuna ajira za aina tatu, kulikuwa kuna ajira ya kudumu. Katika ajira ya kudumu nafurahi kumfahamisha Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwamba walikuwepo wananchi ambao wanatoka katika vijiji vya jirani, siwezi kukumbuka kwa usahihi lakini ilikuwa kati ya wanavijiji sita mpaka tisa. Lakini vile vile kuna ajira ya muda, hiyo nayo pia iliweza kuajiri wanavijiji wanaotoka katika vijiji vya jirani na hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilipofika katika Hifadhi ya Gombe nilikuta ujenzi wa jengo ambalo linategemewa kuwa nyumba ya kulala ya watalii watakaotembelea Hifadhi ya Gombe na pale nilikuta wafanyakazi wengi wanakaribia 60 na wote hao walikuwa ni wajenzi na wasaidizi wa ujenzi, lakini wanatoka katika vijiji vya jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nilifarijika zaidi wakati nikiongea na wafanyakazi hao walikuwepo pia wanafunzi, kama nakumbuka vizuri kati ya wanne na watano ni wanafunzi wa shule za sekondari ambao wazazi wao wana kipato kidogo kwa hivyo walikuwa wanajihusisha na kazi hizo na wanapata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili la nyongeza linalohusu *community base tourism,* napenda kumfahamisha Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwamba mpango huo tunao na ulianza kama majaribio. Ulianza katika Wilaya ya Monduli vile vile katika kijiji cha Mto wa Mbu, Gezaulole na vilionekana kwamba vina manufaa makubwa sana kwa wananchi na pia napenda kukufahamisha kwamba mradi huo uliweza kupata tuzo mjini Berlin kwa jinsi ulivyoweza kushirikisha wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kutokana na majibu marefu, tunahama Wizara tunaenda Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Na. 40

**Mfuko wa Udhamini kwa Wafanyabiashara Wadogo na wa Kati**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeamua kuanzisha mfuko wa kudhamini mabenki na taasisi za fedha kwa ajili ya mikopo ya kuwadhamini wafanyabiashara wadogo na wa kati; na kwa kuwa tayari Serikali imeshaanza kuteua taasisi za kibenki za kushughulikia udhamini wa mfuko huo ambapo nyingi kati ya taasisi hizo ni mabenki makubwa na

mabenki hayo mengi yako Dar es Salaam na labda katika Makao Makuu ya baadhi ya Miji makubwa mfano *EXIM Bank* na kadhalika:-

(a) Je, kwa nini Serikali isiamue tu kwa makusudi kutoa udhamini wa kupitia *SCULT* au vyama vya wananchi vya akiba na kukopa mikopo ambapo huko wananchi wafanyabiashara, wakulima na wafugaji wadogo waliko na wanahitaji sana uwezeshaji huo?

(b) Je, ni lini Serikali itaacha kuyatumia mabenki makubwa na yenye masharti magumu yasiyofikika na Watanzania wengi katika mipango yake ya uwezeshaji jamii?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni makubwa ya kuanzisha mfuko wa udhamini ni ili kuwezesha mabenki kuongeza utoaji wa mikopo kwa sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo kwa kutambua kuwa mikopo itakayotolewa na taasisi za fedha kwa ajili ya sekta itadhaminiwa. Serikali iliutangaza utaratibu huu katika magazeti na kuwaalika mabenki yaliyopenda kushiriki kuwekeana mkataba na Benki Kuu ya Tanzania ili kuweze kunufaika na udhamini. Mlango bado upo wazi kwa benki yoyote kushiriki. Benki zilizoonyesha nia ya kushiriki ni 17 japo mpaka sasa ni benki 14 zimekamilisha taratibu zote. Aidha, mikopo ya dhamana ya shilingi 400 milioni inashughulikiwa na mabenki mbali mbali chini ya mfuko kwa dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa chombo cha *SCULT* na vyama vya kuweka na kukopa vina utaratibu mzuri, mwepesi na wa haraka wa kutoa mikopo kwa wanachama wake, haikuonekana haja ya kutoa udhamini kwa vyombo hivyo kupitia Benki Kuu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa masharti ya baadhi ya mabenki ni magumu, hali inayofanya wananchi wengi kushindwa kunufaika na huduma za kifedha zinazotolewa na taasisi hizo. Mikakati inayochukuliwa na Serikali kurahisisha upatikanaji wa mikopo kutoka taasisi hizo ni pamoja na:-

- Utaratibu unaendelea wa kurasimisha mali ya wananchi ili kuwewazesha kuwa na dhamana;

- Mfuko wa dhamana ya mikopo kama huu tuliouzungumzia unaosimamiwa na Benki Kuu; na

- Utoaji wa mafunzo kwa wajasirimali ili wawe na uwezo wa kuandaa miradi inayokopesheka na kadhalika. Aidha, programu ya *Financial Sector Deepening Trust* inalenga pia kuainisha vikwazo vinavyofanya wananchi

kutonufaika na mabenki na kuandaa mafunzo kwa mikakati ya kurekebisha hali hiyo.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa lengo la Serikali katika nchi yetu ya Tanzania ni kuhakikisha kwamba wananchi wanaondokana na umaskini unaowakithiri na kwa kuwa wengi wa wamaskini na wazalishaji wakuu wako katika maeneo ya vijijini na huko ndiko tunakofikiria kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kubadilisha mazao yao kuwa katika mfumo mpya wa biashara huria.

Je, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kudhamini wafanyabiashara hao wadogo wadogo katika maeneo ya vijijini kupitia vyama vyao hivyo vya akiba na mikopo ambavyo ndivyo wanavyo wao kule kila siku?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili ni kwamba kwa kuwa sasa hivi mabadiliko ya sera na mabadiliko ya sheria mbalimbali zinazohusu masuala ya fedha yamekuwa yakilenga zaidi kwenye mabenki haya ambayo mengi yako katika maeneo ya miji mikubwa na katika maeneo ya mijini na kwa kuwa wakulima, wafugaji na wafanyabiashara wadogo wadogo wanahitaji sana huduma hiyo kwa udhamini rahisi.

Je, Serikali sasa haifikirii, basi ianzishe benki ya wakulima au benki ya wafanyakazi au benki ya wafanyabiashara wadogo wadogo ili udhamini huu uwapate hasa katika maeneo yaliyopo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Kwanza kudhamini vikundi kama *SCULT* na *SACCOS,* kwa sababu mfuko huu wa kudhamini siyo kwamba pesa inatoka benki inakwenda mabenki hayo tunayoyazungumza. Tunaposema dhamana ina maana unakwenda kwenye benki, benki inatumia pesa zake isipokuwa kwa sababu wewe huna dhamana, Benki Kuu inakudhamini siyo kwamba hela inatoka Serikalini au Benki Kuu inakwenda kwenye hayo mabenki. Kwa sababu hizi *SCULT* na *SACCOS* ni vikundi vya watu wanaojuana, huwa hawapendi dhamana, mtu aweke dhamana ndio amkopesha ndio sababu hapakuwepo dhamana kutoka Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pili mabenki yako mjini na hayafikiki kwa urahisi, sasa hivi kuna programu ambayo nimeizungumza ambayo inaitwa *Financial Sector Deepening Trust,* ambayo programu hiyo inafadhiliwa na *DFDI* ya Uingereza, *SIDA* ya Sweden, Uholanzi na *SIDA* ya Canada. Madhumuni ya programu hii ni kutoa mafunzo yanayolenga kuimarisha uwezo wa taasisi za kifedha zinazohudumia wateja wadogo wadogo zikiwemo hizi *SCULT* na *SACCOS,* kutoa msaada unaolenga kuwezesha taasisi kubuni huduma mpya kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo, kutoa msaada

utakaowezesha kuangalia upya sera, mfumo wa sheria unaozuia utoaji wa mikopo midogo midogo na mwisho kusaidia mikakati inayolenga kuongeza upatikanaji mitaji kwa ajili ya sekta ya viwanda vidogo vidogo.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tulikuwa na Benki ya *NMB* ambayo ilikuwa inasaidia sana wananchi wa vijijini na kipindi kilichopita tulipingana na Serikali sana katika kubinafsisha benki hii na sasa naomba nikubali kwamba maji yameshamwagika. *(Makofi)*

Je, Serikali hii ya Awamu ya Nne ina mkakati gani wa kujitahidi kuanzisha benki yenye sura kama ya *NMB? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali lililoulizwa na Mheshimiwa Anne Malecela, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya Serikali sasa hivi si kufanya biashara ila kuwezesha kuweka miundombinu au kuweka taratibu ambazo zinawasaidia wafanyabiashara kufanyakazi kwa urahisi. *NMB* imebinafsishwa lakini imepewa masharti katika ubinafsishaji wake na mpaka sasa hivi wakati wa kubinafsishwa asilimia kubwa ya hisa za *NMB* ziko mikononi mwa Serikali au Watanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali itahakikisha kwamba madhumuni yaliyokuwa yameanzisha *NMB* na taratibu zilizowekwa wakati inabinafsishwa yanatakelezwa kusudi iweze kuwahudumia hao wateja wadogo wadogo kama walivyobainisha wakati wanataka kuinunua hiyo *NMB. (Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa Serikali imeanzisha mpango mzuri wa udhamini wa wananchi kupitia Benki Kuu. Je, ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba taarifa hizi zinawafikia wananchi wote vijijini ili mtu ambaye anapenda kudhaminiwa na Serikali aweze kupata huo udhamini?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, linalohusu namna taarifa kufika kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri na nyie Waheshimiwa Wabunge mmeona Serikali kwa kipindi kirefu ilikuwa ikitangaza kwenye magazeti dhamana hii tuliyoitangaza, dhamana ya Benki Kuu kudhamini vikundi vidogo vidogo.

Lakini kama sisi Waheshimiwa Wabunge tunatambua kwamba labda magazeti au redio wakati mwingine hazifiki kwenye vijiji na vitongoji vyetu. Kwa hiyo, tunatumia nafasi hii kuwaomba Wabunge na wenyewe wakati wa kuzunguka majimboni kwao watangaze huu mfuko na fursa zinazotolewa na Serikali kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo. *(Makofi)*

Na. 41

**Kivuko cha Pangani**

**MHE. MOHAMMED R. ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa kila baada ya miaka mitano Kivuko cha Pangani kimefikia kiwango cha kutokutoa huduma zake kama kawaida kutokana na uchakavu unaojitokeza kutokana na mazingira ya maji chumvi katika eneo hilo; na kwa kuwa Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa *Ferry* mpya na kubwa zaidi lakini sasa muda umepita na hali ya kivuko inahatarisha maisha ya watumiaji na mali zao.

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya upatikanaji wa kivuki kipya?

(b) Je, ni nini mpango wa Serikali juu ya kuweka mkakati wa kudumu katika eneo la kivuko hicho?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kivuko cha Pangani chenye ukubwa wa tani 35 kina uwezo wa kubeba magari makubwa manne na abiria 100 kwa safari moja. Kivuko hiki hutoa huduma kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa moja usiku. Pia huunganisha mji wa Pangani na sehemu nyingine za Wilaya ya Pangani. Aidha, kivuko cha Pangani kina usalama wa kutosha kwa watumiaji na mali zao kwani hufanyiwa matengenezo ya kawaida ya mara kwa mara yaani *periodic maintenance.*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za ununuzi wa kivuko kipya cha Pangani tayari zimeanza baada ya Benki ya Dunia kukubali ununuzi wa kivuko hicho. Zabuni ya ununuzi wa kivuko hicho ilitangazwa kwenye gazeti la *Daily News* tarehe 18 Januari, 2006. Mwisho wa kupokea zabuni ni tarehe 21 Machi, 2006. Aidha, kivuko hicho kitakuwa na uwezo wa kubeba tani 50.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuboresha huduma ya kivuko cha Pangani ikiwa ni pamoja na kuweka uzio sehemu ya kupumzika abiria, pamoja na vyoo pande zote mbili. Mipango hii itaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2006/2007, kutegemea upatikanaji wa fedha za bajeti kila mwaka.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba taarifa ya kwamba kivuko cha Pangani kiko katika hali ya usalama kwa wananchi na mali zao siyo sahihi. Hali ya kivuko cha Pangani ni mbaya sana pamoja na *periodic maintenance* inayofanyika.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri upo tayari kuja Pangani uthibitishe haya ninayoyasema?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, anafahamu kwamba Kivuko cha Pangani ni kiungo muhimu siyo tu kwa wananchi wa Pangani lakini vile vile kiusalama, kinchi ni muhimu sana. *(Makofi)*

Je, Serikali inaweza ikaharakisha utaratibu mzima wa kufungua barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda hadi mpaka wa Kenya ili iwe inapitika kiurahisi na kiusalama kwa nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwanza niko tayari kwenda kukagua kivuko hicho na kuona matatizo yaliyokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la umuhimu wa kivuko hiki nakubaliana naye kabisa kwamba kivuko ni muhimu na ndio maana katika jibu la msingi tumesema tunanunua kivuko kingine kipya na nimesema *tender* au zabuni za ununuzi huo zinafunguliwa tarehe 21 Machi, 2006 kwa hiyo, ni chini ya miezi miwili ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli kivuko kilichopo hali si nzuri na kimekuwa kikifanyiwa matengenezo ya mara kwa mara na hata sasa hivi ninavyozungumza matengenezo hayo au *periodic maintenance* mengine yanaendelea na kwa ujulisho ni kwamba kwa sasa kivuko hicho kimesimama kwa ajili ya matengenezo hayo na kinachoendelea kufanywa sasa hivi ni kutengeneza ukarabati mdogo wa bodi pamoja na ku-*overhaul engine* na kwa sasa wananchi na mizigo yao wanahudumiwa na kwa kutumia Kivuko cha Amboni kinachomilikiwa na *Amboni Estates.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ambayo ameizungumzia hii ni barabara ambayo hata Wizara inajua kwamba ni muhimu na taratibu za kujenga barabara

hiyo kwenda kwenye mpaka wa Kenya ziko katika *long term plan* ambayo Serikali ikipata fedha barabara hiyo itajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MHE. MWINCHUMU A. MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa wakazi wa Kigamboni, Jimbo la Kigamboni hivi sasa wana usumbufu mkubwa wa kivuko cha *ferry,* Wizara inajua hilo?

(b) Je, Wizara ina mpango gani kuifanyia matengenezo *(service)* boti mbili zilizopo *MV Magogoni* na *MV Kigamboni* kwa sababu takriban miaka 10 sasa hivi vinafanya kazi bila kufanyiwa *service*.

Je, Wizara ina mpango gani? Hivi sasa kuna usumbufu mkubwa kwa wanakigamboni haswa katika misongamano ya magari, uwezo wake wa kutembea kutoka ng'ambo hadi ng'ambo umepungua sana na kusababisha foleni kubwa?

(c) Je, Wizara ina mpango gani wa kuweza kununua boti mpya ili kuepusha matatizo yote hayo?

**SPIKA:** Waziri atajibu swali moja tu.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchumu Msomi, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, najua sana matatizo ya kivuko hicho na ndio maana kama ulisoma kwenye vyombo vya habari niliweza kukaa pale masaa mawili kukagua matatizo ya kivuko kile toka saa 12.30 asubuhi mpaka saa 02.30 asubuhi na ninaelewa vizuri tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kivuko kile au vivuko vile vyote viwili vina matatizo na kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikitafuta fedha za ukarabati na kivuko hiki kiko katika mpango wa kurabati vivuko vitano kwa nchi nzima mradi ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Kwa sasa tulichokuwa tunangoja ni *no objection* kutoka Benki ya Dunia, tumeipata na tangazo la kumtafuta mzabuni kwa kutengeneza kivuko hicho litatangazwa tarehe 15 Februari, 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tatizo hilo linashughulikiwa wakati tukiendelea na mikakati ya kununua kivuko kipya na vile vile suala zima la kujenga daraja la kwenda Kigamboni. *(Makofi)*

Na. 42

**Huduma kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu**

**MHE. SUSANA A. J. LYIMO** aliuliza:-

Kwa kuwa elimu ndio msingi wa maendeleo kwa binadamu yeyote; na kwa kuwa Serikali kwa makusudi imeona umuhimu wa elimu ya juu na hivyo kuongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu hususan Chuo Kikuu cha Dar es Salaam:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kuwa wanafunzi hao wanapata huduma bora kama vile malazi kwani sasa hivi wanafunzi wanalala wanne katika chumba kimoja ikizingatiwa kuwa ni watu wazima?

(b) Serikali ina mpango gani kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapatiwa madarasa *(Lecture Theatres)* kwani inasikitisha kuona wanafunzi wakisikiliza wahadhiri wao wakiwa nje ya madarasa hali inayofanya washindwe kufuatilia vizuri kinachofundishwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susana Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa elimu ya juu imeagiza vyuo vikuu vyote vya umma nchini kuongeza idadi ya wanafunzi vyuoni. Katika kuongeza idadi ya wanafunzi, Serikali kupitia Bajeti ya Maendeleo, Mfuko wa Elimu pamoja na mapato ya vyuo imekuwa ikihakikisha kuwa ongezeko hilo la wanafunzi linaenda sambamba na upanuzi au ujenzi wa miundombinu muhimu kama madarasa, vyumba vya mihadhara, maktaba, maabara na mabweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Serikali iliweza kujenga mabweni sehemu ya Mabibo yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 4,000. Aidha, Chuo kilikamilisha ujenzi wa vyumba viwili vya mihadhara vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa kila kimoja.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Chuo Kikuu kinaendelea na ujenzi wa vyumba viwili vya mihadhara vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kila kimoja.

Uwezo wa Serikali bado ni mdogo na hivyo kipaumbele kimewekwa katika ujenzi wa madarasa, maabara, maktaba na vyumba vya mihadhara. Tunatoa wito kwa wananchi, mashiriki ya kidini na mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na sekta binafsi kwa ujumla kuwekeza katika kujenga mabweni ya wanafunzi katika Vyuo Vikuu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba kuna matatizo ya huduma za wanafunzi hasa malazi na kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameahidi kujenga

Chuo Kikuu kipya, je, Wizara haioni umuhimu wa kukarabati au kupanua sehemu za malazi ya wanafunzi kuliko kujenga chuo kipya kwa sasa hivi?

Pili, kwa kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinalenga kwenye mambo makuu matatu yaani *research, consultation and teaching* na kuacha kabisa suala la malazi na pia tuna uhakika kwamba wanafunzi wengi wa Chuo Kikuu hasa wasichana wamekuwa wakikosa malazi na hivyo kuishi maisha ya hatari kwa afya zao, je, Wizara haioni umuhimu wa kujenga mabweni ya wanafunzi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianzie swali la pili. Kama nilivyojibu katika swali la msingi, Serikali inatambua umuhimu wa mabweni na nafasi ambazo wanafunzi wanatakiwa kuzipata katika mabweni, lakini kipaumbele tumetoa katika madarasa, maabara na vyumba vya mihadhara kwa sababu kati ya hivyo vitu viwili unapokuwa huna pesa za kutosha ni vizuri ukawa na madarasa ambapo mabweni wanafunzi wanaweza kujitafutia malazi popote wakaja kusoma katika Chuo Kikuu. Lakini hata hivyo, huo umuhimu unatambulika na vyuo husika vinafanya kila jitihada kwa kutumia Mamlaka ya Elimu Tanzania kukopa fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu mingine. Nimesema tunaalika watu binafsi, mashirika kuwekeza katika vyumba vya mabweni Chuo Kikuu ambapo mtapata fedha nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Chuo Kikuu kipya, ni kweli kwamba ni vizuri kutengeneza miundombinu kwa kukarabati Vyuo Vikuu vilivyopo kuliko kujenga kipya. Lakini hili la kujenga Chuo Kikuu kipya limo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala. Kwa hiyo, ni agizo na hiki chuo lazima kijengwe. Pamoja na kujengwa ukarabati utaendelea kufanywa katika vyuo vikuu vingine kwa kuongeza nafasi na kutengeneza miundombinu mingine ya kuwezesha kujifunza kwa ufasaha.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupewa nafasi hii. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, je, haoni sasa ni wakati muafaka Vyuo vya Elimu ya Juu kuanza kufanya *double* au hata *triple sessions* ili wanafunzi watumie madarasa hayo hayo na maabara hizo hizo na badala yake Serikali ikajikita katika kuwaandaa wataalam au walimu wa kufundisha?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *double session* sio suala la kuamua na kujibu sasa hivi, ni suala ambalo linahitaji kuwasiliana na vyuo husika kwa sababu kila chuo kina mipango yake na *capacity* kulingana na wafanyakazi waliopo katika chuo hicho.

Na. 43

**Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi *Marine* - Zanzibar**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa uko mpango mzuri wa kujenga Chuo Kikuu cha Sayansi *Marine* huko Buyu, Zanzibar na hatua za mwanzo za kulipata eneo hilo ziko tayari:-

(a) Je, ujenzi huo utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taratibu za kuanza ujenzi wa Taasisi ya Sayansi za Bahari huko Buyu Zanzibar zimekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza wakati wowote kuanzia sasa. Jiwe la msingi liliwekwa na Mheshimiwa Fredrick Sumaye, tarehe 11 Januari, 2004. Aidha, Msanifu *(Architect)* pamoja na Mkandarasi ambaye ni *China Railway Jianchang Engineering Co. Ltd.* wamekwishateuliwa. Tayari Mkandarasi amekwishafika katika eneo la ujenzi na kinachosubiriwa ni kukamilisha taratibu za kutiliana saini Mkataba ili ujenzi uanze.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa dhamira ya ujenzi huo wa chuo hicho cha Sayansi *Marine,* Zanzibar ulikuwepo miaka 20 iliyopita na walikuwa wameshateua mahali pa ujenzi sehemu ya Mkokotoni, Mkoa wa Kaskazini Unguja na waliwahi kujenga nyumba moja sehemu hiyo, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana na mimi kwa sababu masafa yanayotoka Mkokotoni na Buyu ni mbali sana, kuitoa nyumba ile kuikabidhi Serikali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lililotengwa la Buyu linatosha kabisa na haliko mbali na eneo analolizungumzia. Kwa kuwa hatua za kujenga chuo hicho zimeshakamilika kama nilivyosema hakuna sababu ya kuhangaika na eneo tofauti na hili ambalo tayari hatua zimeshafika karibu na mwisho kujenga chuo hicho.

Kwa sasa hivi mahali wanapotumia pale mjini kuna miundombinu ambayo inatosheleza kwa wakati huu. Mimi nilifikiri nia yake ni kujua kwa nini mpaka sasa chuo hakijajengwa katika eneo la Buyu ni kwamba ujenzi utaanza wakati wowote kuanzia sasa hivi kwa hatua ambazo nimemshamweleza. *(Makofi)*

Na.44

**Ruzuku kwa Mbolea**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali pamoja na nia njema ya kutoa ruzuku ya mbolea kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, ukiwepo na Mkoa wa Mbeya:-

(a) Je, Serikali inayo habari kuwa ni wakulima wachache wanaopata mbolea hiyo?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuongeza kiasi cha ruzuku hiyo na kuhakikisha kuwa mbolea hiyo inawafikia wakulima wengi zaidi ili waongeze ari ya uzalishaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ilianza kutoa ruzuku ya mbolea mwaka wa 2003/2004 ambapo tani 33,492 zilifidiwa kwa gharama ya shilingi bilioni 2.0. Kiasi hicho kilipelekwa katika Mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini. Katika mwaka 2004/2005, Serikali iliongeza fedha za ruzuku kwa mbolea kufikia shilingi bilioni 7.244 ili kupanua wigo wa kusambaza mbolea yenye ruzuku kutoka Mikoa minne hadi kufikia Mikoa yote Tanzania Bara. Jumla ya tani 74,773 za mbolea zilifidiwa.

Kutokana na ruzuku hiyo, matumizi ya mbolea yameongezeka nchini kutoka tani 92,658 mwaka wa 2003/2004 hadi kufikia tani 112,000 mwaka wa 2004/2005. Kwa wakati huu, mahitaji ya mbolea inayopata ruzuku ni makubwa sana ikilinganishwa na uwezo wa bajeti ya Serikali. Kwa mfano, katika mwaka 2005/2006, mahitaji ya mbolea yenye ruzuku ni tani 174,082 wakati Bajeti iliyotengwa inatosha kufidia tani 63,840 tu. Mkoa wa Mbeya peke yake umeomba kutengewa tani 20,708 za mbolea yenye ruzuku lakini umepata tani 14,275 za mbolea hiyo. Hivyo, Serikali ina habari kwamba Mkoa wa Mbeya pamoja na Mikoa mingine unapata mbolea pungufu yenye ruzuku ikilinganishwa na mahitaji ya wakulima kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali.

(b) Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge unazingatiwa katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 Ibara ya 31(d) inayosema: "...Aidha, utaratibu wa Serikali kutoa ruzuku ya mbolea utaimarishwa na kulenga zaidi kwenye kukuza uzalishaji katika kilimo, kuliko manufaa ya biashara pekee..." Tunategemea utekelezaji wa Ilani utaanza kujitokeza katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2006/2007 na katika miaka inayofuatia.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa hivi sasa Taifa letu linakabiliwa na njaa kali katika baadhi ya maeneo katika nchi hii, Mbeya tumebahatika kwamba mpaka sasa hivi mvua zinanyesha bila matatizo. Kwa kupitia mpango wa dharula, Serikali itakuwa tayari kupeleka mbolea za ruzuku ili kuimarisha uzalishaji kwa kipindi hiki kwa Mikoa hii ya Nyanda za Juu Kusini?

Pili, kwa kuwa pamoja na pengo kubwa la mbolea ya ruzuku lakini uko ukorofi kutoka kwa wafanyabiashara na wakala wa mbolea hizi kuficha mbolea na hatimaye kuziuza kwa bei ya juu, Serikali inatamka nini katika hili?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu kupeleka mbolea kule Mkoa wa Mbeya hivi sasa kwa sababu hali ya hewa ni nzuri, kusema kweli kipindi cha kuweka mbolea kwenye mazao tayari kimekwishapita. Kwa hiyo, hata tungejaribu kufanya hivyo, kipindi kile kimeshapita kwa sababu mvua zilipoanza na *timing* ya mbolea muda umekwishapita, siamini kama itasaidia sana. Kitaalam inaonekana haiwezekani kwa sababu kuna mbolea ya kupandia na kukuzia na majira ya mbolea ya kupandia na kukuzia kwa sasa yamekwishapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la wafanyabiashara ambao wana tabia ya kuficha mbolea ile ya ruzuku ili waiuze kwa bei za mruko hilo ni jambo ambalo inabidi sisi wote tushirikiane kulitupia macho na tunapoona dalili ya namna hiyo basi tutekeleze wajibu wetu kama raia wema kunong'oneza kwa vyombo vya dola. Lengo la Serikali ni kwamba mbolea ile ya ruzuku ifanye kazi iliyotarajiwa kwa kuwafikia walengwa kwa muda unaohitajika na waipate kwa bei ile ambayo ina ruzuku ndani yake. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Moja, kwa sababu kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi tunasisitiza tunataka kuleta mapinduzi ya kilimo na mimi ninavyoelewa hauwezi kuleta mapinduzi ya kilimo kama huna viwanda vyenyewe vinavyozalisha mbolea hasa ukizingatia kwamba hili ni Taifa la kilimo, sasa je, Serikali inatamka nini kuhusu kujenga kiwanda cha mbolea pale Mbeya ili tuweze kusaidia wakulima wa nchi hii? Pili,...

**NAIBU SPIKA:** Swali moja tu Mheshimiwa.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikumbushe kwamba katika Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000 suala la kujenga kiwanda cha mbolea limetamkwa na maelekezo yametolewa kwa Serikali. Kiwanda hicho kitajengwa wapi inategemea wawekezaji. Pia napenda ifahamike kwamba katika utaratibu wa sasa wa soko huria sio Serikali inayojenga bali ni wawekezaji. Kwa hiyo, wawekezaji wanazo taratibu za kupima, kuangalia wapi panapofaa kwa kulinganisha na upatikanaji wa malighafi na soko wanalolilenga. Kwa hiyo, hatuwezi kusema sasa hivi kwamba lazima kitakuwa Mbeya itategemea mvuto utakaowafanya wawekezaji waamue wapi kiwanda hicho kitajengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kama ana sababu au vigezo vya kuvutia kwamba kiwanda hicho kiwe Mbeya au Mbozi na Mheshimiwa Waziri hapa anasema au Chato ni suala la Mbunge kueleza hivyo vigezo viweze kujulikana na

wawekezaji na kuwavutia na kuwahamasisha ndipo uamuzi unaweza kufanywa, si jambo linaloamuliwa na Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali Na.45 litapangwa tena, tunaenda Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Kazi, Mheshimiwa Janet Kahama!

Na. 46

**Utaratibu wa Kutoa Vifaa vya Ujenzi kwa Wananchi**

**MHE. JANET B. KAHAMA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba utahitajika utaratibu rasmi wa kuwapatia wananchi vifaa vya ujenzi wale ambao wangependelea kujijengea nyumba zao wenyewe bila kulazimika kununua nyumba zilizojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa?

(b) Je, ni lini utafiti wa ujenzi wa nyumba zenye gharama nafuu uliokuwa unafanywa na taasisi za ujenzi kwa miaka mingi utaenezwa kwa wananchi wote nchini?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janet Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Serikali kwa sasa siyo kuwapatia wananchi vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kujijengea nyumba zao bali ni kuwapatia mafunzo ya utumiaji wa teknolojia rahisi ya ujenzi wa nyumba bora kwa kutumia vifaa vya ujenzi vilivyotafitiwa na vinavyopatikana kwenye maeneo yao. Serikali imekuwa ikitekeleza jukumu hili kupitia Wakala wa Taifa wa Utafifi wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi *(National Housing and Building Research Agency - NHBRA).* Wakala huu unatafiti vifaa bora vya ujenzi na vya gharama nafuu, mbinu rahisi za ujenzi na kusambaza matokeo ya tafiti hizo kwa wananchi.

Aidha, Serikali inasisitiza ushirikishwaji wa sekta binafsi, *NGOs* na *CBOs* katika uendelezaji wa makazi endelevu nchini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa nyumba za gharama nafuu uliokwisha kufanyika unaendelea kusambazwa kwa wananchi kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhamasishaji unaofanyika kupitia kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya na viongozi wengine na kupitia vikundi vya ujenzi *(Grassroots Building Brigades)* vilivyoundwa. Kwa mfano, kwa kupitia njia hizo, Wakala umehamasisha ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwenye Halmashauri za Wilaya 40 zilizoko katika Mikoa 18 ya Tanzania Bara.

Pia, umetoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa vikundi vilivyoundwa katika Wilaya 23 zilizoko katika Mikoa 16. Wakala umetumia fursa za mikutano na semina kufanya maonyesho ya teknolojia na vifaa mbalimbali vya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikutano na semina hizo ni kama zilizofanyika kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Makatibu Wakuu na Makatibu Tawala wa Mikoa. Aidha, zimejengwa nyumba 40 za mfano katika maeneo mbalimbali nchini.Pia, wakala umeshiriki katika maonyesho ya Sabasaba na Nanenane kuanzia mwaka 2002 - 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ni kuwafikia wananchi wote, lakini imeshindwa kufanya hivyo kutokana na ufinyu wa Bajeti. Hivyo, itajitahidi kuongeza tengeo la fedha kwa Wakala huu ili utoe huduma zinazokusudiwa.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri yaliyoniridhisha, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kauli mbiu ya Chama Tawala ni maisha bora kwa kila Mtanzania na hasa katika suala la makazi, je, Serikali haioni sasa kuna haja baada ya haya yote waliyofanya kushirikisha Halmashauri pamoja na Shirika la Nyumba ili kuanzisha katika kila Wilaya *branches* kwa ajili ya kuwawezesha kutoa mafunzo ya ugani na kuwasaidia watu waweze kujenga nyumba zenye gharama nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wazo lake ni zuri, tumekwishaanza mikakati ya kuhakikisha kwamba tunawafundisha watu mbalimbali au wananchi katika maeneo ya vijiji na ndio sababu nimesema kwamba tuna vikundi vinavyoitwa *Grassroots Building Brigades* ambapo vinaundwa katika kata na vijiji.

Sasa hivi viko katika vijiji mbalimbali kama vile Iramba, Singida, Karagwe, Biharamulo na vingine kote nchini na *group* hizi au vijana ni vijana ambao mnawachagua wenyewe katika maeneo yenu halafu mnaandika barua Wizarani kuomba kuja kufundishwa tunaleta watalaam kwa wakati huu katika kila eneo ambalo mtahitaji na kuwafundisha ili waweze kujenga nyumba za gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakapofikia mfuko ambao tunasema tutaongeza fedha tunaweza kufanya kama Mheshimiwa Mbunge alivyotoa maoni. *(Makofi)*

Na. 47

**Utoaji wa *Passport***

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO** aliuliza:-

Kwa kuwa pamekuwepo na msongamano mkubwa katika Ofisi ya Uhamiaji Dar es Salaam hasa kwa wale wanaotaka kupata *passport;* na kwa kuwa hati hizo za kusafiri nje zimekuwa zikitolewa Dar es Salaam peke yake kwa kuwa ndiko kwenye ofisi zenye

hadhi; na kwa kuwa ofisi za Uhamiaji Mjini Moshi zina hadhi ya juu sana na zingeweza kutoa hati hizo kwa Kanda ya Kaskazini:-

Je, Serikali haioni ni busara kuitumia Ofisi ya Moshi kama Kanda kuiruhusu kutoa *Passport,* ili kupunguza msongamano Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua usumbufu wanaoupata Watanzania katika kufuatilia *passport* zao Makao Makuu, Dar es Salaam. Kutokana na hali hii, Serikali inakusudia kusambaza huduma za utoaji wa *passport* kwenye Ofisi za baadhi ya Mikoa itakayopewa hadhi ya Kanda, kama Mkoa wa Kilimanjaro pindi ikipatikana mitambo ya nyongeza ya kuchapa *passport* na Ofisi hizi zitakapokuwa zimeunganishwa na Makao Makuu kwa mtandao maalum wa *computer.* Serikali hivi sasa inazungumza na wataalam ili kuanza zoezi hilo katika mwaka ujao wa fedha. Hadi hapo mipango hiyo itakapokamilika, *passport* zitaendelea kutolewa katika Ofisi za Uhamiaji Makao Makuu Dar es Salaam na Ofisi Kuu Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, baada ya ofisi ya Dar es Salaam na Zanzibar kuongezewa mitambo, uwezo wa kuchapisha *passport* sasa umeongezeka na msongamano wa watu wanaosubiri *passport* umepungua kwa kiwango cha kuridhisha.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanaridhisha lakini ninalo swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa ofisi hizi sio zinazochapisha *passport* isipokuwa zinatoa na kujaza, kwa hiyo mambo ya kusema teknolojia mpya inakujaje kwani hatuwezi kuanza tu moja kwa moja wakatoa *passport* kule Moshi na hizo Kanda nyingine? Maana hizi *passport* zinachapishwa nje, kule kwenye ofisi wao wanaandikisha tu zile *passport* na kuunganisha kwa *computer* ni kitu rahisi tu kuna haja gani labda kama pesa hazipo za kungojea mpaka mwezi wa saba atuhakikishie kama wataanzisha Mkoa wa Kilimanjaro ni wa pembezoni ambao unabeba Tanga, Arusha na Manyara utapewa *priority* ili tuanze kutoa *passport* pale?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mitambo inayohusika ni *printers.* Zamani *passport* zetu zilikuwa zinaandikwa kwa mkono, Shirika la Usalama wa Usafiri wa Anga likapiga marufuku. *Printers* hizi ni maalum na zinagharimu mabilioni ya fedha. Ingawa *passport* zinachapwa nje, mitambo hii ya ku-*print* majina yale kwa sayansi na teknolojia hufanyika Dar es Salaam na Ofisi Kuu ya Zanzibar. Kwa hiyo, hatuwezi kuchapa wala hatuwezi kuagiza watu wa Mikoa kuzitengeneza *passport* hizo kule kule lazima zifike Dar es Salaam kwa sababu ya utaalam huo niliousema.

**MHE. FELISTA A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa kuwa sasa kuna wageni wengi wanaoingia nchini pasipokufuata taratibu za uhamiaji, je, Serikali ina utaratibu gani wa kudhibiti hati hizo kuhakikisha kwamba zinatolewa kwa wananchi au raia tu wa Tanzania na ukizingatia kwamba hizo *passport* kwa sasa zinatolewa Dar es Salaam tu?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunajaribu kutatua tatizo hilo alilolisema Mheshimiwa Mbunge ambalo ni tatizo la kweli kwa mambo mawili. Kwanza, hizi hati za kusafiria tumeshazifanya ziwe za kisasa, ni *machine readable* kwa hiyo, kughushi sio rahisi. Tatizo lililobaki sasa ni hizi hati zinazoitwa em*ergence travel document.* Hizi ndizo ambazo sasa hivi wanazighushi nazo tuna mpango wa kuzifanya ziwe *machine readable* hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia ya pili ni kuendelea kupambana na hawa *illegal immigrants* katika kuwakamata na kuwafukuza ndani ya nchi. Kwa mfano mwaka 2000 tuliwakamata 1,768, mwaka 2003 tuliwakamata 3,569, mwaka 2004 tuliwakamata 3,165, mwaka 2005 tuliwakamata 1,640. Kwa hiyo, kazi ya kuwasaka, kuwakamata na kuwafukuza ndani ya nchi tutaendelea nayo.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Hili suala la *passport* limekuwa fumbo, hivi Wizara hii inaweza kutuambia mpaka sasa ni *passport* ngapi zimeshatengenezwa na ni watu wangapi wamepewa wa hapa ndani na wa nje ya nchi?

**NAIBU SPIKA:** Swali jipya na *statistics* ni nyingi ila kama una majibu tafadhali endelea!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 2 Februari, 2006, Serikali ilikuwa imepokea maombi 128,000. Katika maombi hayo, Serikali kwa ujumla wake imeweza kuchapisha *passport* 120,721. *Passport* ambazo zinashughulikiwa na ofisi yetu ni 7,600 na katika hizo 2,000 ni za nje na 5,600 ni za humu ndani. Ni matumaini yetu kwamba itakapofika mwisho wa mwezi huu, mzigo mkubwa huu utakuwa umepungua kwa kiasi kikubwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha.

Nina matangazo machache. Kwanza kabisa, lazima tuwapongeze Mawaziri wameanza kuyaweka majibu yao mafupi kwa kiwango fulani wanaweza wakafanya zaidi ya hapo. *(Makofi)*

Lakini pili na Waheshimiwa Wabunge sasa maswali yenu ya nyongeza yanakuwa hotuba. Kwa hiyo, pia na ninyi mna kasoro hiyo hiyo.

Wale wanaoandika maswali waende kwenye hoja maana yake unaandika swali *page* nzima kwa hiyo, anapokuja Waziri naye anashindwa kujua wewe hasa unataka kunasema nini. Kanuni yetu inatuambia tuwe na maswali ya *direct* na wanaojibu wajibu *direct.* Kwa hiyo, tukifanya hivyo kipindi chetu kinakuwa chepesi kufanya kazi. *(Makofi)*

Mnakumbushwa mavazi ya humu ndani. Sio vizuri Spika akuambie wewe leo toka nje kwa sababu hujavaa mavazi rasmi.

Kwa hiyo, msome Kanuni inayohusika na mavazi kusudi tusiweze kuingiliana, unaweza ukavaa suti ya Kitanzania lakini ukosi umekuwa rangi nyingine pia hairuhusiwi, kwa hiyo, naomba pia hasa kwa Waheshimiwa akina baba muangalie mavazi yetu. *(Makofi)*

Ya pili ni kwamba tupo katika *learning process,* kuna Waheshimiwa wachache wameudhiwa na kauli ya Waziri mmoja lakini waliponiandikia ki-*note* wala hawakuandika majina yao kwa hiyo, ni vizuri mnapomuandikia Spika muandike majina kwa sababu hatujapata hoja kwamba wote wameudhiwa ni hawa walioandika. Kwa hiyo, naomba pia mnapoandika *note* zetu, andikeni na majina yenu na sisi tuweze kuwajibu wanaohusika.

Baada ya kusema hivyo kuna matangazo ya mikutano, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa anaomba Kamati yake wakutane leo tarehe 10 Februari, 2006 saa 6.30 mchana katika ukumbi 432 *Wing C,* ghorofa ya nne katika jengo la Utawala. Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mgana Msindai.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Mohamed Missanga anataka kuwe na kikao saa 6.00 mchana katika ukumbi 428 *Wing C,* ghorofa ya nne wale wengine ni 432 na huyu ni 428 saa 6.00 mchana.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira anataka wajumbe wake wakutane saa 5.00 asubuhi katika chumba namba 219 *Chief Kasusura* ghorofa ya pili, saa 5.00 asubuhi.

Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, anaomba kuwatangazia kuwa kesho tarehe 11 Februari, 2006 tutakuwa na semina kwa Waheshimiwa Wabunge hapa ukumbini kuanzia saa 2.30 asubuhi semina itaanza saa 3.00 nadhani hili tutaliangalia tena kwa sababu nakumbuka kuna kitu kingine.

Katibu Msaidizi wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge ambao hawakupata mifuko yenye makabrasha ya Semina ya Wizara ya Afya iliyofanyika *Ubungo Plaza,* Dar es Salaam kuwa wawasiliane na Katibu wa Kamati Ndugu Muswige Bisile, chumba namba 231 ili waweze kupewa mifuko hiyo.

Kwa wanachama wa Chama cha Mapinduzi uchaguzi wa nafasi ya Katibu wa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi wanaambiwa kwamba fomu husika zitaanza kutolewa ofisini kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Dodoma kuanzia tarehe 10 Februari, 2006 hadi tarehe 16 Februari, 2006 saa 10.00 jioni. Wanachukua fomu kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Makao Makuu, Dodoma.

Kesho wanachama wa Chama cha Mapinduzi wanaambiwa kesho saa 4.00 tutakuwa na kikao cha Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi ndiyo maana nikasema inagongana na kikao fulani hapa. Tutaliangali hilo na jioni tutapata ufumbuzi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo naomba tuendelee. Katibu.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa wa Mwaka 2006 *(The National Leaders' Funeral Bill, 2006);***

**Muswada wa Sheria ya Kusimamia Maeneo Maalum ya Uwezeshaji Raslimali wa Mwaka 2006 *(The Special Economic Zones Bill, 2006);* na**

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mpango wa Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje wa Mwaka 2006 *(The Export Processing Zones (Amendments) Bill, 2006)***

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa kwa mara ya Kwanza)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Hoja ya Kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa Bungeni Tarehe 30 Desemba, 2005

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi hii kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Kwanza kabisa niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote waliorudi katika jumba hili Tukufu ili kuweza kuchangia hoja kwa ajili ya maendeleo ya Majimbo yetu.

Nimpongeze vile vile Mheshimiwa Spika, kwa ushindi wake na pia nikupongeze wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupata ushidi wa kishindo kuwa Naibu Spika wa Bunge letu hili.

Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kupata kura nyingi za Wabunge kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amezungumzia mambo mengi mazito ambayo ni ya msingi na yanahitajika au yanahitaji yafanyiwe kazi na Serikali ili yaweze kutekelezwa kwa uhakika na hatimaye wananchi wetu waweze kupata matumaini na Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Niipongeze hotuba ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, amezungumza mengi lakini mengi yameshazungumzwa hapa Bungeni na mimi nichangie machache ambayo kwamba naona ni ya msingi ili Serikali iweze kuyazingatia na hatimaye kuyafanyia kazi kwa utaratibu ambao unatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango mzima wa MKUKUTA mwaka 2025 lakini katika utekelezaji wake tunategemea mambo makubwa ambayo yapo katika nchi yetu wala siyo malighafi au ni mambo ambayo yanatakiwa yatoke nje ili kuja kukamilisha mipango yetu ya MKUKUTA. Maeneo haya ni kama yafuatayo kwanza ni ardhi kwa ajili ya kilimo, ardhi hii hii kwa ajili ya misitu, ardhi hii hii kwa ajili ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia kwamba misitu yetu inakatwa kwa kiwango kikubwa sana na Serikali hivi karibuni kwa kauli yake imesema inapiga marufuku usafirishaji wa magogo, mimi nasema hii haitoshi ukisema usafirishaji wa magogo umepigwa marufuku ina maana unaendelea kuruhusu magogo yakatwe lakini yawe na matumizi mengine lakini siyo kwa usafirishaji.

Katika semina tuliyokuwa nayo wiki mbili zilizopita mimi nilipendekeza mbele ya Serikali nikaiambia sasa Serikali hatuna budi kufunga misitu yetu kwa kipindi cha miaka 40 mpaka 50. Kwa misingi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema tukifunga misitu yetu na tukaacha misitu ambayo imepandwa kwa makusudi hii misitu iliyopandwa ndiyo itumike kwa mahitaji muhimu ya wananchi wetu wetu, tuna misitu ya *pine* ambayo inatumika kwa ajili ya mbao za ujenzi na hata sasa hivi teknolojia imekwenda mbele *pine* hii hii inatumika kwa kutengeneza *furniture* nzuri, wananchi walio maskini pia wanamudu kununua *furniture* hii. Yule mwananchi ambaye anataka apate *furniture* ya *high quality,* mbao nzuri vile vile tuna misitu ya *tic* ambayo ni mbao safi na ya ghali sisi hatuipi thamani mbao hii, lakini huko nje *furniture* yoyote ya *tic* huwezi ukainunua kwa sababu ni aghali sana. Basi tutumie mbao ya *tic* kwa ajili ya mambo mengine ambayo mwananchi yoyote anahitaji labda *quality* nzuri zaidi ya mbao kwa ajili ya mambo mengine ya kwake mwenyewe nyumbani kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini imefika mahali sasa tufunge kabisa misitu yetu kwa muda mrefu kama nilivyopendekeza miaka 40 mpaka 50 ili tuweze kupata mambo yafuatayo:-

Kwanza, turejeshe uhai wa ile *equal system* ambayo sasa hivi imekwishapotea katika misitu yetu. Kuna viumbe vingine havipo tena kabisa katika misitu yetu au katika Tanzania hii ni kwa sababu ya kukata misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, turudishe utiririkaji wa maji katika milima yetu ambayo inatusaidia katika kilimo, tufunge misitu yetu tupate maji na mvua ili tuweze kuendesha mitambo yetu ya umeme. Sasa bila ya kuwa na hivi vitu viwili kuhifadhi misitu tupate maji ili tuwe na kilimo cha umwagiliaji kama mkakati mzima wa MKUKUTA juu ya kumwendeleza mwananchi katika kumwondoa katika umaskini, bila ya maji hatuwezi tukawa na mpango wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kilimo cha umwagiliaji kwa mazao ya chakula na mazao ya kibiashara tuna mipango kwamba mazao ya kibiashara yawe yanasindikwa mengine kama korosho, pamba, kahawa lakini vikienda kiwandani tuna matatizo ya umeme tutakuwa hakuna sababu ya kuzungumzia kuwa na mazao ambayo kwamba yawe *processed* kwenda kiwandani wakati hatuna umeme. Kwa hiyo, narudia tena kwamba umuhimu wa misitu kupata maji kuendesha mitambo ya umeme na hatimaye tuwe na umeme wa uhakika kuweza kutimiza malengo yetu, bila kufanya hivi mimi naona tutakuwa tunapiga kelele bure lakini jambo la msingi na Serikali na Serikali inaelewa kwamba misitu ni msingi muhimu katika uhai wa Mtanzania hivi sasa.

Mimi naiuliza tena Serikali hivi tuambieni *advantage* na *disadvantage* ya kukata misitu yetu. Tumekata misitu mimi nasema tumepata *disadvantage* ambayo tunaiona hivi sasa hivi, ukame huu uliokithiri ni kwa sababu imechangiwa vile vile na kukata misitu yetu hapa nchini.*Population* ya nyuki inapungua kwa utaratibu ambao kwamba unatumia wa kuvuna asali. Sasa hata *population* ya nyuki tunaipunguza na tunategemea vile vile asali iwe ni moja ya zao ambalo litawanufaisha wananchi wetu kule vijijini, tuweke utaratibu mzuri wa kuweza kuhakikisha misitu iliyokuwepo inakuwa endelevu na hatimaye wananchi waitumie vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii ina mchango mkubwa katika suala hili na hii Wizara ya Maliasili na Utalii ni kubwa. Nilisema mimi Wizara hii ya Maliasili na Utalii inatosheleza kabisa kukidhi Bajeti ya nchi hii ikiwa mikakati mizuri itawekwa kuiendeleza Wizara hii katika utaratibu mzuri kabisa ili kuweza kupata bajeti kubwa ya Serikali kutokana na hii Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utakuta misitu yetu kwa taratibu za sheria kuna mkurugenzi mmoja pale Wizarani ambaye anasimamia misitu ya nchi nzima na kule katika maeneo yetu kuna mtu mmoja tu yuko katika Halmashauri au pale Mkoani ambaye hana madaraka kisheria ya kuweza kutoa maamuzi pale ambapo patatokea uharibifu mkubwa wa misitu ni lazima amuarifu Mkurugenzi Wizarani na hatimaye Mkurugenzi achukue hatua. *(Makofi)*

Mimi nasema hivi sasa imefika wakati tuzitazame sheria zetu, tuhakikishe kwamba Mkurugenzi wa Misitu anakuwa na wasaidizi wake katika Kanda wenye mamlaka kubwa kama yeye na wenye maamuzi ya kutosha kuweza kuona kwamba uharibifu wa misitu hautokei kama unavyotokea hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nishati tunayoitumia tunaweza tukatumia umeme kwamba ndiyo nishati nyepesi na rahisi kwa ajili ya maendeleo yetu. Lakini wananchi wetu vijijini hawana umeme na hivi sasa Serikali inatazama nishati mbadala kwa ajili ya matumizi ya nishati badala ya kuendelea kutumia mkaa na kuni kwa wingi. Hivi sasa mimi naiomba Serikali itazame upya ni jinsi gani tutatumia gesi ambayo inavunwa kule Songosongo na *Mnazi Bay* na hatimaye iweze kusambazwa hata vijijini na wananchi wetu waanze kuzoea kutumia nishati ya gesi kwa ajili ya matumizi yao ya majumbani na hatimaye kuweza kuhifadhi misitu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati nyingine ambayo ni makaa ya mawe tunafahamu kwamba tuna *deposit* kubwa ya makaa ya mawe kule Mchuchuma, lakini tunatafuta wawekezaji kwa ajili ya kutumia nishati hii ya makaa ya mawe kwa ajili yakuzalisha umeme. Mimi kwa jiografia ilivyo kule katika maeneo ya mchuchuma siyo rahisi mwekezaji kuweza kuvuna makaa ya mawe na hatimaye kuweza kuyatumia makaa yale kwa ajili ya uzalishaji wa umeme peke yake.

Mimi naona katika utaratibu wa uwekezaji inakuwa hailipi ni vema tupate mwekezaji ambaye kwamba ataweza kuvuna au kutoa makaa ya mawe yale kwa ajili ya umeme na wakati huo hui kwa ajili ya *export.* Hivi sasa hivi makaa ya mawe hata nchi nyingine zinazoendelea zinahitaji makaa ya mawe kwa ajili ya maendeleo yao, China ni moja ya nchi ambayo inatumia nishati ya makaa ya mawe katika maendeleo yake, sisi tuna *deposit* kubwa ambayo kwamba inakadiria kuwa na *1.2 billion tons* ni *deposit* kubwa.

Kwa hiyo, mwekezaji atazame uwezekano wa kutumia makaa yale ya mawe katika uzalishaji wa umeme na hatimaye kuweza kusafirisha kwa kutumia reli ya *TAZARA* na hatimaye kuweza kuunganisha kutoka kwenye mgodi wa makaa na hatimaye kuunganisha na reli ya *TAZARA* mpaka Bandari ya Dar es Salaam ili tuweze kufaidika katika maeneo yote miwili kwa kuuza makaa nje na kutumia makaa haya kwa ajili ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu huu tunaweza tukapata mwekezaji akawa anafanya yote miwili kwa kuuza makaa na makaa hayohayo vilevile yatumike kwa ajili ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka nataka nizungumzie suala la uvuvi....

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ikiwa ni mara yangu ya kwanza kuweza kuchangia katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe pongezi za dhati kabisa kwa kuchaguliwa Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Waziri wetu Mkuu, Viongozi, Wabunge wote ambao walioingia katika Bunge hili Tukufu.

Lakini pia sitawasahau wananchi wa Jimbo la Chwaka kwa kunichagua katika Bunge hili Tukufu kwa kipindi cha tatu na ninaahidi kwamba nitawatumikia na nitawatekelezea yale ambayo yanastahili na kunipa moyo kwamba wanahitaji kwa mafanikio na kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hotuba hii imemaliza mambo lakini tuna wajibu wa kukarabati na kukumbushana ili tuweze kupata ufanisi mzuri zaidi. Katika hotuba hii ukurasa wa 18 hotuba inasema: "Nachukua uongozi wa Taifa letu nikiwa nasononeshwa sana na mpasuko wa kisiasa kati ya Unguja na Pemba na kati ya Pemba na sehemu nyingine." mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais anaonyesha imani kubwa na upendo kwa Wantanzania na mapenzi makubwa sana asingetamka haya, lakini haya ametamka kwa uchungu kutokana na matendo yanayojitokeza na hii anakumbusha kwamba kama yapo basi yasitokee tena, lakini hata hivyo tuna wajibu wa kueleza hali zilivyo na kwa nini inajitokeza hii hususan nikiwa natoka Zanzibar nina wajibu wa kueleza hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, historia inajirudia. Siasa ya Zanzibar siyo siasa ya Tanzania Bara nataka tuelewe vizuri kabisa. Kwanza Tanzania Bara tunajua tuliweza kushinda kwa kalamu tu na wale tuliowashinda nina imani kwamba hawapo sasa, lakini ninavyojua Tanzania Visiwani tumefanya chaguzi nne, mwaka 1957 na *ASP* ilishinda ikapata viti 5, *Muslim Association* ilipata kiti kimoja na *ZNP* haikupata kiti hata kimoja, hiyo ni historia. Tukaja Januari 1961 tukafanya uchaguzi *Zanzibar Nationalist Party* walipata viti 9, *ASP* ikapata viti 10 na *ZPPP* ikapata viti vitatu. Tukaja Juni tukafanya uchaguzi tena baada ya kuona kwamba *ASP* inashinda wakaona lazima waweke Jimbo Mtambile ili kwa kufanikisha uchaguzi ili kushinda na waliweka kwa hiyo, mpira ukaja *draw ZNP* viti 10, *ASP* viti 10, *ZPPP* viti vitatu, lakini hawa wote ni jamii moja hususan sehemu ya Kisiwa cha Pemba.

Sasa tuione hiyo hali ilivyo na uchaguzi wa mwisho tukafanya mwaka 1963 na waliungana baina ya *ZNP* na *ZPPP,* waliungana sasa hii ndiyo hali iliyojitokeza lakini tarehe 12 Januari, 1964 tukaona hakuna njia isipokuwa lazima kufanya Mapinduzi na ilikuwa ni Mapunduzi ya kihalali kabisa ili kuondoa Usultani, leo nashangaa mtu aseme Wazanzibar kwamba hawayatambui Mapinduzi, kichekesho kikubwa sana lakini siwezi kustaajabu kwa sababu tuliowaondoa sisi ni waarabu na ndiyo waliotutawala na nina imani kabisa kwamba bado vishina vipo sasa hii inaonyesha ni tofauti na huku Tanzania Bara kwamba hatuwaoni yuko wapi Mwingereza hapa kwamba mmefanya uchaguzi hapa ataingia? Nataka tuelewe vizuri kabisa historia inavyotoka na hawa wanakuhadaeni sana hawa kwa sababu hamuijui historia, lakini pia nikupeni pongezi Watanzania Bara kwamba hakupata *CUF* Jimbo, wote wako nje.

Sasa hali hii inatuletea usumbufu mkubwa sana na ndiyo Mapinduzi yale Rais Karume akaona ajenge umoja ikafika hadi kuoana ili tuwe kitu kimoja, tujenge damu moja, lakini wale wale ndiyo waliomuua Karume. Tunakwenda wapi? Halafu wanakuja hapa wanakwambieni maneno sisi tunataka kusaidia. Hawana msaada, wangesaidia kwao Pemba nakwambieni mimi, maendeleo gani waliyoyafanya? Isipokuwa maendeleo wanayabomoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ina imani sana, inatoa mambo yote sawa haina ubaguzi Unguja na Pemba, leo wanakuja kusema hakuna maendeleo, wanadai uongozi wapate uongozi gani? Makamu wa Rais anatoka wapi? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Pemba!!

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mnataka nini? Mnataka kitu gani wenzetu? Najua wengine mmekuja hii historia hamuijui na unajua kwamba mimi Pemba kama sikuwa *CUF* siwezi kupata uongozi na ndiyo uliokuletea na pengine mna imani sana na Chama cha Mapunduzi, najua mbele yenu mpo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiongozi mmoja alisema maneno hapa si mazuri na kwa kweli sisi kwetu si jambo la busara kuweza kufanya vile kwamba labda Pemba wananyanyaswa, wanafanyiwa vitendo viovu, hiyo si kweli, mimi najua wao ndiyo wenye vitendo viovu, mimi binafsi mtoto wangu ameuawa Pemba amechinjwa kama kuku, nakwambieni leo sijasema mimi hapa kipindi cha tatu niko Bunge hili sijasema mtoto wangu Haji mmemuua kama kuku sijasema Bunge hili mimi. Katibu wa Chama cha Mapinduzi Jimbo la Ziwani mmemuua kama kuku mkawakata vipande vipande, uungwana kweli?

Mnakuja mnazunguza nini binadamu ati unasema wewe muislam, mtu anakwenda msikitini unampiga panga unamkata, kweli akili hii? anakwenda kuswali halafu unasema wewe muislam. Tunakwenda wapi? Kama tuna imani tuwe kitu kimoja mtafute maendeleo ya nchi, yale yalishapita na ninakwambieni Zanzibar, Zanzibar tuna mtihani kwa sababu wenzatu hawa mimi binafsi Ali Macho kaenda Dubai na akaulizwa Serikali tutapata Zanzibar haki ya Mungu na Mtume mimi muislam na leo ijumaa, kaulizwa hivyo itakuwaje mtu wa Dubai aulize Serikali ya Zanzibar inamhusu nini? *Halah! (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo. Tumefika sasa wakati ....

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja iliyokuwa mbele yetu.

Kwanza naanza kwa kutoa pongezi kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Makamu wa Rais pamoja Rais wetu wa Zanzibar kwa kuchaguliwa kwa ushindi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kutoa shukrani kwa akima mama wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kuniwezesha kurudi tena Bungeni katika kipindi hiki cha pili. Nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua nafsi hii kutoa rambirambi kwa wazee, ndugu na jamaa wa watoto kumi na moja waliofariki Zanzibar juzi kwa ajali ya baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya dibaji hiyo naomba nami nichangie hoja yetu hii ya leo kwa mchango wa jumla jumla. Nitaanza na sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi waliosimama hapa kuchangia walizungumzia sekta ya kilimo na hii haikuja hivi hivi tu, lakini ni kwa kuwa sisi tunaguswa sana na sekta hii kwa sababu ni imani yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge walio wengi mizizi yetu ni huko kijijini na tuna jamaa, ndugu na wazee wetu ambao hivi sasa ndiyo wanaendelea na kazi ya kilimo kule vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 29 alisema kuwa kilimo ni mhimuli wa uchumi na wengi wetu humu tumekuwa tukisema kilimo ni uti wa mgongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo hivi sasa bado haijaonyesha kuwa kilimo kweli ni uti wa mgongo kutokana na hali mbaya ilivyo katika sekta hii. Suala la *modernization* katika kilimo ni suala ambalo halitaki mjadala wala mbadala. Ni suala ambalo ni lazima lipewe kipaumbele ili kubadilisha sura nzima ya kilimo chetu. Kilimo cha jembe la mkono kimeshapitwa na wakati na wala hakiwezi tena kuhimili kilimo katika Tanzania yetu hii ambacho kinategemewa na wengi.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa tutafute matrekta kwa nguvu zetu zote tupeleke vijijini, tufanye kilimo cha umwagiliaji maji kwa sababu Tanzania kama inavyoelezwa na kama tunavyojua ina vyanzo vingi sana vya maji na hata pale ambapo hakuna vyanzo vya mito na maziwa lakini ukichimba tu chini hufiki mbali sana, maji yanapatikana kama ilivyo hapa Dodoma. Kwa hiyo, ni kitendo kidogo cha aibu cha kuonyesha nchi kama hii ina maji mengi sana lakini tunashindwa kabisa kuzalisha chakula ambacho kinaweza kututosheleza sisi wenyewe Watanzania humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utafiti ni suala muhimu sana katika maendeleo ya nchi yoyote ile. Nchi zote zilizoendelea zimetoa kipaumbele katika kufanya utafiti wa kimaendeleo katika sekta zake zote. Kwa hiyo, tukija katika sekta ya kilimo utafiti ni kitu muhimu sana, utafiti wa mbegu bora, utafiti wa viuatilifu na visumbufu na utafiti wa

mambo mengine ambayo yanaleta maendeleo katika sekta ya kilimo. Hivyo zile Taasisi ambazo zinashughulika na mambo ya utafiti zipatiwe mahitaji yao yote ili yaweze kuendeleza utafiti huu, wapatiwe motisha ya kutosha ili na watafiti nao wapate ule moyo na mori wa kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni hili la huduma ya ugani, huduma ya mabwana shamba. Mabwana shamba wanajitahidi kufanya kazi zao lakini wanapewa maeneo makubwa na hawana hata usafiri wa kufuatilia katika kufanya shughuli zao huko Vijijini, kwa hiyo wanashindwa kufanya kazi zao ipasavyo. Kwa hiyo, tuwapatie vitendea kazi hawa watu ili waweze kuwafikia watu walio wengi na kutoa elimu inayostahili, kwa sababu hivi sasa elimu haiwafikii walio wengi, hata huo utafiti ukifanywa matokeo ya utafiti hayawafikii wananchi kwa sababu Mabwanashamba hawawezi kuwafikia. Kwa hiyo, suala la kuwapatia vipando vile vile tulipe kipaumbele ili waweze kufikisha haya matokeo ya utafiti na hatimaye wakulima wetu waweze kuzalisha vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bora kwa wakulima ni kitu muhimu sana. Tutafute njia nyingine yoyote ambayo inaweza kutumika ili elimu ifike kwa wakulima wetu. Pengine kupitia redio na *Television* haitoshi lakini tutumie labda *machinery* za Serikali zilizoko mpaka vijijini huko, kuna Serikali za Mitaa, Serikali za Vijiji tutafute watu tuwape elimu waweze kuwasomesha kwa lugha zile ambazo zinakubalika katika vile vijiji. Kuna mambo kama *crop rotation,* sasa hivi umekufa mtu analima zao moja hilo kila wakati hata kama katika hiyo ardhi haiwezi kutoa tena mavuno ya kutosha. Kuna haja ya kutoa elimu ya mabadiliko ya miongo, miongo inabadilika lakini watu wetu wapo pale pale mwezi huu ni wa kupanda, kwa hiyo waelimishwe ili waende sambamba na miongo inavyokwenda.

Vile vile kuwe na kutoa elimu ya kubadilishwa *mind sets* ya watu wetu katika shughuli za kilimo. Imezoeleka tu mimi hapa ninapanda mahindi, kwa hiyo, maisha yote nitakuwa napanda mahindi bila kuangalia kwamba sasa hivi mambo yamebadilika. Ukame tunaouona hivi sasa mtu bado ameshikilia tu mimi nitapanda mahindi hata kama kuna ukame, kwa hiyo, tutoe elimu ya kutosha kubadilisha *mind set* za watu wetu kujua chakula chochote ni chakula ili mradi kinalinda uhai wako na uhai wa familia yako. Kwa hiyo, tuwaelimishe watu wetu. Sasa hivi acheni kulima hiki lakini sasa kilimo kiwe mfano muhogo na muhogo wenyewe sio ulimwe kama kule kwa wale ndugu zetu wa Kusini wanachomeka tu kile kijiti, lakini wakipiga matuta, hata uharibifu wa eneo la juu la udongo unakuwa unapungua, kwa hiyo mazao yanakuwa makubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni vijana na kilimo. Vijana tunasema hawataki kulima lakini sio hivyo wanakimbia hali halisi ilivyo ya kilimo, hakuna miundombinu ya kuwafanya vijana wavutike na kilimo. Vijana wenyewe wamesema kama wakipatiwa matrekta, ikawekwa miundombinu ya kilimo ya kutosha wao wapo tayari kulima kuliko kutembea na soksi mkononi kutwa nzima wala hawajui nini wanachokipata. Tutumie mitandao tuliyo nayo, kwenye CCM tuna Umoja wa Vijana, tuutumie Umoja wa Vijana kuhamasisha vikundi vya vijana vijiunge pamoja wapatiwe

hizo nyenzo na vitendea kazi vingine, vijana wapo tayari kulima na wanasema wenyewe wanajua mazao gani wakilima yatawapatia mapato haraka haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije upande wa uchumi wa Zanzibar. Katika hotuba imeainishwa kabisa na Mheshimiwa Rais kuwa sasa hivi ataangalia namna gani Serikali ya Muungano inaweza kusaidia uchumi wa wa Zanzibar. Tunaelewa Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Tanzania imeundwa na nchi mbili, kwa hiyo ni kitu kibaya sana kuona sehemu moja inakua vizuri sana na nyingine bado iko chini. Kwa hiyo, Rais wetu ameliona hilo na amesema yupo tayari kusaidia katika kipindi hiki na kwa vile kauli imetoka kwa mkubwa sisi tumepata faraja sana tunaona mambo yatakwenda vizuri katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la afya. Tuliambiwa kwenye semina kwa takwimu tuna madaktari 1,500 tu kwa Tanzania yetu nzima yenye watu karibu milioni thelathini na tano. Ukiangalia hiyo unakuta daktari mmoja anahudumia watu karibu thelathini na tatu elfu. Serikali iweke mikakati ya kutosha ya kuongeza hawa madaktari kwa maana ukiangalia takwimu hizo zinaonyesha kuwa kuna baadhi ya watu hawapati matibabu mazuri kutokana na hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mengi lakini kutokana na muda, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi natoa shukrani zangu kwa kuweza kunipatia nafasi hii asubuhi hii kuchangia hotuba hii ya Rais.

Kwanza na mimi niungane na wenzangu kukupongeza sana kwa ushindi mkubwa ambao umeupata na unamudu kuwa Naibu Spika wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawapongeza vile vile viongozi wote, itifaki imezingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie mambo matatu. La kwanza, hii hotuba imeandaliwa vizuri na Rais wetu na kwa kweli isingefaa tuijadili, ilitakiwa iende moja kwa moja kwa utekelezaji ila kwa vile tunataka kuchangia kuweka msisitizo tunaomba Serikali ambayo ameiunda kuifanyia kazi hotuba hii, ina mwelekeo mkubwa na mpana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nichangie katika suala la elimu. Amechanganua sana kwamba tunahitaji Utaifa, sisi tumesoma kupitia utaratibu huo, nimetoka Umasaini, nikaenda Uchagani, nikaenda kila mahali na kisomo ndio kimenifanya nielewe Tanzania na sasa tungependa kwamba wanafunzi wetu waweze kutapakaa katika nchi ili umoja wetu uendelee katika nchi yetu. Hili ni wazo zuri sana.

Kwa hiyo, naomba kuna ahadi ambayo ilitolewa na Rais kipindi cha tatu katika elimu, alituahidi katika Wilaya za Ngorongoro, Monduli, Simanjiro na Kiteto kwamba tutajengewa sekondari moja ya Kitaifa katika maeneo hayo, sisi hatuna. Kipindi kimepita na huyu naye ameahidi katika Ilani ya Uchaguzi, tunaomba sana Wizara ya Elimu na

Mafunzo ya Ufundi, katika maeneo yetu hayo bado tunahitaji ahadi hiyo itekelezwe. Kila Wilaya ipate sekondari ya Serikali ili na sisi tuwe sawa sawa na Watanzania wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa Kiteto, Kiteto hali yake ya elimu ni mbaya sana, iko chini, Kiteto kielimu ni ya pili kutoka mwisho Tanzania. Naomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ikaangalie na kufanya utafiti kitu gani kinasababisha Kiteto iwe namna hiyo. Nasema hivyo kwa makusudi kabisa kwa sababu mazingira ya Kiteto ni sawa sawa na mazingira ya Simanjiro, Monduli, Loliondo na Ngorongoro. Kuna tatizo gani Kiteto mpaka elimu yake inakuwa chini kiasi hicho? Nimepiga kelele katika Bunge hili lakini Serikali imekaa kimya, basi naomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ikaangalie au ikachunguze Kiteto kuna matatizo gani. Naomba washirikiane na TAMISEMI ili Kiteto kielimu iweze kulingana. Kuna sekondari mbili tu na hazijai watoto na kuna shule za *primary* karibu 90 na walimu ni wengi. Naomba likachunguzwe hilo ili mtusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nizungumzie juu ya suala la upungufu wa chakula. Tuna tatizo, Kiteto kuna njaa lakini inawezekana Kiteto kwenye takwimu haipo. Kwa kweli Kiteto ni sehemu ambayo inazalisha chakula hata ukiangalia soko la Tandale tunashiriki kupeleka chakula, lakini sasa hivi ina njaa na naomba nikiwa mwakilishi wao kama takwimu hazijaja katika Ofisi ya Waziri Mkuu wana Kiteto wana tatizo la njaa hususan Tarafa ya wafugaji ya Makami yote na Tarafa ya Kijungwi yote hawana chakula. Hata sehemu nyingine za Kiteto wamemaliza chakula. Mimi nitakuwa shahidi kabisa wa mwisho na wana Kiteto wananisikia na wana njaa ya kweli kweli, nawaombeni wapelekeeni chakula Kiteto katika Tarafa hizo zote cha kununua na kuwasaidia ambao hawajiwezi.

Nimeangalia katika majedwali hapa hakuna Kiteto. Mimi nitakuwa shahidi kama mtu atakufa Kiteto tumeshatoa taarifa tayari, mimi mwakilishi wao nimeshatoa taarifa kwamba wana njaa, sasa sio kazi yetu bali ni jukumu lenu sasa ambao mnahusika kusambaza chakula, kama hampeleki chakula Kiteto basi ninyi ndio mmeua, sio mimi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba nizungumzie suala la mazingira. Tunaomba sana, Kiteto tuna msitu unaitwa Soledo, msitu tu mzuri ambao umevamiwa sasa hivi sasa na uliwahi kupata zawadi kubwa uko *Tariworo Eastern Central.* Sasa hivi umevamiwa na umeuzwa na Serikali haisimamii.

Naomba Wizara ya Maliasili na Utalii ikalete ile heshima ya zawadi tuliyoipata katika msitu huo na ufanyiwe uchunguzi na uvamizi huo. Watu wanakuja Kiteto wanatajirikia Kiteto na kupata mafuso kwa kuuza misitu yetu. Mimi sitaki kutaja majina lakini njooni mchunguze watu wanapata zawadi, wanauza misitu na kula rushwa kwa kuuza misitu yetu, tunafikiri wanakuja kutuhudumia kumbe wanakuja kutajirika. Hebu njooni watu wa maliasili, muone wenyewe na tutasaidiana katika suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la kilimo lakini wenzangu wamezungumzia, naomba tujitahidi. Sasa naomba nimalizie na wafugaji. Maeneo ya

wafugaji sisi tumetenga, namwomba Waziri wa Maendedleo ya Mifugo, wafugaji wapate maeneo mahsusi, hatutaki sasa wafugaji kutangatanga, tunataka maeneo yetu. Sio kwamba tunahamahama ovyo, hatuna maeneo. Mkulima anaingilia maeneo ya wafugaji, Serikali inanyamaza, inawaogopa wakulima, lakini mfugaji akiingia eneo la wakulima, Tanzania nzima inatikisika. Nawaombeni kama tunataka kufuga kila watu wapate maeneo yao na walindwe. Watu wa Serikali hawawezi kusimamia maeneo ya wafugaji, sasa wasimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati wa uzinduzi wa Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuwapongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuweza kuiongoza nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote na Manaibu Waziri kwa kuteuliwa kwao. Nampongeza Mheshimiwa Spika na wewe pia Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania na kuweka historia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano kuwa na Naibu Spika mwanamke toka enzi ya Uhuru, nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru na kuwapongeza wanawake wa Mkoa wa Iringa walionipa kura zao ambazo zimeniwezesha kuweza kurudi hapa kwa mara ya pili na kuwawakilisha. Napenda niwaahidi kwamba nitawawakilisha kwa uwezo wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nianze moja kwa moja kwa kuchangia hoja hii nikianza na suala la uboreshaji wa afya za akinamama. Hotuba ya Mheshimiwa Rais imeelezea wazi kwamba ipo haja sasa ya kuboresha huduma za afya katika maeneo yote na katika hili naomba nizungumzie kwamba vifo vya akinamama wajawazito bado vipo juu. Serikali ifanye juhudi kuhakikisha kwamba vifo vya akinamama wajawazito vinapungua, vifo hivi vimekuwa juu kwa sababu mbalimbali ikiwemo mzigo mkubwa wa kazi walionao wanawake kutokana na huduma duni ambazo wanachukua muda mrefu kutafuta mahitaji muhimu kama maji, utafutaji wa kuni, ikitokea na uharibifu wa mazingira na kuwafanya akinamama wapate shida ya kutafuta huduma muhimu na hivyo kuweza kuathiri afya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napata wasiwasi sana kwa vile sasa hivi tunazungumzia suala la njaa na tunaelewa kwamba huduma za afya kwa akinamama wajawazito ni duni, nakuwa na wasiwasi kwamba vifo vya akinamama wajawazito vinaweza kuongezeka kama hatua mahsusi hazitachukuliwa za kuhakikisha kwamba mgawo wa chakula utakaotolewa akinamama wajawazito waangaliwe kwanza na akinamama wanaonyonyesha pamoja na makundi mengine maalum. Tusije tukasema tu ni wale wenye shida, tukawasahau akinamama wajawazito kuwaweka katika makundi

maalum ambayo yanahitaji uzito unaostahili wa kuhakikisha kwamba wanapata chakula katika wakati huu mgumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la elimu. Serikali imeboresha elimu ya msingi kwa kupitia mpango wa *MMEM* na kufanya watoto wengi waweze kupata elimu na kuinua kiwango cha elimu kwa kufanya watoto wengi waweze kufaulu. Changamoto iliyopo na inayozungumzwa ni ya kuhakikisha watoto hao wote wanaofaulu wanaweza kupata elimu ya sekondari. Sasa tuna wengi ambao wamefaulu na hawakuweza kupata nafasi za kuendelea na sekondari lakini pia tuna wale ambao hawakuweza kupata nafasi za kuchaguliwa kujiunga na sekondari nafikiri sasa tunahitaji kutilia umuhimu pia vyuo vya ufundi na nashukuru Mheshimiwa Rais, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ameiongezea jukumu la kuangalia masuala ya Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya ufundi sasa ni muhimu sana kuangaliwa kwa sababu tunao watoto wanaomaliza darasa la saba lakini tunao wengi pia wanaomaliza sekondari. Tumeongeza watoto waingie sekondari wengi lakini tunatakiwa pia tuangalie elimu ya ufundi ili wengi wanapomaliza shule waweze kujitegemea. Hii ni pamoja na kuongeza kidato cha tano na cha sita. Kwa hiyo, utaratibu wa kuwa na mitaala katika shule hizi kuwe pia kuna mtaala wa ufundi ili kuhakikisha kwamba watoto wanatoka pale wakijitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la huduma za ugani. Huduma za ugani hususan katika huduma za kilimo. Tuna wataalam wa kilimo walioko kwenye maeneo mengi vijijini lakini wataalam hao hawawezi kumfikia kila mkulima kwa sababu wakulima wengi wanalima kile kilimo cha asili, kila mmoja ana shamba dogo la kutumia zana duni na matokeo yake hata kilimo chenyewe kinakuwa duni.

Mimi nilikuwa nafikiri kwamba sasa tunahitaji kuboresha elimu ya kilimo kwa wakulima. Tuimarishe vyuo tulivyonavyo ili viweze pia kutoa kozi fupi kwa wakulima, kwa mfano kuna vituo vya utafiti sehemu mbalimbali kama vile Kituo cha Utafiti cha Kilimo Ismani na vituo vingine vidogo ambavyo vinaweza kutumika kama vituo vya mafunzo kwa wakulima kutegemeana na zao lile wanalolilima na pia kutegemeana na mahitaji yao. Kwa hiyo, tuzingatie kwamba wakulima waweze kupata elimu inayotakiwa na hii itawawezesha vijana wetu kuweza kujiajiri baada ya kuwa wamepata elimu ya kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningeshauri sasa hivi tunaongeza vyuo, vyuo vingi vinaongezeka na kupandishwa madaraja lakini sijasikia tukiongeza vyuo vya kilimo au kupandishwa madaraja. Kuna vyuo kama Ukiriguru, Nyegezi, Uyole, Ilonga, Morogoro, vyuo hivi ni vya muda mrefu, nafikiri sasa tufikirie kuvipandisha daraja ili viweze kutoa wataalam wa ngazi mbalimbali ikiwemo pia Stashahada za juu za kilimo. Vyuo hivi vinatoa *Diploma* tu za kawaida za kilimo na tunahitaji wataalam wa kilimo wengi wenye ujuzi unaoendana na utaalam wa kisasa na soko huria lililopo. Kwa hiyo, tunahitaji kupandisha vyuo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la UKIMWI. UKIMWI ni tatizo kubwa sana na naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wale ambao Mikoa yao haijaathirika sana wasije wakakaa wakafikiri kwamba wapo salama. Elimu ya UKIMWI inatakiwa itolewe katika maeneo yote, kule ambako kumeathirika sana tutumie njia mbalimbali za kuweza kuboresha hali ya wale walioathirika lakini kwenye Mikoa ambayo haijaathirika sana elimu inatakiwa ili tupunguze maambukizo tusije kujikuta kote kunakuwa na maambukizo yanayolingana.

Kwa hiyo, ni jukumu la kila mmoja wetu sisi Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, wananchi wa kawaida na kila mmoja wetu kuchukua jukumu la kupambana na UKIMWI kama jukumu la kila mmoja ili kuiokoa nchi yetu na kupunguza idadi ya mayatima. Hili litakuwa ni jambo la msingi zaidi hasa tunapokuwa sisi wenyewe tukiwa mstari wa mbele na kuhudhuria vikao ambavyo vipo kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napendekeza kwamba kwa sababu kuna Kamati za UKIMWI ngazi za Wilaya na ngazi za Kata na Vijiji, ni vizuri sasa hata hili Bunge lako Tukufu lifikirie kuwa na Kamati ya UKIMWI ambayo itazungumzia masuala yote yanayohusu UKIMWI nchini kulingana na utaratibu ambao umewekwa na Wizara na Kamati za UKIMWI zilizopo kwenye ngazi zote zishiriki kikamilifu katika mapambano haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la malezi ya watoto yatima. Suala la malezi ya watoto yatima limekuwa ni tatizo kubwa kwenye maeneo yaliyoathirika kama Mkoa wa Iringa na hasa katika Wilaya ya Makete na hao watoto yatima pia tunao wengi katika Wilaya ya Njombe na Wilaya zote za Mkoa wa Iringa. Nafikiri kwamba tunahitaji kufikiria jinsi ya kusaidia familia zinazolea watoto yatima na kuongeza Taasisi mbalimbali ambazo zimekuwa zikishirikiana na Serikali katika kusaidia watoto hao. Lakini sasa ni jukumu la kupanga mikakati gani ambayo tunaweza kusaidia watoto hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la utamaduni. Katika mchakato wa uchaguzi tumeona vikundi mbalimbali ambavyo vimekuwa vikitoa hamasa kwa kutoa elimu. Ni vizuri sasa na napongeza kwamba Serikali imeunda kitengo kabisa kwa kuwa na Naibu Waziri wa masuala ya utamaduni. Hawa vijana waimarishwe, watambuliwe ujuzi wao na vipaji walivyonavyo halafu wapewe ujuzi ili waweze pia kujiajiri, inaweza kuwa ni njia mojawapo ya kuongeza ajira. Tumeona kuna vipaji mbalimbali vilivyopo huko kwenye jamii, vipaji hivi viendelezwe na viweze kutumika kama njia mojawapo ya kuongeza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la saratani ambayo inawaathiri akinamama. MEWATA wamefanya kazi nzuri kwa kushirikiana na *ITV* nawashukuru. *(Makofi)*

Lakini iwe ni changamoto kwamba sasa tuangalie mpango mahsusi wa kuchunguza akinamama saratani ya maziwa na saratani ya kizazi. Kuwepo na mpango mahsusi ambao utafika mpaka vijijini ili tupunguze tatizo la saratani kwa sababu

akinamama wanakuja kugundua wakiwa wamechelewa sana na wale wa vijijini hawapati huduma muhimu na matokeo yake tunapoteza akinamama wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii ya mimi kujiunga na Wabunge wenzangu kuchangia katika hoja ya hotuba ya Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukupongeza wewe pamoja na Spika kwa kuchaguliwa kwenu kwa kura nyingi au kwa ushindi wa kishindo kuchukua hatamu ya uongozi katika Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niwashukuru kwa namna ya pekee wananchi wa Jimbo la Babati Vijijini, walionichagua kwa kura nyingi sana. Nami naahidi kuwatumikia kwa nguvu zangu zote kwa bidii na kwa unyenyekevu mkubwa kama nilivyofanya miaka mitano iliyopita. Kwangu mimi hii ni mara ya pili, imani yao ndio imenirudisha hapa kutokana na jinsi tulivyofanya kazi pamoja nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua fursa hii kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi mkubwa alioupata yeye na Makamu wake wa Rais na pia nampongeza Rais wa Zanzibar kwa ushindi mkubwa alioupata.

Mheshimiwa Rais Kikwete katika Jimbo langu alipata kura nyingi zaidi ya asilimia tisini na moja, kwa hiyo, anastahili kupongezwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kwake na hatimaye kupitishwa na Bunge hili kwa kura nyingi na sisi tutashirikiana naye katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Nampongeza Rais vile vile kwa hotuba yake nzuri ambayo leo hii tunaijadili humu Bungeni. Hotuba ya Rais wetu ni dira na maelekezo na ni maagizo yanayotakiwa yatekelezwe katika miaka mitano ijayo. Lengo kubwa likiwa ni kuondoa umaskini, kuleta maendeleo kwa kila mwananchi na hivyo kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maagizo haya lazima yatekelezwe katika kipindi hiki cha miaka mitano na hii inahitaji ushirikiano mkubwa sana kati ya wadau mbalimbali wakiwemo wananchi na viongozi wao. Ni lazima kuwe na nidhamu, kuheshimiana na kuwajibika ipasavyo baina ya viongozi wa ngazi mbalimbali katika kumtumikia mwananchi. Uzoefu wangu katika miaka mitano iliyopita unaniambia kwamba kwa kweli suala la kuleta maendeleo kwa wananchi wetu linahitaji ushirikiano kwa ngazi mbalimbali au wadau mbalimbali wakiwemo wananchi kama nilivyosema. Hakika ni lazima kushirikiana kati ya Mbunge na Madiwani, Mbunge na *DC,* Mbunge na Mkurugenzi, Mkurugenzi na watendaji wake. Kwa sababu bila ushirikiano huo hatuwezi kuwafikia wananchi hao. Mbunge mwenyewe hawezi, Rais mwenyewe hawezi, lakini kwa kushirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi pamoja na kuleta maendeleo lakini ni katika vile vile kumtumikia mwananchi huyu katika kuondoa kero mbalimbali ambazo kwa hakika kero hizi ziko ndani ya uwezo wa Madiwani, Mkurugenzi na Watendaji wake, vinginevyo kama hawa wangekuwa wanafanya kazi nzuri kwa uzoefu nilioupata miaka mitano iliyopita ni kwamba kwa kweli matatizo mengi ya wananchi wetu yangekuwa yamepungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe kwenye dira ya miaka 2025. Sasa leo tuko mwaka wa sita, tuna kila sababu ya kuangalia je, tuko ndani ya kipindi au tuko nyuma ya wakati. Sasa haya mambo muhimu na kwa bahati nzuri katika miaka 10 ijayo chini ya uongozi wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete lengo letu ni kuondoa umaskini uliokithiri wanaita *object poverty.* Sasa hili linahitaji katika kipindi hiki cha mwanzo cha uongozi wa Rais wetu kuwa na mkakati mzuri. Bajeti nzuri za kutekeleza ahadi mbalimbali tulizozitoa wakati wa uchaguzi. Ili ahadi hizo ziweze kutekelezwa katika Bajeti ijayo kuanzia Julai maana yake Serikali ije na mikakati ya kibajeti. Bajeti iliyopangwa vizuri ili kwa Bajeti hiyo sasa tuweze kuihoji Serikali katika utekelezaji wake, tuweze kujipima kwamba tumefanya nini kwa mujibu wa mipango tuliyojipangia. Sasa nikienda moja kwa moja katika maeneo mbalimbali yanayotugusa. Nianze na hili la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa mimi natoka Mkoa wa Manyara, Mkoa ambao ni mmoja katika Mikoa iliyo na upungufu wa mvua. Lakini nasikitika na nashangaa kwa nini Wilaya ya Babati haimo katika orodha ya Wilaya zenye matatizo au upungufu wa chakula. Wilaya ya Babati haikutajwa kabisa katika utaratibu wa kutoa chakula cha njaa. Najua Vijiji vingi katika Wilaya yangu au jimbo langu kuna upungufu mkubwa na mvua haikunyesha. Sasa najaribu kuiomba Serikali ilipokee hili kama *DC* au uongozi wa Wilaya haukuleta tatizo hilo. Mimi ninaamini ni katika kupitiwa lakini nasema kwa kweli Babati kuna tatizo kubwa la njaa, watu wenye njaa wapo wanahitaji msaada, kunahitajika msaada wa chakula, chakula cha msaada na cha bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nije kwenye maeneo mengine, eneo la maji. Katika Bunge hili tumezungumza sana habari ya kilimo kwa miaka nenda miaka rudi tukisema kilimo chetu kiboreshwe. Lakini kilimo bila maji hakiwezi kwenda mahali. Lazima kuwe na mkakati uliothabiti kuleta maji au kuwezesha maji kuwepo katika nchi yetu bila matatizo. *(Makofi)*

Napenda kuishauri Serikali kwamba ianzishe mradi wa maji nchi nzima wa kuchimba mabwawa au kujenga mabwawa katika mabonde ya mito. Niseme kuwe na mkakati wa kujenga mabwawa *at least* kila kijiji kiwe na bwawa moja la maji ili kuweza kukinga maji ya mvua. Wakati mvua inanyesha unakuta maji ni mengi sana lakini ndani ya siku mbili hakuna hata tone la maji, kwa nini. Kwa sababu yote yametiririka yamekwenda baharini au ziwani. Mimi nashauri Serikali ianzishe mradi unaofanana na uliowahi kuwepo mradi wa uwiano wa barabara walikuwa wanaita *IRP.* Mradi kama ule uanzishwe ndani ya Wizara ya Maji namshauri Waziri wa Maji akimbie dunia nzima kutafuta fedha za kuhakikisha mradi kama ule unaanzishwa ili kuhakikisha tatizo la maji

linapungua kama sio kwisha katika nchi yetu. Tatizo hili la maji ni la msingi lakini sio mabwawa peke yake lakini vile vile na visima vifupi na virefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la afya. Sera yetu inatutaka tuwe na zahanati mpaka *level* ya Kata. Lakini mimi nashauri Serikali kwamba ili tuweze kusogeza karibu huduma hizi kwa mwananchi, tuhakikishe mwananchi wetu hatembei zaidi ya kilometa tatu kwenda kutafuta huduma hii. Kwa maana hiyo basi, zahanati ziende mpaka kijijini, kila kijiji wananchi washirikishwe kama ilivyokuwa mradi wa MMEM. Wananchi wajenge kwa mfano majengo ya zahanati mpaka kwenye *level* ya *linter* lakini Serikali itoe msaada kwa maana ya kuezeka au kupaua. Mradi huu utakuwa rahisi zaidi lakini huduma za afya itakuwa zimewafikia wananchi wetu katika ngazi za Vijiji. Lakini hili liendane pia na mpango mzima wa kuhakikisha mafunzo kwa waganga ili waweze kutoa huduma hizi za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuleta maendeleo kwa wananchi wetu linahitaji viongozi kuwa karibu na wananchi. Katika jimbo langu la Babati Vijijini tatizo hili ni kubwa kwamba Mbunge wa jimbo hilo ana eneo kubwa sana la kuhudumia. Kwa hiyo, kwa sababu Bunge na kipindi hiki ndio cha kufanyia kazi ya hotuba hii Rais mojawapo basi liwe kugawa Jimbo la Babati na lirudi kuwa Jimbo la Babati Magharibi na Mashariki kama ilivyowahi kuwepo kabla ya kuunganishwa na kuwa Babati Vijijini. Kwa namna hii tunaweza kuwakaribu na wananchi na kufanya kazi nao kwa pamoja na ile dhana ya kwamba Mbunge awe karibu na wananchi wake inaweza kuwa-*realised*. Vinginevyo mwaka unaweza kupita bila kumaliza kutembelea jimbo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisije nikagongewa kengele ya pili nilipenda tu nitaje hayo machache na kadri muda unavyokwenda basi tutazidi kuishauri Serikali tuhakikishe kwamba Rais wetu tunampa ushirikiano mkubwa na wananchi wetu wanapata huduma na ushirikiano unaostahili kutoka kwa viongozi wao ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru sana na mimi ndio mara yangu ya kwanza kusimama hapa Bungeni nakupa hongera sana ya kuchaguliwa kuwa Naibu Spika, hii inaonyesha sisi wanawake tunaweza kwa kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri na wengine wote. Nashukuru sana hotuba ya Mheshimiwa Rais imetufanya tuweze kuchangia sehemu mbalimbali za Majimbo na isipokuwa Majimbo yetu.

Mimi naomba niongelee tatizo la Kanda ya Ziwa. Kanda ya Ziwa nitaongelea kuanzia kwenye kilimo. Kanda ya Ziwa imesahaulika kwa muda mrefu hasa kilimo. Kanda ya Ziwa tulikuwa na kilimo cha kahawa. Kahawa ilikuwa ni kitega uchumi kizuri sana kuanzia kwa mababu zetu lakini kulingana hakina uboreshaji mpaka sasa hivi wa mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea kuhusu ndizi. Kanda ya Ziwa hasa Mkoa wa Kagera hatuna soko. Naomba tuweze kusaidiwa angalau soko la mazao yetu hasa kama ndizi, ukienda kama Uganda unakuta ndizi ina faida sana wanasafirisha ndizi kupeleka nje, wanasafirisha matunda wanapeleka nje, lakini sisi unakuta hasa kama

Wilaya ya Karagwe wanabeba ndizi wanapeleka kwenye masoko madogo madogo wakishakosa muuzaji wanakata kata pale pale. Naomba tufikiriwe tuwe na soko la kuweza kuuza mazao yetu ya kuweza kutusaidia au tuwe na kiwanda cha kuweza kutengeneza kama matunda. Sisi tuna kilimo cha matunda sana kama mananasi matunda *passion* lakini hayana soko tukija tunasema kwamba uchumi haupo. Uchumi hauboreshwi tunavyo vitegauchumi vingi na naomba vianze kuboreshwa tuone kama tutapata uchumi na kuweza kupata ajira za vijana wetu pamoja na wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye Ziwa. Ziwa Victoria kipindi cha nyuma chote wavuvi walikuwa wana uchumi mwisho sana kwa sababu ya kuvua samaki. Nilikuwa nashauri angalau Serikali iweze kutafuta mtego wa kuweza kuwakopesha wavuvi wadogo wadogo ili waweze kujipatia uchumi katika kipato chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye ulinzi na usalama. Ulinzi na usalama sisi Mkoa wa Kagera tulikuwa tunatafuta mchawi kipindi cha uchaguzi watu wengi wamepata shida, akinamama mpaka sasa hivi wengine hawaamki, nina ushahidi na picha zao, mimi ndiyo nilikuwa nafanya hiyo shughuli ya kuweza kuwashughulikia. Lakini tulikuwa hatujapata mchawi leo hii amejitokeza kuonyesha kwamba mimi ndiyo nilikuwa natumia hizo mbinu za kuweza kufanya hivyo. Naomba na hilo jambo liangaliwe. Kiongozi huwezi ukatoa gazeti mambo kama haya amejionyesha kabisa kwamba mimi ndiyo nilikuwa nafanya kitendo kama hicho. Naomba gazeti la Majira lililotoka leo linaonyesha wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye hotuba ya Rais amesema kuboresha biashara, kuwafundisha kuwa na semina ya biashara. Nakubaliana naye na amefanya vizuri sana kwa sababu watu wengi vijana, akina mama wanafanya biashara bila ya kuwa semina. Wakikopeshwa fedha kufanyia biashara, hawaelewi watarudisha vipi na watafanya vipi. Nashukuru sana naomba lianzie kwenye Mikoa. Kwa sasa hii lianzishwe ili tuweze kutoka kwenye umaskini wa mikopo. Mikopo inatolewa kuna mikopo ya *Thinker, Pride* kuna mikopo ya Makanisa lakini kutojua maana ya biashara ndio maana unaona watu wanafanya mpaka mahali akina mama wananyang'anywa hata nguo zao. Naomba na hilo lifanyiwe kazi na nashukuru Rais hotuba yake imetufanya ili tuweze kuwa na nguvu na sisi kuweza kuingia kwenye Majimbo yetu kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye afya. Sisi tuna Hospitali ya Mkoa nzuri sana na ninashukuru sana, ila madaktari na vifaa. Kuna *X-ray* lakini unakuta hawana yule wa kuweza kufanya *X-ray* wanaku-*refer* Bugando unaweza ukakuta hapo hapo huyo mtu aliyem-*refer* Bungando hana hata fedha ya kwenda kule na *X-ray* ipo pale pale. Naomba na hiyo Waziri wa Afya aliangalie katika Mkoa wa Kagera na madaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye elimu. Elimu watoto wengi wameshinda sana mwaka huu lakini shule hatuna ya kuwaweka watoto. Nilikuwa naomba na hilo jambo la elimu lifikiriwe ili watoto wetu walioshinda wengi unawakuta wako nje hawana nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefika hapo nakushukuru sana kwa hotuba hiyo, imetufanya sisi tuweze kusema na kuweza kutoa matatizo yetu tuliyonayo. Namshukuru Mheshimiwa Rais aliyetupa Waziri Mheshimiwa Nazir Karamagi, kuwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. Kwa hiyo, sasa huo Mkoa namkabidhi Mheshimiwa Nazir Karamagi. Kwa hiyo, naomba katika biashara kwanza mboreshe hayo niliyoyatoa ili tuje tuongelee mambo ya semina ya biashara. Huwezi ukafanya semina ya biashara na huku hujaona utafanya nini. Naomba ya kuboresha biashara ianze kwanza kabla ya yote tupate masoko, viwanda halafu wavuvi tuwafikirie kwamba hawa watu ni wanyonge hawana kitu ni maskini wa kutupa.

Kwa hiyo, Serikali ikiweza kuchukua ile mitego angalau wanawakopesha au wananunua kwa sababu usipofanya hivyo wataendelea kunyanyasika wavuvi. Kila anavyoweka mtumbwi kwenye maji anapigwa, akiloa vile visamaki vidogo vya sangara vile anapigwa ananyang'anywa vinachomwa na kumwagiwa mafuta ya taa. Kweli huo ni unyanyasaji na ziwa ni letu lilileltwa na Mwenyezi Mungu.

Kwa hiyo, mtu lazima uchukue kitega uchumi kwenye kitu ambacho kiko pale hatununui wala hatufanyi nini. Naomba hilo jambo la wavuvi, Kanda ya Ziwa wote wameteseka sana, wanapigwa, wanafuatwa Ziwani wanapigwa wanadumbukizwa kwenye maji na mitego yao inachomwa, kwa hiyo, naona hiyo semina bila ya kuanza kutayarisha hivi vitu itakuwa ni sawa sawa na wafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishia hapo. Nashukuru sana na nilikuwa naendelea kuboresha hiyo hotuba ya Mheshimiwa Rais, nisije nikapigiwa kengele labda ndio siku nyingine utanikubalia nisimame kuongea. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Nkasi, kwa kunirudisha kwa mara ya tatu mfululizo. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na eneo ambalo Mheshimiwa Rais alielezea majukumu ambayo yataweza kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano, majukumu ambayo yako 10. Nijikite katika jukumu la 5 na 6. Naomba kunukuu alisema kwamba: "Serikali ya Awamu ya Nne itaimarisha uwezo wake wa kulinda maisha na mali za raia wake, tutapambana na uhalifu wa kila aina na majambazi hayataachwa yatambe yatakavyo."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mfupi uliopita majambazi yamekuwa yakitamba yatakavyo. Hii ni uvunjaji wa amani, ni uvunjaji wa kauli ya Mheshimiwa Rais. Wanaopambana na majambazi pale wanapoyashika pengine kwenye *Television* huwa tunawaona. Tunaona hata silaha walizozitumia lakini Waziri anayehusika aende akatazame ni rekodi ya namba zipi zilizotumika na wamiliki wake ni akina nani yaani wale wa awali. Mawili, moja unaweza ukagundua kwamba baadhi ya silaha zilizotumiwa hutoka *armoury,* lakini inawezekana sana hutapata hizo namba. Utazionesha tu kwenye *Television* namba zake hazipo, lakini ndio zile zile zinazotoka *armoury* nani anazitumia, nani anaziruhusu zifanye hivyo. Nendeni mkachunguze haya mambo katika ofisi zenu. Kuna baadhi ya walinzi wetu ambao sio waaminifu wakubwa kwa wadogo,

wanashirikiana na majambazi. Mbaya zaidi ajira inayotolewa kule hasa chombo cha polisi wengi utakuta ni mtoto wangu, mtoto wa dada, mtoto wa mjomba na hao hao ndio wanaofanya ujambazi kutafuta mali hizo. Namba hamtaziona, mtaona tu lundo la silaha lakini baadaye zitarudi *armoury*.

Katika eneo la 6 nanukuu amesema: "Serikali ya Awamu ya Nne itahakikisha mipaka ya nchi yetu ipo salama, hatutaruhusu mtu au nchi yoyote kuchezea mipaka ya nchi yetu na uhuru wetu." Ziwa Tanganyika kuna ujambazi mkubwa mno na wanaofanya ujambazi ule ni wenzetu kutoka Kongo na walio wengi ni kutoka Jeshi la Kongo. Hao ndio wanavamia katika eneo. Wanajeshi waliopelekwa kule ni wachache mno na sana sana wamekaa katika vituo vikubwa viwili au vitatu Kigoma, Kirando na wanatembelea baadhi ya maeneo kama vile Karema na Wampembe lakini hawako katika vituo hivyo vikubwa na maeneo hayo ndipo Wakongomani wengi wanaingia na kufanya uhalifu mkubwa. Wananchi wanapokwenda kuvua wananyang'anywa mali zao, wanauawa na mara kadhaa huwa tunapata taarifa kwamba mali zile zilizoibiwa ziko kule Kongo na wanadai njooni mzichukue atakayekuja kuzichukua ahakikishe ana dola 300 au 400 wengine uambiwa 500 kutegemea na chombo kilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, huo sio uvamizi wa mipaka wa wazi wazi? Naomba Serikali basi iweze kuimarisha Jeshi la Wananchi ambao wako kule pamoja na vyombo vyake vya kisasa ili kusudi eneo la Ziwa Tanganyika liweze kulindwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amesikitishwa sana na mpasuko ambao upo kati ya Pemba na Unguja kule Zanzibar. Akasema kielelezo alichokitoa ni Uchaguzi Mkuu ambao umeonyesha wazi wazi mpasuko huo. Mimi niliwahi kufanya kazi kule Pemba takribani mwaka mmoja na miezi nane, miaka ya nyuma kidogo. Wakati ule nimefanya maeneo ya vijijini pia maeneo kama vile ya Wambaa, Makombeni, Ole Kiuyu, Kangagani, Mtambile na maeneo ya kule Micheweni. Nimejaribu kukaa maeneo hayo Chake Chake pamoja na Wete.

Mimi ni Mkristo lakini nililazimika kwenda kusali msikitini wakati ule misikiti ya Kizota inajitokeza ndio vuguvugu lile la kuanza kudai vyama vingi na baadhi ya wahusika kutoka kwenye Serikali yetu kuingia huko. Mambo yaliyokuwa yanasemwa humo siwezi nikayasema hapa lakini ni yale yaliyopelekea baadhi ya vyama fulani kuundwa na Makao yake Makuu yakiwa Uarabuni hadi leo Tanzania ni kiini macho. *(Makofi)*

Nilipokuwa eneo la Mkoani ilikuwa ni mwezi wa Ramadhani, nakumbuka nilikwenda sokoni nikakuta wanauza vitumbua nikanunua. Niliponunua nilifuata Ubara wangu nikala kitumbua pale pale nikashikwa. Niliposhikwa kwamba umevunja sheria kula hadharani mwezi mtukufu wa Ramadhani nikajaribu kujitetea, nilimwona Mswahili mwenzangu mwenye nywele za kipilipili kama mimi mweusi kuliko mimi akasema *yakhe* unajua sisi tabia zetu Waarabu huwa hatuwezi tukavumilia mambo haya. Nilichukia na kumtukana kwamba wewe mweusi kuliko hata mimi halafu nywele za kipilipili una Uarabu kiasi gani. Akajibu sisi ndivyo tunavyotaka Waarabu hatutakitaki mambo mengine haya ndiyo maana mnatusumbua. Nilikaa kimya. Matokeo ya Pemba

sisemi mtu kwa rangi, nasema kwa tabia ni wale wanaodhani Pemba ni Kisiwa cha Waarabu na lazima kirudi kwa Waarabu na hao ndio wanaoleta mpasuko. Wale wanaokaa maeneo ya Gando. Gando kule Wasukuma wengi wanalima kule, lakini hufukuzwa kwamba mrudi kwenu. Wakati ile ni Tanzania lakini wanafukuzwa mrudi kwenu. Kwenu wapi? Bara. Mbona sisi Bara hatuwafukuzi Wapemba waliojaa kila eneo? Naomba Watanzania wenye asili ya Tanzania tuwe macho. Tuwe macho vinginevyo na sisi tutakuwa katika hali hiyo ya kusema sisi ni Waarabu wakati sisi sio Waarabu, sisi ni Waafrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika rushwa. Upande wa rushwa kwanza anayetoa rushwa anapenda kutoa rushwa na anayepokea rushwa anapenda kupokea rushwa. Kudhibiti rushwa ni ngumu ingawa tunajitahidi. Nasema hivyo kwa sababu gani? Mbaya zaidi ni pale unapoona vyombo vya haki ndivyo hivyo vinavyokumbatia rushwa. Mimi ningetegemea kama ningekuwa polisi, ningekuwa polisi wa kufuata sheria. Lakini ukiingia polisi ni mtaji. Ukiingia polisi unaomba uende *traffic,* ama uende upande wa upelelezi, ni mtaji. Kama nilikuwa kembamba kama mimi baada ya siku mbili, tatu, nitaota kitambi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama. Kuanzia Mahakama ya Mwanzo sina uhakika na Mahakama Kuu lakini hadi Mahakama ya Hakimu Mkazi walio wengi ni wala rushwa, ni wachache tu ndio wanaokataa rushwa, wengi wanakubali rushwa. Vyombo vya ajira hali kadhalika. Mtu yeyote kama unatafuta uongozi wa aina yoyote tusidanganye kama wengine tupo hapa ukishatoa rushwa utapokea rushwa ama utadai rushwa. Maana fedha unayoitoa au mali unayoitoa ni yako wewe umeitafuta, kwa nini utoe ili upate uongozi? Ni nani anayetoa mtaji halafu akategemea kupata hasara na akafurahia hasara. Ukitoa mtaji lazima unategemea kupata faida. Ukitoa rushwa kwa dhumuni fulani unategemea upate hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo vita ni lazima tuipige wote si suala la kusema mdomoni halafu ukatenda vitendo vya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kukwepa kodi. Ni wakubwa wangapi ambao hatuna teksi bubu? Wakubwa katika vyombo vyote viwe vya usalama, viongozi mbalimbali na kadhalika ni nani kati yenu? Mimi binafsi nimekuwa nikikataa nikiona kuna teksi bubu namwambia wewe hulipi kodi nachukua ile yenye namba nyeupe. Wananiambia Mheshimiwa tunalipa hivyo hivyo mbona ni za wakubwa. Sipandi teksi bubu kwa sababu hailipi kodi, napanda ile yenye namba nyeupe. Lakini walio wengi tunayo mateksi bubu. Je, kodi tutachangiaje? *Guest House* bubu, vioski bubu. Tunakwenda kununua vifaa hatudai risiti. Tunakwenda mahali tunalazimisha misamaha ya kodi. Unategemea tutengeneze nchi vizuri iwe maji, hospitali, barabara, mishahara, marupurupu mbalimbali sisi wenyewe hatuchangii kodi vitatoka wapi na wala hatusimamii uovu wowote unaotokana na uchangiaji wa kodi vitatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, uvunjaji wa sheria mbalimbali. Hivi juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa amri kwamba pombe yoyote ya nafaka isitengenezwe maana

huwezi ukafa kwa kutokunywa pombe, lakini watu wanatengeneza, viongozi wapo hawasimamii, unategemea nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na napenda kukushukuru, pia napenda kukupongeza kwa kuteuliwa kwako kuwa Naibu Spika. *(Makofi)*

Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwa kuteuliwa kwake na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano kwa kura nyingi kuwa Spika wa Bunge hili. Napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Wilaya ya Ilemela kupendekeza jina langu kuwa mgombea wa Viti Maalum na kulituma katika Chama Taifa. Shukrani kubwa naipeleka kwa uongozi wa Chama cha *CUF* Taifa, kuteua jina langu kuwa Mbunge wa Viti Maalum katika Bunge hili lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Napenda kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa asilimia mia moja kwani hotuba hii imejitosheleza na sisi tunafanya kama ni kuchimbua chimbua kupaka mafuta na kuongeza tu, lakini hotuba hii imejitosheleza. Mheshimiwa Kikwete kwa busara zake na hekima yake amegusia nyanja zote katika hotuba hii. Amegusia mpasuko wa Pemba kwani ameuona kabla yetu sisi. Amegusia kilimo, elimu, kazi na kadhalika.Kwa hiyo, hakuna alichobakiza katika hotuba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia upande wa kilimo. Tumeongea kuhusu njaa, kweli njaa ipo, sasa kama njaa ipo tufanye nini? Chakula cha msaada kimekwisha patikana. Je, tutasaidiwa mpaka lini? Naiomba Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika wakati tunajadili njaa na chakula kitapatikana vipi kianze moja kwa moja sasa hivi suala la kilimo. Najisikia vibaya na ninaona aibu sana ninaposikia Mikoa ya Kanda ya Ziwa ina njaa wakati Mikoa hiyo imezungukwa na Ziwa Victoria ambalo linaweza likalisha Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Mikoa ya jirani. Naomba Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, iangalie hili mapema sana kabla ya chakula ambacho tunaomba hakijaisha na iweze kuelekeza nguvu zote Kanda ya Ziwa kwa kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si kuelekeza nguvu tu, waelekeze wataalam, vifaa vya kutendea kazi na mbolea. Kwani sasa hivi Wizara ya Kilimo imekuwa ni Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Lakini wataalam, mabibi shamba na mabwana shamba wao hukaa mjini. Hawawezi hata kufika kule kijini na kuangalia wakulima wanalima vipi, hii mbolea tunayowapa wanaitumia vipi, je, wanaiweka kwa kiwango kinachotakiwa au vipi? La! wao hukaa mjini. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika iliangalie suala hili upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kurudi kwenye usalama wa raia na mali zao. Wengi tumelituhumu Jeshi la Polisi, wengi tumelipongeza Jesho la Polisi. Lakini na mimi pia napenda nichangie upande huo. Tumesema kwamba Jeshi la Polisi wanahitaji vifaa. Jeshi la Polisi wanahitaji makazi bora. Mfano Jimbo ninalotoka mimi wanamoishi polisi

hawa ni aibu hata mtu kwenda kupaona. Polisi kalala ndani nyumba imepasuka mtu ukiwa nje unamwona. Ninaomba Wizara hii iiangalie polisi upya.

Lakini pamoja na kuwaangalia polisi hawa upya, napenda pia niwatuhumu polisi hawa hawa. Pamoja na kuwatetea lakini polisi ndiyo wamekuwa chanzo kikubwa cha mgogoro. Polisi huyu akimkamata kibaka anampeleka *central.* Akimfikisha pale yule kibaka atakaa ndani siku moja au ni jambazi kabisa anakaa ndani siku moja, kesho yake anatoka nje anakwenda. Kaongea nini na *OCD,* huelewi. Kesho yake na yeye huyu polisi akimwona jambazi hamkamati anamsaidia kuiba. Tatizo la ulinzi na usalama liko kwa wakubwa na si kwa polisi wadogo wadogo. Wanakamtwa majimbazi wakubwa wanapelekwa na silaha wakishafikishwa kule ndani, anaongea siku mbili, tatu, mtaisikia kesi inaanza kuunguruma itakapoishia hamuielewi. Aliye mhukumu hamtamwona. *(Makofi)*

Polisi hawa hawa wakubwa, inatokea kipindi unatokea msako.Wakati wa msako kwa mfano kule Jimboni kwetu msako wa gongo, japo ni pombe haramu vifaa vinapatikana vya kusaka gongo. Polisi na bunduki wanakwenda kusaka gongo chupa moja. Lakini ikitokea ujambazi Polisi humwoni, majambazi wakiondoka ndiyo polisi wanakuja, vifaa havipatikani kwenye ujambazi. Kwenye gongo chupa moja vifaa vinapatikana japo ni pombe haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea polisi hawa hawa anapojeruhiwa mtu akapelekwa polisi anakwenda hospitali, akishafika hospitali anapewa *PF3*. *PF3* ikirudishwa polisi kama yule mtu kajeruhiwa vibaya aliyemjeruhi anakuja kuhonga polisi, *PF3* inapotea matokeo yake ushahidi unakosekana yule mtu ameumia kiasi gani? Nina mfano hai, kuna bwana mmoja anaitwa Karumi katika Jimbo la Rorya, bwana huyu kajeruhiwa kwa mapanga yasiyopungua 16, kapigwa na risasi kachukuliwa mpaka Bugando. Amelazwa Bugando siku ya siku anakuja polisi anasema ametumwa na *OCD PF3* ijazwe, polisi amefikia kiasi cha kumuamrisha daktari ajaze *PF3* wakati mgonjwa bado mahututi. Naomba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, iangalie suala hili, anaomba *file* lipotee ili mgonjwa ashindwe kutibiwa na kweli, *file* limepotea na mgonjwa sasa hivi anatibiwa bila *file.* Naomba Wizara ya Afya na Ustawii wa Jamii, kupitia kwa Wakurugenzi wa Afya waliangalie suala hili upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii na penyewe tutasema kwamba polisi wanahitaji vifaa? Kuiba *PF3* polisi anahitaji kifaa? Kwa kweli Jeshi la Polisi limepoteza imani kwa wananchi, Jeshi la Polisi limepoteza maadili ambayo kikawaida alipokwenda kula kiapo amekwenda kinyume na kiapo na hii yote si polisi wadogo wadogo tunasema kwamba Mheshimiwa Jakaya Kikwete amesema kwa nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya tunaomba aanzie kwenye Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia eneo la madini, Mheshimiwa Rais amesema kwamba ataangalia mikataba ya madini upya. Katika mikataba hiyo atakayoiangalia upande wa madini, mimi ninatoka Kanda ya Ziwa, naomba kwanza aangalie kwa haraka zaidi aliyefunga mkataba wa kuihamisha nchi ya Tanzania ndani ya Tanzania na kuipeleka nje ya nchi ya Tanzania kama Japan na nchi zinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanafunga mikataba mpaka mtu anafunga mkataba wa kuchukua mchanga ndani ya Tanzania na kuupeleka nje ya Tanzania kwa muda wote. Je, baada ya mkataba huo kuisha tutabaki na mashimo, tutawaeleza nini watoto wetu na wajukuu na watayafukia vipi mashimo haya? Naomba Mheshimiwa Rais, aangalie upya mikataba ya madini hususan Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye Afya, afya kimekuwa kikwazo, akinamama wengi wanakufa Tanzania kwa ajili ya afya, wanakosa huduma bora. Pale tunakuwa sisi tunaona ma-*nurse* wanasoma miaka minne ndio wanakuwa *nurse.* Lakini leo hii *nurse* hata akisoma miezi sita anaruhusiwa ruksa sindano atakuchoma, dawa atakupa na hata atakuandikia kama daktari, hii inapelekea kutojua huyu anaumwa nini, unafika hospitali wewe unaumwa *pressure* unaongezewa maji ambayo hayahusiani na ugonjwa unaoumwa, kwa sababu ni yule *nurse* tu hana elimu ya kutosha. *(Makofi)*

Tungewaomba basi Wizara ya Afya iangalie upya elimu za ma-*nurse,* elimu za madaktari. Pia iangalie upya ni jinsi gani watu wanavyohangaika, akinamama wanakuja kujifungua, mama amejifungua, akinamama watatu wote wanalazwa kitanda kimoja. Kuna magonjwa ya mlipuko, tumesema kuna magonjwa ya kuambikiza, watoto watatu akina mama watatu kitanda kimoja na kitanda hicho kila mama mmoja amekichangia shilingi 2,000. Hapo hujaambiwa kwamba dawa, hujaambiwa kwamba yaani kadi aliinunua kwa shilingi ngapi kitanda kimoja. Ina maana kitanda kimoja kinalipiwa shilingi 6000, mtu mwisho wake unafikia kusema ni bora hata ningelala *guest house* peke yangu ningeambiwa kitanda kimejaa kuliko kwenda hospitali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tunaiomba iangalie upya masuala ya akina mama, kwani hakuna mtu ambaye hakuzaliwa na mama duniani, kila mtu amezaliwa na mama. Kwa hiyo, tunawaomba upande wa maeneo ya kujifungulia akina mama myaweke yawe stara na siyo yawe wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hotuba hii ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, imejitosheleza tunachokiomba ni Mawaziri, Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na viongozi wengine wote tuweze kumsaidia shughuli hii ili aweze kufanya kazi kwa ufanisi na ili awe kutekeleza na kufikia azma aliyoitarajia kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja katika hotuba nzuri sana ya Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Kikwete.

Awali ya yote naomba nikupongeze sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi yako kuweza kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge hili Tukufu, pia naomba nimpongeze Spika wa Bunge hili unifikishie salaam zangu kwake.

Pia naomba niwapongeze, kwanza nimpongeze Waziri Mkuu kwa kuchaguliwa kwake, kuteuliwa kwake na kupitishwa na Bunge hili Tukufu kwa asilimia mia moja.

Nawapongeza Mawaziri wote na Manaibu Waziri kwa nafasi zao, pia nawapongeza Wabunge wenzangu wote ambao wamepata nafasi hii ya kuwepo hapa kujadili maendeleo ya wananchi na pia naomba niwapongeze wanachama wa chama changu cha *CUF* kwa kuniwezesha kuwepo hapa kuungana na Wabunge wenzangu kuweza kujadili maendeleo na kuwasaidia katika maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja kwamba hotuba ya Rais inajitosheleza na inajikamilisha, tunachofanya sisi wachangiaji ni kuweza kugusagusa na kuweza kuangalia kipi cha kuongeza kidogo kwa kuchangia na ile ambayo ameweka yeye iweze kufanya kazi na kuweza kutimia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitachangia kwenye suala la mazingira. Hali ya mazingira, hasa uharibifu wa mazingira kwa hapa Tanzania sasa hivi inakithiri na imetishia usalama. Hali ya uhifadhi kwa Tanzania kwa kweli imerudi nyuma kwa asilimia karibu 90 mpaka 80 na hali hii inajionyesha wazi kwenye hali ya hewa ambayo imebadilia, sasa hivi tuna kilio cha njaa, tuna kilio cha kutokuwepo na maji ya kutosha kwenye Mito na hivyo tuna kilio cha kutokuwepo kwa umeme wa kutosha na vilio vingine vingi ambavyo ukiangalia kiini chake hasa unaenda kwenye uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uharibifu wa mazingira hapa Tanzania haikuanza ghafla. Imeanza kidogo kidogo na Wizara, Serikali, jamii ikiwa inaangalia na hali kufikia hatua hii. Tukijaribu kuangalia huko nyuma, hali ilivyokuwa, wazazi wetu au wazee wetu walikuwa na mbinu za kuweza kufanya ili kuweza kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kuhifadhi mazingira, walitumia hata mbinu za kusema kwamba msitu fulani ni msitu wa Jaji au ni msitu wa mila, hiyo walitumia ni kama kauli tu kwa watoto na wajukuu, lakini nia ilikuwa ni kwamba uhifadhi wa mazingira uwepo kwa ajili ya kuhifadhi vyanzo vya maji, kuhifadhi misitu, kuhifadhi mali asili zilipo na vinginevyo, ili kuhakikisha kwamba hali ya nchi inakuwa na maji ya kutosha kipindi chote cha mwaka.

Lakini kidogo kidogo hilo limeanza kupuuziwa na vizazi baadhi ya vizazi vimeanza kukata ile misitu ambayo ni misitu mikubwa, misitu yenye maji ya kutosha na hali imefikia sasa imeleta ukame katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa sasa hivi ni sisi wote kwa pamoja kuisaidia Serikali kurejesha hali iliyokuwepo huko nyuma kila mmoja kwa nafasi yake. Kuna mbinu mbalimbali ambazo huku nyuma zimekuwepo, kwa mfano kuwepo kwa sera ya ushirikishwaji. Mimi sera hii naiunga mkono kwa asilimia mia moja, kwa sababu unapomshirikisha mwananchi katika kuhifadhi eneo linalomhusu, kwanza unamjengea ile dhamira kwamba hii ni mali yako. Kwa hiyo, ukimwezesha akianza kufanya ile kazi ambayo unampa kikamilifu kwa kweli matunda yake yanakuwa ni mazuri, na ni kwa sababu yeye yuko jirani sana na yale mazingira na maliasili ambayo anaihifadhi, inakuwa ni rahisi kumtumia yeye kulikoni hata ukitumia watu wengi kutoka nje hata wataalam na watu na wengineo.

Lakini kwa upande wa kutumia huu ushirikishwaji, inabidi Serikali iangalie kwa makini sana kwa mfano nikichukua mfano kumekuwepo na ushirikishwaji wa misitu ambao tunaita ni *Forestry Participatory Management*. Halafu kuna tena ushirikishwaji wa kuanzisha maeneo ya hifadhi za wanyamapori ambayo ni *WMA's* ushirikishwaji huu utafanya kazi na kuweza kuleta manufaa kama Serikali itaangalia *implementation* kuangalia ule utekelezaji wake uwe wa haraka na wa manufaa kwa wananchi. Nikijaribu kuangalia kwenye suala la ushirikishwaji wa kuanzishwa maeneo ya Hifadhi za Wanayamapori, wananchi wamekuwa wanajitolea. Ilipoanzisha huu mfumo wananchi wengi sana wamejitolea maeneo mengi ya Tanzania wapo wananchi ambao walitenga maeneo ya misitu yao wakaanza kuilinda na kuihifadhi kwa nguvu kwa nyezo zao ndogo walizokuwa nazo, wakawa wanafanya doria, wanafanya *patrol* mara zote na wakahakikisha kwamba kwa kweli karibu kila kijiji kina eneo ambalo limelindwa ili lisizidi kuharibiwa

Lakini kwa hali inavyokwenda sasa wananchi wameanza kukata tamaa kutokana na kwamba ile *implementation* yaani utekelezaji wake unakuwa ni mgumu. Wananchi wanakuwa wanasubiri, sasa tumeanza kuhifadhi miaka zaidi ya nane mpaka sasa hivi, lakini mbona hatupewi ile dhamana, mbona hatupewi ile nafasi ya kuweza kusimamia kikamilifu maliasili hizi. Kwa hiyo, unakuta kwamba kanuni ambazo zimewekwa kwa ajili ya kuwezesha mpango huu ni ngumu na zinamahitaji makubwa sana kiasi kwamba wananchi wenyewe wanashindwa kuweza kutekelezwa.

Kwa hiyo, ninachoomba kwa Serikali kwa kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii ijaribu kuangalia tena kanuni hizi kwa karibu iondoe vile vikwazo vinavyoonekana kwamba hivi vinasababisha utekelezaji wa huu mfumo kutokuwepo, iondoe iweke vile vigezo muhimu ambavyo vitawezesha wananchi kuweza kupewa ile hadhi ya kusimamia maliasili zao.

Pia kwenye suala la ushirikishwaji, wasishirikishwe wananchi tu, washirikishwe pia wale wadau wote. Kuna viwanda ambavyo vinatumia maji kutoka sehemu mbalimbali na wao pia ni wadau wa maji haya pia washirikishwe kwenye kuhifadhi vyanzo vya maji, washirikishwe kwenye kuhifadhi misitu, washirikishwe kwenye kuangalia vile vyote ambavyo kwa sababu bila kuwepo kwa maji viwanda vyao haviwezi kufanya kazi.

Kwa hiyo, naomba ushirikishwaji uende pia kwa wao wenye viwanda vikubwa ambavyo vinatumia maji, uende pia kwa watu ambao wana mashamba makubwa japo wako mbali na vyanzo vya maji lakini wanatumia maji yale. Pia ushirikishwaji uende kwa watu kama hao, wawashirikishe ambao wale ni makampuni au ni mashirika au ni watu wakubwa ambao wanatumia maji washirikishwe ili wote waweze kufanya kazi ya kuweza kuhifadhi mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, nizungumzie suala la ujambazi au suala la usalama wa raia. Usalama wa raia kwa nchi yetu sasa hivi kweli linatoweka. Amani tunayosema, lakini amani inaelekea kupotea. Sasa hivi imefikia hatua kwamba mtu unalala usiku huna uhakika kwamba utaamka ukiwa salama, unasafiri huna uhakika kama utafika kwa usalama, unaenda labda benki unaenda labda kwenye *Bureau de Change*

unaenda sehemu yoyote ile huna uhakika na maisha yako. Wengine tuko hapa sasa hivi lakini huna uhakika nyumbani kule kuna usalama kutokana na kwamba ujambazi umekithiri. Kwa hiyo, tunaomba hali ibadilishwe, kwa kushirikiana sisi wenyewe na kwa kushirikiana na Wizara husika, Wabunge tutafute mbinu ya kuweza kuondoa hili, hili karibu kila Mbunge kwa kweli ameligusia na mimi pia linanigusa ninaomba hali hii ibadilishwe ili wananchi waweze kuwa na amani. Ni uwogo kusema kwamba tunaamani, wakati huna uhakika na maisha hata nusu iliyoko mbele yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa zaidi ambacho kinaniuma kuliko vyote kwenye ujambazi unaofanyika, ni kule kudhalilishwa, bora mtu aingie ndani achukue mali aondoke, lakini kinachofanyika, majambazi wanaingia wanachukua mali wanafanya vitendo vya kinyama kwa wenye nyumba. Wale wanaosafiri barabarani labda wametekwa, magari yametekwa wanawavua nguo wanawalaza chini wanafanya vitendo vya ajabu kwa wanawake, kwa kweli hilo linauma, linauma sana, ni bora mali ipotee lakini amani iwepo. Sasa utaniambia niwe na amani inatoka wapi, wakati sina imani ya maisha yangu kwa muda wote ule, kwa hiyo, naomba hilo liangaliwe kwa kweli, vitendo vya ajabu wanafanyiwa wanawake uzalilishwaji zaidi ya hata ya mali ambazo zinachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nagusia kwa ufupi ni suala la rushwa. Kwa kweli suala la rushwa kwa nchi yetu, sijui hata niseme nini, inasikitisha na inatia huruma na hasa pale rushwa inapozidi kwenye maeneo ambayo yanatoa huduma muhimu kwa jamii. Maeneo kama hospitali, sio watu wote ambao wana hela au wana uwezo wa kutoa rushwa ili wapate huduma ya matibabu, lakini ukishangaa ukienda hospitali, kuna vibao vikubwa kabisa *corruption free zone, corruption free zone,* hakuna rushwa lakini ukiingia ndani bila kutoa hela hupati huduma, utashinda kwenye kiti muda wa siku nzima hakuna huduma. Utakuwa unapigwa dana dana nenda hapa, nenda hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iangalie hilo kwa hii awamu, tunaimani kabisa kwamba kwa kuwa Rais wetu ametambua hilo na amegusia yote haya katika hotuba yake ninaimani kabisa kwa ushirikiano wa Wabunge wote tukimpa nguvu Rais wetu pamoja na Wizara husika yote haya yanawezekana. Tunaomba kwa kweli haki itendeke na hasa kwenye hospitali ambapo ndipo uhai wa watu. Hili linagusa uhai wa mtu moja kwa moja, bila kupata huduma unapoumwa huwezi kufanya shughuli ya maendeleo, huwezi kufanya shughuli nyingine yoyote ile. Kwa hiyo, tunaomba suala la hospitali liangaliwe japo sehemu zote ni muhimu hasa pale ambapo uhai wa mtu upo, naomba liangaliwe kwa makini sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naunga mkono hotuba ya Rais wetu kwa asilimia mia moja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuturejesha katika Bunge hili Tukufu na kuwafanyia kazi Watanzania.

Pili, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitawashukuru kweli kweli watu wa Jimboni kwangu kwa kufanya kazi ya ziada kunirejesha hapa na kuitoa jino CCM bila ya ganzi katika Jimbo la Mji Mkongwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alitumia saa mbili kuhutubia, *two hours* haikumchosha mtu yeyote ndani ya Bunge hili na Tanzania hii, hotuba yake iliyojaa busara, hekima, maazimio na ahadi za maendeleo kwa nchi yetu ya Tanzania na haikutoa peke yake kwa Watanzania, imetoa imani hata katika Jumuiya ya Kimataifa, kwamba Tanzania sasa tumepata *capable President. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akatunga hotuba akatuletea hapa ili tuichambue Wabunge na sisi *maturity* yetu ya kisiasa ni kubwa sana ndio maana tukaletwa hapa ili tujadili masuala ambayo yanawagusa wananchi waliotuchagua hapa kwa niaba yao ili kuijenga Tanzania, kuwa Tanzania yenye siasa na demokrasia ya kweli na uchumi wa kisasa utakaoinua hali za Watanzania katika nchi yetu. Jambo lililonigusa na ambalo nalifurahia nam-*encourage* Mheshimiwa Jakaya Kikwete, ni kufuatilia kwa karibu sana masuala ya kisiasa yaliyorejesha nyuma sana sana maendeleo ya Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba yaani Zanzibar. *(Makofi)*

Kuna watu wamei-*hijeck* hii hotuba wanaelezea tofauti na anavyotaka kufanya Mheshimiwa Jakaya Kikwete. Mheshimiwa Jakaya Kikwete asirudi nyuma, tuko pamoja naye tutampa ushirikiano ili kuondoa *crisis* za kisiasa katika Visiwa vyetu na amesema kwamba atahakikisha kabla ya kumaliza muda wake atakwenda zaidi ya muafaka ili anapoondoka madarakani aone mpasuko wa kisiasa ambao unaitwa jina la kwamba kuna Wapemba na kuna Waunguja, kuna Wazanzibari na Wabara unaondoka na linabakia suala moja tu kwamba kuna Wazanzibari na kuna Watanzania kwa sababu ni Serikali mbili tofauti zinazoendeshwa na Katiba mbili tofauti Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusijenge hisia za kwamba hiki chama ni chama cha Wapemba, *is a wrong concept*. Hiki si chama cha Wapemba ni chama cha Watanzania *registered fully,* na kimechukua *qualification* zote za kujulikana, *is the political party*. Hivi kweli Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, alichaguliwa na Wapemba kule Bukoba Mjini? Mimi nimechaguliwa na Wapemba watupu kule Jimbo la Mji Mkongwe, hapana, *is real wrong.* Hiki ni chama cha kisiasa, si cha kigaidi kama wengine wanavyokifikiria na kukitafsiri hivyo. Kwa hiyo, sisi lazima tujenge misingi imara na kusimamia ukweli wa mambo ulivyo kama alivyochangia Mheshimiwa Wilson Masilingi kwamba iundwe Tume maalum ambayo haita- *base* upande wowote, iende Zanzibar, ije Bara tukae na viongozi wa vyama vyote CCM, CHADEMA, *TLP, CUF* tuondoe tatizo lililopo Zanzibar. *(Makofi)*

Waheshimiwa, mpo…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, unapozungumza unamwambia Spika. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, leo asubuhi kabla ya kuja Bungeni nilifungua *television* nikayapitia magazeti haya hapa yote yamekivuruga na kukipaka matope Chama cha Wananchi *(CUF)* kwamba kinahusika moja kwa moja na hali ya ujambazi uliopo Tanzania.

Jamani hebu tuzungumze ukweli, *ethics* za kazi ziko wapi hapi hapa. Iwapo Omar Mahita tunayemtegemea, tunayemtarajia kuongoza Jeshi la Polisi la Tanzania kuondoa uhalifu, kuondoa *crisis* hizi, anakuja na kauli kwamba sisi tunahusika. Tunahusika vipi?

Kwa kuonyesha visu vyenye rangi ya *blue,* kwani ujambazi uliofanyika Ubungo, watu walikwenda na visu pale, walikwenda na mapanga pale? Walitumia *AK 47,* walitumia *Sub Mashine Gun* na si hasha kesho wakatumia *bazooka* kubomoa mabenki yetu na uchumi wa nchi yetu kwa sababu tu ya utashi wao wenyewe. Ujambazi hauchagui chama wala rangi, wala kabila, wala jinsia. Waweza ikawa jambazi akatoka CCM, akatoka *CUF,* akatoka chama kingine chochote, ukawa hauna chama ni ujambazi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusiwe na *concept* ya kuwa hiki chama ni chama cha kigaidi ni chama cha kisiasa sio *guerilla party, is a political party* kilichokuwa *matured* chenye viongozi waadilifu wenye uwezo. Afute kauli hii na akitake radhi kwa maandishi kwa Chama cha Wananchi *(CUF)* kwamba sio chama cha majambazi, wala hatuhusiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, alisema kwamba ujambazi uko mpaka *Lake Tanganyika,* uko mpaka Ukerewe. Je, huko vile vile viongozi wa *CUF* wanahusika na ujambazi huo? *Is ridiculous.* Sisi tunachotaka kusema Jeshi la Polisi hatujalilaumu, tunataka lipewe zana za kisasa lifanye kazi ya ziada, liwakamate majambazi na kama kweli wapo viongozi wa *CUF* wanaohusika na suala hili wakamatwe, wafikishwe katika vyombo vya sheria, waonekane katika nchi hii.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna silaha hata moja. Hata hivyo visu ilikuwa tu, labda kama haikuwa *fabricated,* ni *business* mtu anaweza akatia nembo ya rangi ya kijani, ya bluu kwa sababu ya biashara yake na wakati ule. Lakini haina maana kuchukua kisu ukakionyesha katika vyombo vya habari ukasema hiki kisu kimeletwa na *CUF* na mfanyabiashara ambaye mpaka leo hatujaonyeshwa katika chombo chochote wala mahakama yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuwe waangalifu sana katika masuala ya Kitaifa. Sisi hapa tunawawakilisha watu, hatuwakilishi vyama. Anapokuja mgeni akaingia katika jengo hili akaona namna tulivyokaa haulizi yule ni Mheshimiwa kutoka chama gani yule ni chama gani? Anajua kwamba kaingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Muda ni mfupi sana lakini nina mambo mengi sana ya kuongea. Kwa kuwa Shirika la Ndege la Tanzania ni miongoni mwa mashirika ya Muungano, tunataka tujue na sisi Wazanzibari *share* yetu ni kiasi gani katika Shirika lile. Tunataka tujue tunapata kiasi gani kwa kila mwaka. Tunataka tujue tunashirikishwa vipi katika mikataba ya

kuliingiza Shirika hili na ubia na Shirika la Afrika ya Kusini. Ndiyo haki ambazo Wazanzibari wanazipigania na wanazililia ili kujua haki zao ziko wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo elimu ya juu na ufundi ni elimu ambayo inaendeshwa na chombo cha Muungano. Nenda *University of Dar es Salaam.* Wanakuja wanafunzi wetu kutoka Zanzibar kufanyiwa usaili kati ya 20 kwa mwaka wanachukuliwa watoto watatu au wanne tena wa *division one* wanarudishwa Visiwani, kwa nini? Mnataka kweli kuisaidia Zanzibar kuinua hali yake ya elimu? Tupeni nafasi maalum katika masomo ya juu kwa vile hasa Zanzibar viwango vya elimu viko duni kidogo na kulikuwa na mpango kabambe huko nyuma kwamba viwango vya Zanzibar vilishushwa ili wanafunzi wa Zanzibar wapate nafasi kuingia katika Vyuo Vikuu. Hilo lifanyike mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo hii Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin Mkapa, kamaliza miaka yake kumi, nilikuwa naangalia kila mwisho wa mwezi anapotoa hotuba, hata mara moja hakugusia maendeleo ya Zanzibar, *why?* Yeye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano. Mheshimiwa Jakaya Kikwete katoa ahadi kwamba ataendeleza hotuba zile kila mwisho wa mwezi, tunamwomba na yeye agusie matatizo na uchumi wa Zanzibar kama alivyotoa ahadi ili Zanzibar ifaidike na Rais wake wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni jambo la aibu kumwona Rais wa Jamhuri ya Muungano kakaa miaka kumi, Waziri Mkuu kakaa miaka kumi mara ngapi ametembelea Zanzibar, mara ngapi walikuja wakakaa na Wazanzibari wakaona matatizo yetu. Mheshimiwa Jakaya Kikwete asimalize Kariakoo peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aje na Zanzibar, aende Pemba, tumpeleke vijijini aone kwamba ni sehemu, *is a part and parcel* ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba tena sana kwamba hili suala la kwamba sisi ni chama cha kigaidi na ambacho hakitaki maendeleo, liondoke katika vichwa vyetu na sasa hivi tujenge misingi imara ya kujitetea Zanzibar kiuchumi ili Zanzibar nayo ifaidike kama mnavyofaidika ninyi Tanzania Bara. Tunaona wivu, tunaona uchungu kuona nchi yenu inajengwa. Kuna watu wanawekeza hapa vitega uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna majumba yanajengwa makubwa makubwa, kuna barabara nzuri, lakini unapoenda Zanzibar maendeleo yoyote hayaonekani kwa sababu Serikali ya Muungano haijihusishi kikamilifu katika kusimamia maendeleo ya upande mmoja wa Zanzibar nayo ni sehemu ya Muungano ya visiwa vya Unguja na Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *we must be fair, otherwise crisis* hazitaondoka, itakuwa kama India na Pakistan, *crisis* za Kashimir.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kukutana hapa kujadili hotuba ya

Mheshimiwa Rais ambayo ninaamini michango yetu itaweza kumsaidia sana Mheshimiwa Rais.

Pili, nakushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Spika wetu kwa kutuongoza vizuri kwenye Bunge hili. Namshukuru vile vile Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi yake kubwa ya usiku na mchana kuhakikisha kwamba Mtanzania hafi kwa njaa. Wengine, nawashukuru sana wapiga kura wa Jimbo la Chambani ambao walinihakikishia na baadaye kunichagua kwa wingi wa kura hata wale wanachama wa CCM. Kwa kweli walinipa kura nyingi mno ambazo mpinzani wangu alipata kiwewe.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu, nasema kwamba mimi nilipata nafasi ya kujadili hotuba hii ya Mheshimiwa Rais na baadhi ya wapiga kura wangu na haya nitakayoyazungumza ni pamoja na maoni yao, si yangu peke yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza kwa dhati sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa hotuba yake nzuri ambayo imejenga matumaini mapya kwa Watanzania wote ikiwa vitendo na maneno ya hotuba hii vitakwenda sambamba. Juzi Mheshimiwa Wilson Masilingi, alipokuwa anachangia alisema kwamba wapinzani wanapoipongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais, maana yake wanaipongeza sera ya CCM. Nataka kutoa siri moja hapa ambayo Wabunge wenzangu wa CCM hawaijui, ni kwamba hii hotuba ya Mheshimiwa Rais imebeba sera nyingi sana za chama cha *CUF* na ndiyo maana wana-*CUF* na wapinzani wengi hotuba hii wanaipenda sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimegundua kwamba baada ya mchango wa Mheshimiwa Ali Said, jana na Mheshimiwa Khalifa Suleima Khalifa na leo itakuwa mchango wa Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, kwamba Waheshimiwa Wabunge wa upande huu wa Muungano, Tanzania Bara wameanza kufahamu nini tatizo la Zanzibar. Kwa maana hiyo basi, naomba hili nalo nilikazie ili katika mambo yangu matano ambayo nitaenda kuchangia kama muda upo, na hili nilikazie ili wazidi kufahamu tatizo la Zanzibar liko wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amezipongeza Taasisi mbali mbali ambazo zimesadia katika mchakato mzima wa uchaguzi wa Tanzania. Mimi nasema hiyo ilikuwa ni haki yake kuzipongeza hizo Taasisi mbalimbali ambazo zimesaidia katika uchaguzi na hatimaye kumweka yeye madarakani na Wabunge wa CCM. Lakini nataka kutumia nafasi hii vile vile kutoa maelezo kidogo kuhusu michango hiyo.

Mheshimiwa Rais amepongeza sana vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Tanzania kwa kazi yao nzuri. Nasema huo ni wajibu wake, ni haki yake kufanya hivyo. Lakini niseme tu kwamba kwa bahati mbaya sana kwa upande wa Tanzania Visiwani vimekuwa ni wavunjifu wakubwa wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya Ulinzi na Usalama vimemuua kijana kwa bunduki hapo hapo wakati wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura kule mkoani Pemba.

Vile vile wamempiga risasi na kumuua kijana hapo hapo baada ya uchaguzi na baada ya matokeo kule Wete, Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo hivi vya usalama vimewapiga watu sana Unguja na Pemba, vimevunja majumba ya watu, vimechukua mali za watu, vimenyanyasa watu, vimenajisi watu wakati mwingine mke mbele ya mumewe au watoto wakubwa mbele ya wazee wao. Ni mambo ya kusikitisha kweli. Halafu, la zaidi ni kwamba hakuna hatua zozote za kisheria ambazo zimechukuliwa kwa hao waliohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi za haki za binadamu wanasema hawawezi kufanya kazi Zanzibar. Sasa Wazanzibari waende wapi? Walie kwa nani? Wao ni binadamu kama sisi. Tofauti yao ni kwamba wana itikadi tofauti tu ya chama, lakini ni binadamu kama sisi na wanahitaji vile vile haki za binadamu ziwe upande wao. Kwa hiyo, hili ni masikitiko makubwa kwa upande wetu kwamba vyombo hivi ingawa vinasifiwa, lakini kwa upande mmoja vimesababisha maafa makubwa kama alivyoeleza jana Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, hapa kwa upande wa Piki na sehemu zingine, maana hata na Wabunge wako Mheshimiwa Naibu Spika, wamepigwa vibaya sana kule Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, Mheshimiwa Rais alipongeza vile vile vyombo vya habari. Lakini, nasema ni haki yake. Lakini nasema vyombo vya habari vimelalamikiwa sana na Watanzania walipa kodi na wanasiasa na viongozi wa siasa kwamba vimekuwa na upendeleo wa wazi kwa Chama Tawala cha CCM na hasa vile vyombo vya Serikali, nasema kwamba havikuwatendea haki Watanzania wale ambao walikuwa na mawazo tofauti na wao. Kwa hiyo, hili ndiyo swali kubwa kwa vyombo vya habari kwa sababu ni vyombo ambavyo vinatakiwa vifanye kazi kwa uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imefikia mahali kule Zanzibar huwezi hata kufungua *TVZ* au redio kwa sababu kinachoonyeshwa wakati wa uchaguzi ilikuwa ni CCM tupu, kidumu, kidumu basi na pale kuna vyama vingine vingi, kuna CHADEMA, *CUF* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais vile vile kapongeza Tume za Uchaguzi, hapa ndiyo kwenye tatizo. Tume za Uchaguzi zimekuwa ndiyo tatizo la msingi la Zanzibar, kwamba wao wamejifanya ma-*referee. Referee* ni mtu wa mwisho, nachukua mfano wa timu za mpira wa miguu, *referee* anaposema hilo ni goli, basi ni goli. Sisi *CUF* tumejiandaa vizuri kama timu, tumeingia uwanjani katika mchezo, tumejipanga vizuri na tulikuwa na uhakika kwamba tunashinda uchaguzi. Lakini kwa sababu yeye *referee* wetu ndiyo mwamuzi wa mwisho, alivyofanya, ndiyo hivyo alivyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niingie moja kwa moja sasa katika mpasuko wa kisiasa. Kwanza nampa pole sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa hili. Lakini wakati huo huo nampongeza sana kwa sababu ni kiongozi wa kwanza aliyezungumza hadharani kwamba kuna mpasuko wa kisiasa Zanzibar. Kwa hili nampongeza kwa *challenge* yake. Nataka kusema kwamba mpasuko huu uko kati ya Zanzibar na Pemba, si kati ya Pemba na sehemu zingine za Tanzania. Mpasuko huu umeandaliwa makusudi na viongozi ambao wamo kwenye madaraka tokea 1995.

Baada ya uchaguzi wa mwaka 1995, viongozi ambao wamo kwenye madaraka kwa kuona hali halisi ya kisiasa kwamba *CUF* imechukua majimbo yote Pemba, imechukua Majimbo mawili Zanzibar na Rais wetu alikuwa ameshinda uchaguzi, hali ndiyo ikaanza kuharibika. *CUF* wakaanza kutengwa kisiasa, wakaanza kutengwa kiuchumi, wakaanza kutengwa kwenye huduma za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokea wakati huo, Wapemba waliokuwa na madaraka, wote walishushwa vyeo na wale ambao hawakuwa na vyeo lakini walikuwa na kazi Serikalini, basi walipata uhamisho katika sehemu ambazo zingewa-*frustrate.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo ya kisiasa tunasema hakuna uwiano, viongozi wengi kule Zanzibar, kwa mfano, Spika, Naibu Spika, Mkuu wa Jeshi la Polisi, Jaji Mkuu, Kamishna wa Polisi, Uhamiaji, Mkuu wa Magereza, Mkuu wa KMKM, Mkuu wa JKU, Mkuu wa KVZ, wote hao wanatoka Zanzibar kwa maana ya Unguja. Sasa utashangaa hapa kwamba kweli Serikali hii inafanya haki kwa Wazanzibari? Uwiano uko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, uwiano wa kiuchumi, zao la Karafuu ambalo ni zao kubwa kule Pemba linateremshwa bei kila wakati, wakati mwingine ni wakati wa msimu ambao wakulima wameanza kukodi, basi ghafla bei inakuwa chini, unakuta wanapata hasara. Barabara zote Pemba ni mbovu, zote ni mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hii ndiyo hali ya kiuchumi. Kwa hiyo, nilichotaka kusema hapa ni kwamba uwiano huu umekuwa mbaya kwa sababu nia ya Serikali ya Mapinduzi siyo nzuri na watu wanaposema hawaitambui Serikali maana yake ni kwamba haina mambo mazuri ambayo inawafanyia watu. Kwa hiyo, watu kwa kweli wanakuwa *reluctant* kukubali uongozi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda wangu uliobakia ni mdogo, nataka nizungumze kidogo kuhusu kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kupata nafasi ya kuchangia katika hoja hii ya hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa tarehe 30 Desemba, 2005 wakati anazindua Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kishapu, kwa kunipa kura nzuri za kupendeza na kuniwezesha kufika katika Bunge hili niweze kuwawakilisha katika miaka mitano inayokuja. Nawashukuru sana na mimi napenda kuahidi kwamba nitawatumikia na nitafuatilia kwa makini utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ambayo inalenga katika Jimbo la Kishapu. Naomba niwapongeze pia, Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri na Wabunge kwa ushindi mzuri walioupata katika uchaguzi wa tarehe 14 Desemba, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais, imetoa dira nzuri na imewapa matumaini Watanzania wote. Nami nitachangia maeneo machache kwa kuzingatia muda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nizungumzie suala la njaa inayolikabili Jimbo la Kishapu. Jimbo la Kishapu ni moja ya maeneo ambayo yamepatwa na ukame mkubwa mwaka huu. Kuna maeneo katika Jimbo la Kishapu hayajapata mvua kwa muda wa miaka miwili, mitatu mfululizo na kuna sehemu ambazo zimepata mvua kidogo sana. Kwa hiyo, kuna ukame mkubwa na kuna upungufu mkubwa wa chakula.

Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuweza kutembelea Jimbo la Kishapu na wananchi walishukuru sana na nashukuru Mawaziri walioambatana na Mheshimiwa Waziri Mkuu wameweza kujionea wenyewe hali halisi ya Jimbo hili. Suala la ukame, mifugo mingi inakufa, watoto wa shule hawawezi kwenda shule kutokana na ukosefu wa chakula. Naishukuru Serikali kwa kuamua kutoa chakula kwa Jimbo la Kishapu. Ninachopenda na ninachoomba kusisitiza, naomba hicho chakula kiende mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeletewa taarifa wananchi 25 wa kijiji cha Mani, Jumapili waliweza kuzilai kwa kukosa chakula. Lakini wamesaidiwa na Kanisa. Wakapewa magunia mawili, wakapata chakula. Kwa hiyo, naiomba Serikali ipeleke chakula kwa utaratibu wa dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie sekta ya maji. Ni ukweli usiopingika kwamba maji ni muhimu kwa ajili ya maendeleo na nchi zote duniani ambazo zimepata maendeleo ni nchi ambazo zina maji mengi, lakini pia zimechua hatua za makusudi za kuwekeza katika sekta ya maji na zimepata maendeleo makubwa. Nchi za Bara la Afrika, Tanzania ikiwemo zina maji, lakini hazijawekeza vya kutosha katika sekta ya maji.

Kwa hiyo, maendeleo siyo ya kasi sana. Sera ya maji ya mwaka 2002 ya Tanzania imebainisha kwamba ifikapo mwaka 2025, Tanzania tutakuwa na upungufu wa maji. Kwa sasa, kila Mtanzania anaweza akapewa maji au akatumia maji mpaka kufikia mita za ujazo 2,700 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango hiki kinaashiria kwamba tunayo maji ya kutosha. Lakini hatujawekeza vya kutosha. Ifikapo mwaka 2025, kiwango hiki kitapungua mpaka kufika 1,700 kwa kila Mtanzania. Inaashiria kwamba tutakuwa na upungufu mkubwa wa maji. Kwa hiyo, Serikali yetu inahitajika ichukue hatua madhubuti na za kidharura ili tusiweze kukumbwa na tatizo kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu na hasa Mheshimiwa Edward Lowassa ambaye kwa sasa ni Waziri Mkuu. Aliweza kuchukua hatua mbalimbali na kuboresha sekta ya maji au kutatua matatizo mengi katika sekta ya maji. Ameweza kwa usimamizi wake kuanzisha bodi za maji ambazo zilikuwa zimebakia saba na matatizo mengi ameyatatua. Lakini tunahitajika kwenda zaidi ya hapo na

ninaunga mkono makusudio ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kuweza kulipa kipaumbele suala la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupendekeza mambo yafuatayo ili kweli tuweze kufanikiwa katika kuleta mafanikio katika hii sekta ya maji na kuweza kuyafikia makusudio ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:-

Naishauri Serikali ikamilishe utaratibu wa kuanzisha Mfuko wa maji Kitaifa. Katika Mabunge yaliyopita, Wabunge walikubali kuanzishwa kwa mfuko wa maji Kitaifa kwa sababu za kimsingi zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kukabiliana na matatizo katika sekta ya maji, Tanzania inakadiriwa inahitaji kupata dola bilioni moja ili kuweza kuwekeza katika sekta ya maji. Kati ya hizo, dola milioni 38 ni kwa ajili ya kusimamia rasilimali za maji nchini. Fedha hizo haziwezi kupatikana katika Bajeti ya nchi. Kwa hiyo, tunatakiwa kuanzisha Mfuko wa maji. Kwa hiyo, Serikali iharakishe utaratibu huo ili Mfuko wa Maji uweze kuanzishwa ili tuweze kupiga kasi kubwa katika sekta ya maji. Tuna Mfuko wa Afya, Mfuko wa Elimu na Mfuko wa Barabara na hiyo Mifuko imeweza kuleta mafanikio. Naamini kuanzishwa kwa Mfuko wa Maji kutatuongezea kasi katika kutatua matatizo katika sekta ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende tena katika suala la ukame. Kutokana na kubadilika kwa hali ya hewa ambayo inatokana na kuongezeka kwa joto duniani, inawezekana ukame ukaendelea kwa muda mrefu. Serikali katika Awamu ya Tatu ilikuwa imetoa mpango wa kuweza kuzingatia maeneo ya ukame yachimbiwe mabwawa, malambo, ili angalau mvua inaponyesha hata kwa muda mchache, maji yanayopatikana yaweze kuvunwa na yaweze kusaidia wananchi katika kilimo na kwa mifugo wanayofuga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali iendelee kuzingatia suala la kuchimba mabwawa na malambo katika maeneo kame na Wilaya ya Kishapu au Jimbo la Kishapu lipewe umuhimu wa kipekee kutokana na ukame mkubwa ambao umelipata eneo hilo. Kishapu kweli ni kame sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika hoja hii ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali naomba nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa wanawake wa Mkoa wa Kagera, Umoja wa Wanawake Tanzania na Chama cha Mapinduzi kwa kunipa tena nafasi katika Bunge hili kwa kipindi cha tatu, nawashukuru sana.

Pili, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi mkubwa alioupata na hivyo akaweza kuunda Serikali, Serikali ya watu makini. Mheshimiwa Edward Lowassa wote tunamwelewa, ni mtu makini sana na Mawaziri wote wamekwishatuonyesha kwamba kweli watachapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Spika na wewe pia katika nafasi hizi ambazo tuliwachagua sisi wenyewe na kazi yenu ni nzuri, tunaiona. Mwisho, niwapongeze Wabunge wenzangu wote katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais imepokelewa vizuri sana na wananchi. Imewapa matumaini makubwa na matarajio yao ni makubwa kabisa kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano, basi mambo mbalimbali, matatizo na kero mbalimbali zitaweza kutatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, hotuba hii ni changamoto kwa kila Mtanzania mahali alipo kila mtu afanye kazi kwa bidii ili kwamba kwa kusaidiana na nguvu za Serikali basi tuweze kutatua matatizo kama wananchi, lakini pia kwa kila mmoja, mmoja. Tusitarajie miujiza kama watu hawatafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 15 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais, amezungumzia kwa kirefu kidogo kwamba Serikali itajali maslahi ya makundi maalum ambayo ni wanawake, vijana, watoto, walemavu, yatima, lakini pia wazee. Naomba nizungumzie zaidi kundi la wazee maana na mimi niko miongoni mwao lakini pia wote tunaelekea huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameeleza kwamba atawajali na akaeleza kwamba hivi sasa wazee hawatakiwi kutozwa kodi ya nyumba katika nyumba wanazoishi Mijini, nadhani ni ile wanayoita *property tax.* Lakini sina hakika kama kuna maelekezo kwa watoza kodi ili kodi hii isitozwe. Mimi ninavyoona watu hawa wanatozwa kodi katika nyumba hizo.

Kwa hiyo, mimi nadhani kwamba Serikali itoe maelekezo hayo ili hili liweze kuzingatiwa. Lakini pia akaeleza kwamba wazee wanapata huduma za matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina wasi wasi na nina mashaka kabisa katika baadhi ya maeneo nimekwishapata malalamiko. Wazee hawa kwanza wakienda na kwa sababu wamekwisha, ni wazee, hakuna mtu anaye wajali wazee hawa wananyanyasika kabisa.

Lakini pia ukizingatia kwamba hata katika hospitali unakuta kwamba baadhi ya dawa hazipatikani, zinapaswa kununuliwa katika *pharmacy* ambayo unapaswa kwenda kununua kwa fedha. Sasa baadhi ya wazee kwa kweli hawana uwezo wa kuweza kununua hizi dawa.

Kwa hiyo, mimi naomba kwa sababu Rais amesema atawajali basi kwa kuwajali, uwepo utaratibu maalum wa kuwahudumia hawa wazee. Kama kutakuwepo na fungu la kuweza kuwapatia kuhakikisha kwamba wanapata dawa hizi ambayo ni haki imekwishatolewa, basi fungu hilo lijulikane na katika hospitali ijulikane ni mganga gani anahudumia hawa wazee. Siyo mzee anafika ananyanyasika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi huwa naumia sana, kwa sababu wazee hawa ndiyo waliotufikisha sisi hapa tulipo. Kwa hiyo, mimi ninaomba wapewe kipaumbele, wapewe nafasi nzuri ya kutibiwa na liwepo fungu la kuhakikisha kwamba wazee hawa wanapewa, wanapata matibabu wanayostahili, ikizingatiwa pia kwamba katika umri wa uzee basi yanajitokeza maradhi mbali mbali.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie wastaafu. Tulilalamika sana hapa sisi Wabunge siku za nyuma na Serikali ikakubali kuwarudisha katika malipo wale wazee waliokuwa wamelipwa mkupuo. Lakini walio wengi malipo yao yalikuwa kidogo sana kwa hiyo utakuta kwamba malipo kiwango cha chini ni shilingi elfu 20,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niambie kwa 20,000/= mtu anafanya nini. Wengine walikuwa na vyeo vikubwa. Mwingine ni Katibu Mkuu wa Wizara lakini sasa hivi anapata pensheni ya shilingi 20,000/=.

Sasa nilikuwa najiuliza kwa nini  Serikali haikuwajali kama Rais alivyosema, hawa wastaafu warekebishiwe hizi pensheni, angalau zilingane na watu wa vyeo ambavyo walikuwa wamevishika wale wazee wakati wakiwa kazini kabla ya kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kwamba wazee vijijini huko hasa akinamama ambao wamepika sana kwenye majiko ya moshi. Akishakuwa na umri kama wangu anaambiwa ni mchawi kwa sababu macho yake ni mekundu. Wanauwawa bila huruma! Sijui Serikali haioni!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashangaa sana! Hivi mtu anaweza akauwawa hapa, nyumba ya jirani wasijue! Kwa nini jirani wasibanwe wakasema nani amewaua wale watu. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nadhani kwamba suala hili wamelizembea. Sijui lilianzia ni Shinyanga, sijui ni wapi. Sasa limeenea karibu Mikoa yote wazee wanauwawa bila huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninaomba suala la wazee vikongwe kuuwawa liangaliwe na lidhibitiwe. Watu wasiuwawe hivi hivi, sasa hiyo haki ya binadamu, haki ya kuishi iko wapi? Kwa hiyo, ni Serikali basi inabeba lawama hiyo ya watu kuuwawa bila sababu, wala bila huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda umekwisha, ninaomba na nikushukuru tena na niunge mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kipindi chetu cha asubuhi kimekwisha, tutakaporudi naomba wafuatao wawe wamejiandaa,  Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes na Mheshimiwa  Castor Raphael Ligallama.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha kikao mpaka saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jioni hii ataanza Mheshimiwa Paul Kimiti, atafuatiwa na Juma Killimbah na Mheshimiwa Yono Stanley Kevela. Kama Mheshimiwa Kimiti hayupo basi namwita Juma Killimbah na Mheshimiwa Blandes ajiandae.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nashukuru kwa Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii muhimu na hasa kwa kunijalia afya njema kufika hadi siku ya leo na kuweza kuchangia mjadala huu muhimu sana wa Hotuba ya Rais aliyoitoa tarehe 30/12/2005 wakati akizindua Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii nikupongeze wewe mwenyewe binafsi hasa kwa kuchaguliwa na Wabunge kwa kura nyingi kushika nafasi hiyo. Pili, nimpongeze Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yeye pia kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Spika wa Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kura alizozizoa, kura nyingi, kura za kishindo. Pia, nimpongeze Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa. Pia niwapongezeni sana Waheshimiwa Wabunge wa majimbo yote mlioshinda, wale wa Viti Maalum na wale walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika wadhifa wa Ubunge. Vile vile, niwapongeze Mawaziri na Manaibu Waziri wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa shukrani zangu, labda niingie kwenye mjadala wenyewe na ninaamini mjadala umeishaongelewa kwa vipengele mbalimbali na michango imetolewa sana na Waheshimiwa Wabunge, lakini nami nitakuwa na mchango kwa kadri ninavyoweza kuchangia na hasa nitaanza kama alivyozungumzia Mheshimiwa Rais katika hotuba yake, nikianzia na kipengele cha hali ya kisiasa ndani ya nchi yetu. Ni dhahiri ninakipongeza Chama changu cha Mapinduzi (CCM) na hasa viongozi wake wakuu kwa utaratibu mzuri waliouweka na kutuwezesha sisi wagombea wote kufanya vizuri sana. Ninaamini kwamba utaratibu mzuri uliopo ndani ya Chama cha Mapinduzi, sera nzuri na Ilani nzuri ndizo zilizowavutia wananchi na wakaweza kutuchagua kwa asilimia kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inashangaza pale watu wanapobeza ushindi wa CCM, wanavyosema ya kwamba eti hatukushinda kwa kishindo, kwamba ushindi ulikuwa ni wa kuiba! Matokeo yalishazungumziwa tangu awali na hata watafiti waliwahi kufanya utafiti walizungumza. Lakini pengine wenzetu hawazingatii ya watafiti pamoja na wasomi. Walikuwepo watafiti kama wa *REDET* na Chuo Kikuu, walizungumzia tangu mwaka 2003 na 2004 na wakasema CCM itashinda kwa ushindi mkubwa na ndicho kilichotokea mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea na hali ya kisiasa, ni kweli kabisa kwa mazingira mazuri na uendeshaji mzuri wa Serikali uliopo ndani ya CCM, kwa kutumia kigezo cha vyama vingi watu wameweza kujichukulia sheria ambazo pengine wanajificha kwenye vyama na wanaamua kufanya matendo makubwa zaidi ambayo yanaleta uvunjifu wa amani kama yale yaliyotokea. Tunafahamu kilichotokea baada ya uchaguzi kuahirishwa na ilipotokea kufariki kwa Mgombea Mwenza wa CHADEMA. Tulijionea vurugu zilivyoandaliwa kule Zanzibar, lakini tunashukuru Mungu na ninalipongeza sana Jeshi la Polisi kwa kusimama imara kule Zanzibar na hata kudhibiti vurugu pale eneo la darajani. Ilikuwa hakuna sababu za kuogopa, sababu ni halali kwamba Polisi walikuwa wanalinda usalama wa raia.

Nachukua nafasi hii pia kuelezea hali hii ya kisiasa. Nilaani hizi tabia ambazo zinaendeshwa na baadhi ya vyama kwa kuwapiga watu wasio na hatia na pengine wakiwemo waandishi wa habari eti kwa kisingizio kwamba wametumwa na CCM. Kwa kweli tabia hii ninailaani kwa nguvu zote na ninaomba katika hii Serikali ya Awamu ya Nne tabia hii ikomeshwe kabisa na ikiwezekana vyama vinavyodhihirika kuwa na tabia hiyo vidhibitiwe na ikiwezekana ile sheria namba 5 ya mwaka 1992 itekelezwe ipasavyo na Msajili wa Vyama asione aibu kuviondoa katika daftari lake hasa vyama vinavyokiuka maadili ya vyama vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la janga la njaa linalokabili nchi nzima au taifa zima kwa ujumla. Ukweli kabisa njaa inatisha! Ndiyo maana kila Mbunge aliyesimama ameongelea sana, sana, sana, tatizo hili la njaa. Lakini nashukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ninawashukuru viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi kwamba kwa kiwango kikubwa wameonyesha juhudi za dhahiri na kwamba wameonyesha wanawajali wananchi kwa hali na mali. Hili ni jambo la kupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri ambayo naamini viongozi wa juu wameifanya, jana wakati Mheshimiwa Rais anahutubia wananchi wa mkoa wa Dodoma ametueleza wazi wazi akasema kwamba, chakula kipo na takwimu ziliishakamilika na mgao tayari uliishagawanywa. Ni kweli na sisi nakala tunazo hapa Waheshimiwa Wabunge wote na akasema huu ni uzembe wa Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kwa nini hawa watu wanataka kutujengea wigo wa kupewa lawama sisi Waheshimiwa Wabunge? Sisi Waheshimiwa Wabunge ndiyo tunaolaumiwa na tunaambiwa kwamba hatufuatilii! Kumbe tayari taratibu zote za chakula kupelekwa kwa wananchi zimeshakamilika. Kwa hiyo, kwa sababu Wakuu wa Mikoa wameapishwa leo hii, ninaamini kwamba hawa tutakaoanza nao naomba hala hala wapeleke chakula mikoani na hasa katika Jimbo langu la Uchaguzi la Iramba Magharibi waharakishe ili chakula kiweze kwenda kuokoa hali ya wananchi waliopo kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nigusie suala la Utawala Bora. Ni kweli kabisa dhana ya utawala bora ni dhana muhimu sana na hii dhana ina mihimili mikuu mitatu, uwajibikaji, ushirikishwaji na uwazi. Lakini ni bayana kwamba tumekuwa hatuna hili

suala la uwazi, tunasikitika sana hasa juu ya uendeshaji wa shughuli zinavyoendeshwa katika Halmashauri zetu za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano nikielezea Halmashauri ya Wilaya kwenda kuwaondoa Madiwani kwenye vikao vya *tender board*, kwa kweli ni jambo ambalo linaonyesha kwamba tunawanyima haki wapigakura na kodi zao zinashindwa kusimamiwa ipasavyo. Tukiwaachia Wakuu wa Idara wakawa ndiyo wajumbe peke yao, wao ndiyo watekelezaji, matokeo yake yamejionyesha na ninaweza nikatokea mfano katika Jimbo langu la Iramba Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya miradi ambayo imetekelezwa si madhubuti kutokana na kwamba ilikosa usimamizi mzuri na pengine Madiwani hawaelewi hata wale wazabuni waliochukuliwa na kuweza kutekeleza hiyo miradi. Ningeomba sana hili suala la kuwaweka pembeni Waheshimiwa Madiwani wasiwe washiriki katika Vikao vya Bodi ya Zabuni za Halmashauri zao, Serikali ya Awamu ya Nne iliangalie kwa makini kwa sababu linawaondolea wapigakura wasimamizi wa kodi zao katika Halmashauri zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kuzungumzia suala la Usalama wa Raia na hasa hili wimbi la ujambazi uliojitokeza. Nitazungumzia katika mtazamo wa peke yake. Wazungumzaji waliozungumza wamezungumzia sana namna ya kwamba Polisi wamekosa vifaa, wamekosa vitendea kazi na pengine wameshindwa kufanya kazi kwa umakini kutokana na kukosa hivyo vifaa kama silaha na kadhalika. Lakini hali halisi inavyoonyesha ni kwamba pamoja na hayo, inaonyesha dhahiri …

*(Hapa Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji Kumalizika)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuongea ndani ya Bunge lako Tukufu. Vile vile, nichukue nafasi ya kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Pia, nichukue nafasi hii unipelekee pongezi zangu kwa Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Njombe Magharibi kwa kunichagua mimi Yono niwe mwakilishi wa Jimbo lao hasa kwenye hizi tarafa za Mdandu, Imalinyi na Wanging'ombe. Kwa kweli nawapongeza sana na ninawashukuru sana. Mpaka wanakubali mabadiliko, siyo kazi ndogo! Mimi ni mara yangu ya kwanza kugombea na ni kijana wao. Kwa kweli walifanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walichokifanya ilikuwa siyo kazi ndogo, asilimia tulizopata ni nyingi sana. Kitaifa nilikuwa mshindi wa tatu. Tulipata asilimia 96.5, ni kama asilimia 100 tu. Kwa hiyo, nawashukuru sana na Mungu awabariki. Vile vile,

namshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu siyo kitu rahisi mpaka siku ya leo niwe na afya nzuri, ninamshukuru sana kwa kunijaalia na kunifanya niingie kwenye Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi nyingi sana ziende kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Natoa pongezi kwake kwani wananchi wangu walimpa kura nyingi zisizo na kifani. Nimpongeze pia Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, niwapongeze Mawaziri na Manaibu wao bila kusahau Makatibu wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Wabunge wote na Wenyeviti wa Kamati ambao wamechaguliwa hivi karibuni. Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipompongeza Mwenyekiti wangu wa Wizara ya Mambo ya Nje, Mheshimiwa Anna Abdallah. Sisi Mwenyekiti wetu tumemchagua mwanamke, tunafurahi sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za mwisho niwape viongozi wa Chama na Serikali ambao waliniwezesha mpaka siku ya leo kuwa Mbunge. Nawashukuru na ninawapongeza sana kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba Jimbo la Njombe Magharibi ni kubwa sana katika wilaya ya Njombe. Tuko katika majimbo matatu, yaani kuna Jimbo la Kusini, Kaskazini na Magharibi. Jimbo langu limekuwa ni kubwa sana, lakini bahati mbaya huduma zile za muhimu zimekuwa hafifu sana. Yaani tuseme kama limechelewa. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kusema kwamba tuna matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba nachangia hii hotuba, lakini tuna matatizo makubwa sana hasa katika upande wa mbolea. Mbolea inakuja ya ruzuku, lakini ina tatizo kubwa la usambazaji na wakati fulani kuna ubadhilifu na wizi, wakati fulani inapelekwa mpaka nchi nyingine za jirani kiasi kwamba inanisononesha sana. Bahati nzuri nilipomueleza Waziri Mkuu amechukua hatua, nimesikia baadhi ya tarafa zangu zimeishapata mbolea, kwa sababu zilikuwa hazifiki kwa walengwa. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni tatizo la barabara. Kwa kweli kwa suala la barabara kule kumesahaulika kabisa, barabara zina mashimo. Ukitaka kupata raha sana ya zile barabara ni wakati wa mvua, hazipitiki kabisa. Tunategemea kipindi hiki Serikali ya Awamu ya Nne itaangalia, hasa huyu Waziri wa Miundombinu ataangalia kwa jirani hasa barabara na madaraja. Kuna daraja kama hili la Usuka, yaani wakati wowote nafikiria lolote linaweza likatokea, daraja ni bovu kabisa na magari yanapita pamoja na abiria. Nimejaribu kuongea sana na Mkurugenzi wa pale Njombe, lakini naona hajachukulia uzito unaostahili. Tuna hofu kwamba lolote linaweza likatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tuna tatizo la maji. Kule kwetu Njombe kuna sehemu ambazo zina chemchem kama Mwiramba. Yale maji yapo mengi sana pale na ni salama. Bahati nzuri kuna wafadhili, kuna Taasisi za Kidini, huyu *Father Kamilo* ameanza kusaidia sana kusambaza maji sehemu za Igosi, Kipengere na maeneo ya jirani.

Kwa hiyo, tunaomba Serikali ijitahidi kuungana na wale wafadhili pamoja na nguvu za wananchi kuhakikisha kwamba yale maji yanasambaa sehemu zote kwa sababu sehemu zingine ndiyo tuna tatizo kubwa sana la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tarafa za Wanging'ombe, kuna vijiji vya Lyamluki na Lyadebwe, watu wanapanga foleni ndefu kuchota maji kwenye kisima ambacho hakitoi maji. Nilienda pale kwa kweli nilisikitika sana. Waziri wa Maji nilimuandikia atusaidie tuchimbe visima vile vya ku-*drill,* vile virefu kabisa ili tuondokane na hilo tatizo kwenye hizo tarafa za Wanging'ombe na Saja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu elimu. Kweli Serikali inajitahidi sana, ina juhudi nzuri sana za kuhakikisha kwamba elimu inakuwa ni nzuri, ni bora, lakini kwenye Jimbo langu kuna tatizo kubwa la ajira, kwamba ile elimu iendane na vyuo. Kwa mfano, tunakazana kujenga shule za msingi, shule hizo ziko nyingi sana, lakini ukiangalia shule za ufundi hakuna! Sekondari ziko karibu 14. Kulikuwa na shule ya ufundi Ulembwe, ni matatizo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kwamba kwa sababu kuna majengo ambayo yako wazi, kazi ni kupeleka mitambo tu, tushirikiane na wananchi kwani nguvu zao waliishatoa, tujenge vyuo vya ufundi mbalimbali ili kupunguza tatizo la ajira kwa sababu siyo siri Mkoa wa Iringa unasifika kwa kutoa dada zetu ambao wanakuja kufanya kazi ambazo siyo nzuri. Kwa hiyo, Serikali ichukue nafasi hii kuweka shule za ufundi nyingi ili angalau vijana ambao ni akina dada wetu wapate ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia ni kuhusu mikopo. Kwenye Jimbo langu suala hilo lilikuwa ni hadithi. Mikopo mingi ilikuwa inaishia kwenye sehemu ambazo ni nje ya Jimbo langu tu. Kwa hiyo, kwa kipindi hiki tunategemea kutatokea mabadiliko makubwa hasa katika Wizara ya Ushirika na Masoko. Tunategemea kwamba mtatuangalia tofauti kwa sababu muda mwingi tulikuwa tumesahaulika hasa katika maeneo ya Ilembula na Igosi. Tarafa hizi tatu za Wanging'ombe, Mdandu na Imalinyi kwa kweli tulikuwa tunasahaulika sana. Akina mama walikuwa wanapata shida sana, wanasikia kwamba wenzao wa Makambako wamepata mikopo, wenzao wa Njombe Mjini wamepata mikopo, lakini wao na vijana kule walikuwa hawapati kabisa na hatuelewi tatizo lilikuwa ni lipi, labda lilikuwa ni la kisiasa au nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kipindi hiki nafikiria kwa sababu wanapenda Chama cha Mapinduzi huenda Wizara yetu itajitahidi sana kuhakikisha kwamba *SCULT* na Vyombo vya Fedha vinapeleka pale mikopo pale kwa sababu tunapata shida sana. Wakati fulani tunakuwa wepesi kwenda Mbeya kwa sababu tuko mpakani mwa Mbeya. Wananchi wanaenda kulima hata mpaka Lujewa. Hali si nzuri sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mambo yako mengi na muda naona unataka kuniishia, nieleze haraka haraka kuhusu suala lingine. Nataka nitoe mapendekezo tu kwamba, kuna kijiji cha jadi ambacho hapa Tanzania ni kijiji pekee,

sijaona kijiji cha jadi cha asili kingine. Kijiji hicho kipo Mlevela kinaitwa Nyumbanitu. Pale kwa suala la utalii kama tungepatumia vizuri pangeweza kutuendeleza vizuri sana na nchi yetu ingepata fedha sana. Sawa huwa wanakuja wanafunzi kutoka Chuo cha Sokoine pale wanajifunza, kuna mimea ya ajabu iko pale, kuna kuku wa ajabu wako pale, tukipatumia vizuri huenda nchi yetu ingekuwa na mapato makubwa ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiria kwamba kama kutakuwa kuna uwezekano tufanye jitihada ya makusudi kile kijiji cha Mlevela, kijiji cha Nyumbanitu kiendelezwe na yale mapango yaendelezwe. Vile vile, kuna ile *Mpanga Game Reserve,* wananchi wangu wanalalamika kule kwamba wamehamishwa, lakini wamepunjwa sana malipo. Kwa hiyo, Wizara ya Maliasili nadhani itachukulia umuhimu wa kipekee kuhakikisha kwamba wananchi wale wanalipwa vizuri na wale ambao hawajalipwa wanaishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili suala la nishati nalo ni tatizo kidogo. Kule kuna shule nyingi lakini hazina umeme, shule moja ndiyo ina umeme. Vijana wetu wanateseka sana. Pale Kidugula wanateseka sana kwa sababu umeme haupatikani pamoja na sehemu nyingine za kata za Njombe Magharibi. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuziomba Wizara zinazohusika zilichukulie suala hili umuhimu wa kipekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kuzungumzia kuhusu suala la majambazi, rushwa na mambo ya ukwepaji kodi, sasa hilo kwa kweli nadhani …

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Rais.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, nakushukuru.

**MHE. GOSPERT B. BLANDES**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii, ikiwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia kwenye Bunge hili Tukufu. Awali ya yote, naomba nitoe shukrani kwa wananchi wangu wa Jimbo la Karagwe kwa kunichagua kwa kura za kimbunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi ulikuwa mgumu sana, lakini wananchi wa Karagwe waliamua kwa dhati kunichagua, nami napenda kuwahakikishia kwamba sitawaangusha, nitachapa kazi mpaka wafurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shukrani zangu nadhani sitatenda haki kama sitamshukuru kiongozi wa vijana waliojitolea, rafiki yangu Karim Amri, kwa niaba ya vijana wote wa Karagwe. Naomba apokee shukrani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa viongozi wote kuanzia Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika, wewe Mheshimiwa Naibu Spika, Mawaziri, Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa

kuchaguliwa na kushika nafasi ya kuongoza kipindi hiki cha 2005 hadi 2010. Nawaombea afya njema, Mwenyezi Mungu awajaalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa kweli ni nzuri sana na imezungumzia karibu yote ambayo yako kwenye ilani. Mimi leo hii nitagusia kidogo maeneo ambayo naona ni bora nichangie.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni hili suala la njaa. Mimi natoka wilaya ya Karagwe, wananchi wa Karagwe ni wakulima wazuri sana na ni wachapakazi, lakini kwa bahati mbaya ukame umewakumba na wamepata shida na sasa hivi wanahangaika na njaa.

Wakati Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anatoa taarifa hapa kuhusu usambazaji wa chakula, nimesikitika sana kuona kwamba wilaya yangu ya Karagwe na hasa Jimbo la Karagwe hawajapata mgao wa chakula mpaka sasa hivi. Nitamuomba Waziri wa Kilimo na Chakula ajitahidi sana kupeleka chakula Karagwe kwa sababu ninasumbuliwa na simu pamoja na ujumbe mfupi kwamba wananchi wanateseka sana na njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nigusie suala la mifugo. Kwenye Jimbo la Karagwe wananchi wa Karagwe ni wafugaji wazuri mno, tatizo walilonalo ni tatizo la ardhi, mahali pa kufugia. Serikali iliuza iliyokuwa ranchi ya Kitengule kwa kiwanda cha *Kagera Sugar,* sasa wananchi wamekosa ardhi.

Tulitegemea Serikali iwatafutie maeneo ya kufugia, lakini mpaka sasa hivi nimefuatilia kwenye Wizara ya Mifugo, nimeambiwa kwamba kuna *blocks*, vipande tisa ambavyo wananchi wanategemea kugawiwa kwa vikundi, lakini naomba suala hili lifanywe kwa haraka sana kwa sababu wananchi wanateseka sana na mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ambalo limejitokeza kuhusiana na ufugaji, Karagwe imetokea wimbi la wahamiaji haramu wenye mifugo mingi sana kutoka nchi jirani ya Uganda. Hawa wanakuja na mifugo mingi sana, wameingia Karagwe, siyo raia na mifugo yao haina kibali, inaharibu mazingira sana na wananchi wanakosa mahali pa kulishia mifugo yao.

Ninaomba Serikali kupitia Wizara ya Mifugo ilifanyie juhudi ya haraka mno iwezekanavyo ili hawa watu waondoke kwenye eneo la Karagwe ili wananchi wapate malisho ya mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Usalama wa Raia siyo jambo la mchezo. Mheshimiwa Rais amezungumza kwamba, hatawaacha majambazi watambe kwenye nchi yetu. Suala la ujambazi kwenye Jimbo la Karagwe imekuwa ni kama jambo la kawaida. Majambazi wanatamba kama wanavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi wakati niko hapa kuna gari moja la Halmashauri ya Karagwe likiwa linatoka mjini Bukoba kuelekea Karagwe na likiwa na mishahara ya Chama cha Mapinduzi limetekwa katikati ya njia ya Kyaka na Karagwe.

Kuna mama mmoja anaitwa Devotha Byashala alikuwa amebeba mshahara huo milioni 1 na laki 8 amechapwa viboko, alikuwepo *DAS* wa Wilaya ya Karagwe amechukuliwa Shilingi laki 5.

Kusema kweli tatizo la majambazi kwa Karagwe ni sugu mno na ninamuomba Mheshimiwa ambaye amepewa dhamana ya Usalama wa Raia ajikite kisawasawa katika Jimbo la Karagwe na hasa katika njia ya Karagwe kuelekea Bukoba kuna sehemu moja inaitwa Uzuri wa Kondoo, hiyo imekuwa ni kama kambi ya majambazi.

Vile vile njia ya kutoka Karagwe kwenda *BENACO Ngara,* pori la Kimisi hiyo ndiyo kambi ya majambazi. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri aweke mkakati maalum kwa ajili ya Jimbo la Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Rais imegusia suala la Maliasili na Utalii. Kwenye Jimbo la Karagwe ipo mbuga ya kuhifadhi wanyama inaitwa Kimisi ukiwa unatoka Karagwe kuelekea Ngara kupitia *BENACO.*

Hili Pori la Kimisi, zamani lilikuwa ni pori ambalo halikuwa hifadhi, lakini sasa hivi limekuwa Hifadhi ya Taifa. Tunafurahi sana kwamba Serikali imeliona hilo, lakini pamoja na hayo kuna matatizo ambayo hifadhi hii imetulea sisi wananchi wa Karagwe na hasa Kata ya Nyakasimbi ni kwamba mipaka ya Hifadhi ya Kimisi imeingia ndani ya mipaka ya Vijiji jirani, kiasi kwamba wananchi sasa wanasogezwa kutoka kwenye Vijiji vyao inatengenezwa hifadhi ya wanyama. Sasa mimi hapa napata shida kujua nchi yetu inamjali nani mnyama wa pori au raia wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la miundombinu namwomba sana Mheshimiwa Waziri, anayehusika na miundombinu aiangalie barabara ya Kyaka - Karagwe ambayo ni kilomita chache sana karibu kilomita 70 tunaomba sana watujengee barabara ya kiwango cha lami. Vile vile kutoka Karagwe Mjini kuelekea Ngara ni barabara ambayo inapitisha malori makubwa sana yaliyobabe kahawa, maharage pamoja na ndizi tunaomba ijengwe kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, akiwa kwenye kampeni aliahidi kwamba ataipatia umeme sehemu ya Nyaishozi na Mji wa Kyanyamisa, ni wakati muafaka sasa umeme kwenda maeneo hayo kwa sababu ni kilomita chache karibu 30. Umeme upo wa kutosha Karagwe, nguvu ipo kwa sababu unatoka nchi ya Uganda ambao hawategemei ukame kama huu wa kwetu huku kwenye *grid* ya taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la soko la maharage na ndizi. Wilaya ya Karagwe, inalima maharage mengi sana ya kulisha nchi hii na nchi jirani, lakini hawana soko. Tunazo ndizi za kutosha, tunaomba soko la kupeleka mazao haya nje ya nchi ili tuweze kujikomboa na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni tatizo sugu kwenye Mji wa Karagwe, Mji wa Kayanga na Mji wa Omurushaka, hili Mheshimiwa Rais, aliahidi kabisa kwamba atatupatia maji. Tunayo maji mengi sana ya kutosha, tunayo mito, tunayo maziwa, tuna ziwa Kajunju, linatosha kabisa kusambaza maji kwenye Wilaya ya Karagwe yote na Vijiji jirani kwa mfano Vijiji vya Thanda, Chonyonyo, Lukole, Nyakaanga vinastahili kupata maji kwa sababu maji si tatizo, tatizo ni mitambo ya kusukuma maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ndiyo ufunguo wa maisha, wanafunzi katika Jimbo la Karagwe, wamefaulu wengi sana lakini wameshindwa kuchaguliwa kuingia kwenye Sekondari kwa sababu madarasa hayatoshi. Wananchi wako wanajenga shule zao, Kata ya Kituntu imejenga shule moja na Kata zingine za Nyaishozi, tatizo imekuwa ni mabati. Tunaomba Serikali ipeleke mabati haraka sana tuweze kunusuru hawa watoto waingie shuleni waanze haraka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, afya na yenyewe imezungumziwa na Mheshimiwa Rais, katika hotuba yake, kusema kweli Jimbo la Karagwe lina tatizo sana ya zahanati na vituo vya afya. Utakuta kwamba kuna kata kwa mfano kama Kata ya Ihembe ambako mimi ndiko nazaliwa, kata nzima yenye vijiji 4 haina hata kituo kimoja cha zahanati wala kituo cha afya, wananchi wanatembea karibu km 30 kwenda kutibiwa kwenye Hospitali ya Wilaya ya Nyakahanga. Sasa tunaomba sana Wizara ya Afya, iwasaidie kwa haraka wananchi wa Kata ya Ihembe na kata zingine kwenye Jimbo la Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa kunipa nafasi na kwa vile ni mara yangu ya kwanza, awali ya yote napenda niwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Kilombero, Mkoa wa Morogoro kwa kuniwezesha kupata ushindi wa asilimia 80 dhidi ya wapinzani wangu. (*Makofi*)

Aidha nawapongeza pia kwa kumpa Rais wetu ushindi wa asilimia 90. Kadhalika nampongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika. Pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa nafasi aliyopata katika uteuzi wa Rais kwa nafasi ya Waziri Mkuu na kulidhiwa na Bunge lako Tukufu. Aidha nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa na Rais kushika nyadhifa zao. (*Makofi*)

Baada ya salaam hizi za shukurani, napenda nichangie Hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa kusema yafuatayo:-

Katika ukurasa wa 30 Mheshimiwa Rais amesema naomba ninukuu: “Serikali itahakikisha kuwa mpango kabambe wa umwagiliaji maji unaongezewa fedha na wataalam ili kupanua maeneo yanayotumika hivi sasa kwa kilimo cha umwagiliaji maji”. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki iliyopita tulikuwa na semina pale Dar es Salaam, Sera ya Kilimo, tulielezwa na ikaainishwa vizuri zaidi katika suala hili la kilimo cha umwagiliaji maji kwamba katika kipindi cha miaka mitano Wizara inakusudia kuweka hekta milioni moja katika kilimo hiki.

Sasa mimi nikiwa natoka kwenye eneo ambalo kilimo hiki kina nafasi nzuri ya kutekelezwa, naomba Wizara itupe kazi hiyo ya kulisha Watanzania. Sisi tuna maji ya kutosha, tuna mito zaidi ya 20 ya kudumu, kwa wale wasiofika katika eneo letu la Wilaya ya Kilombero kutoka Kidatu kuelekea Mlimba mpaka Taweta tuna mito mikubwa ya kudumu zaidi ya 20. Ninavyozungumza mito ndugu zangu kwa sababu hakuna mfano wa kuonyesha labda niseme zaidi ya Ruvu tunaovuka kutoka Dar es Salaam.

Mito hii inatoka kwenye hifadhi, ambako vyanzo vyake nina uhakika ni vya kudumu kwa sababu milima ambako mito hii inatoka ni milima ya Udzungwa na ni hifadhi kwa hiyo hamna siku ambayo milima hiyo itaacha kuleta maji. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile Wizara lazima itupe sisi kazi ya kulisha taifa hili ili tuondokane na aibu hii ya njaa. (*Makofi*)

Wilaya yangu ina uwezo wa kulima hekta 336,000 katika mpango wa umwagiliaji maji. Mkoa mzima wa Morogoro unaweza kulima hekta 434,000. Kwa hiyo, tunachoomba kwa Wizara kama ilivyoitwa kuweka mpango kabambe wa umwagiliaji maji. Picha ninayopata mimi ni kama Mpango wa Kilimo cha Gezira Sudan. Kwamba kama ni Gezira basi Gezira ihamie kwenye *Kilombero River Basin*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza vizuri mpango huu tunaomba Wizara itutafutie huduma hizi za ugani mapema ikiwezekana waende kwenye *study tour* na Wabunge wa pale ili waende wakaone jinsi sehemu kama hizo za Gezira zinavyofanya kazi.

Pia, sababu nyingine ni kwamba hata Waziri Mkuu, alipokuwa anahitimisha katika *point* yake ya pili, alisema kwamba rasilimali za umwagiliaji tunazo, kwa hiyo tusije tukaenda kwenye maeneo madogo madogo wakati kuna maeneo makubwa na sisi bahati nzuri katika kampeni wananchi tumewa- *sensitised* kwa kilimo hiki kwa hiyo, wanangojea kazi hiyo. Kwa hiyo, nina uhakika Waziri ataweka Wilaya yangu kwenye mpango huu kabambe na kama hakuuweka nafikiri atauingiza leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye eneo lingine la kilimo cha miwa. Sisi Wilaya yetu ni wazalishaji wa sukari. Wakulima wadogo wadogo ambao wanazunguka Kiwanda cha *Kilombero Sugar Company* wamefanya kazi nzuri sana. Wao ndiyo wanaozalisha asilimia 53 ya miwa yote inayokwenda kiwandani, wakati kiwanda kinatoa asilimia 47. Lakini wale wakulima wadogo wadogo wana tatizo moja, msimu wa kuvuna miwa yao unapita miwa yao hawana mahali pa kuuza kwa sababu kiwanda kimezidiwa. Wale wananchi wengi wao wamechukua mikopo kwenye *SACCOS,* kwenye Mabenki inakuwa ni shida kurudisha. Wamefanya jitihada wamezalisha vizuri lakini hawana mahali pa kupeleka miwa yao. Kwa hiyo, naomba Wizara inayohusika na ubinafsishaji au wawekezaji waone jinsi gani viwanda vile vinaweza vikatatua tatizo hili kwa kununua miwa ya watu waliyolima kuzunguka kiwanda hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kuongelea hapa katika Wilaya yetu kuna shamba lililokuwa linalimwa kwa ushirikiano wa Serikali yetu na Serikali ya Korea lilikuwa linaitwa shamba la *KOTACO (Korea Tanzania Cooperation)* Wakorea wameondoka mwaka 1994 mpaka hivi leo lile shamba lilibinafsishwa likachukuliwa na mwekezaji mmoja lakini kinachoonekana pale zaidi ni kuhodhi ardhi, yale mashamba ambayo yalikuwa *destumped* kwa, kung'oa miti sasa hivi miti hiyo imeota tena na wananchi ambao wametoa ile ardhi kwa kujua kama hapa kuna mwekezaji wanazunguka wana hamu ya kuilima hawaruhusiwi. Sasa kwa vile ardhi iliyobaki pale ni kama imehodhiwa nilikuwa naomba Waziri, anayehusika na jambo hili awaruhusu wananchi wa Tarafa ile ya Mngeta ambako shamba hilo liko walime lile shamba kuliko kuliacha tu na mtu amelihodhi bila matumizi yoyote ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni miundombinu, Wilaya ya Kilombero kila mtu anajua tunalisha sehemu nyingi sana. Tukivuna mpunga watu kwanza kuja kununua ni watu wa Pemba. Lakini miundombinu kwa maana ya barabara katika Wilaya ile ni mibaya. Sasa barabara mara nyingi hufuata bidhaa, tunalisha Dar es Salaam ndizi, mpunga, mahindi. (*Makofi*)

Naomba Serikali itufikirie kutupa barabara yenye kulingana na mazao tunayozalisha. Wilaya yangu kuanzia mwanzo mpaka mwisho ina umbali wa km zisizopungu 300 na katika Wilaya nzima ukiondoa labda sehemu ya Mgodi wa Kihansi ambao una kilomita 30 za lami hamna lami tena. Ni mwaka juzi tu walipewa kipande kidogo cha km 12 cha lami, sasa hiyo kazi imefanyika mpaka leo miaka miwili yule mkandarasi anahangaika kujenga kilometa 12 za lami, inasikitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni umeme. Umeme tunazalisha katika migodi miwili ya Kihansi na Kidatu. Lakini wananchi kazi yao ni kulinda zile *pylons* zinazopeleka umeme *grid* ya taifa. Kwa kweli inasikitisha hata kama Wilaya yangu haifanya kazi ya kuzalisha kama Wilaya lakini umeme unatoka kule na ni vizuri wananchi wale tukawapa angalau *priority* ya kupewa umeme ili wawe walinzi wazuri wa zile *pylons* zinazobeba umeme *grid* ya Taifa.

Kwa hiyo, hapa naomba Serikali ifanye jitihada angalau chini ya Mfuko wa Nishati Vijijini, wale wananchi wote ambako umeme umepita karibu yao wapewe umeme kama kipaumbele ili wawe walinzi wazuri kuliko kulinda *pylons* ambazo wananchi wengine mnakuja kupata umeme huku na wale wananchi wa Wilaya yangu wakiwa na manung'uniko. Ni kibinadamu tu kwamba angalau umeme umepita kwao na wao wafaidike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Rais. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami kunipatia nafasi ili nichangie Hotuba hii ya Rais, ili nisije nikamaliza wakati kabla sijaunga mkono. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makosi*)

Awali ya yote nampongeza mwenyewe Mheshimiwa Rais kwa ushindi wa kishindo katika uchaguzi, Makamu wake Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar, Waziri Mkuu, ambaye vile vile tulimthibitisha kwa kishindo hapa. Nampongeza vile vile Mheshimiwa Spika, kwa kushinda pamoja na wewe Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofi*)

Vile vile nawapongeza Mawaziri wote na Naibu Waziri waliochaguliwa. Naona safu iliyochaguliwa safari hii nayo ni njema na itafanya kazi zake vema kabisa. Mwisho kabisa nawapongeza Wakuu wa Mikoa wote waliochaguliwa hivi karibuni na leo kuapishwa. (*Makofi*)

Ili nisiwe mwizi wa fadhira nawashukuru sana wanachama wote wa CCM wa Jimbo la Koani ambao katika kura za maoni waliniambia niendelee kuwa Mbunge. Lakini vile vile baada ya mchakato wa uchaguzi mkuu nawashukuru wanachama wangu wa CCM wote. Lakini vile vile vyama vya upinzani. Kwa nini nimesema hivyo, mimi nadhani upinzani wa vyama watu wa Unguja wanajua namna ya kumteua mtu na kumchagua, tofauti na upande wa pili wa Kisiwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa mwenzangu Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, alipata asilimia 64 ya kura zote zilizopigwa katika Jimbo langu la Koani. Lakini kwa vile ndugu zetu wapinzani, waliona kwamba huyu tutampa kura zaidi walinipa asilimia 74. Sasa nashangaa upande wa pili wao hata akitokea mgombea mmoja awe mzuri wa aina gani mwenye utendaji mzuri wa aina gani, wao wanasema huyu *no*, huo siyo ugomvi, vyama vya siasa ni utendaji mzuri na tunataka sote tujenge nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Hotuba ya Rais ya tarehe 30 Desemba na nasema hayo kwa sababu nimewasikiliza ndugu zetu wa upinzani wote hakuna hata mmoja aliyesema haiungi mkono. Hata ndugu yangu mpenzi wangu Mheshimiwa Sanya ameiunga mkono. Sasa mimi nashangaa wameiunga mkono hotuba hii, yaliyokuwemo humu ndani ya hotuba hii yote Mheshimiwa Rais, ameyachukua katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Kwa maana hiyo, kumbe wanaelewa kwamba mambo mazuri ndiyo haya katika ilani ya uchaguzi kilichobakia Mheshimiwa Sanya na wenzako tunawaomba kama walivyokuwepo wenzenu waliokuwepo hapo mbele leo mnaona wako huku wengine Mawaziri na Inshallah na nyie mtaonekana vile vile. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, katika hotuba yake amezungumzia sana suala la umoja wa kitaifa na ninadhani tukirejea nyuma sijui kwa nini tukawa sasa tunanung'unika, tunapiga kelele kama vile Muungano wetu siyo. Mimi nawambia ndugu zangu tunaotoka Visiwani kabla ya mwaka 1964 kulikuwa hakuna siyo Mpemba tu hakuna Mzanzibar hata mmoja utakayemkuta Kigoma, Shinyanga, Kahama na

kwingineko. Muungano huu ndiyo uliosababisha kwamba leo unapokwenda kama hotuba inavyoeleza hapa kwamba ndugu zetu wa Pemba wako katika kila eneo la *mainland* wapo kule. Sasa Muungano lazima tuimarishe. Tukifanya mchezo wetu tutajikuta mahali pabaya. Leo tumo ndani ya Bunge hili sisi Wazanzibar wenzetu wa huku hawapo kule kwa sababu ya Muungano. (*Makofi*)

Kulikuwa na suala ambalo alizungumza Mheshimiwa Yahya, asubuhi hapa ilikuwa nilizungumze lakini mimi sitasema chochote kwa sababu ameyamaliza. Nitaongezea jambo moja tu la uchaguzi wa mwaka 1963 walipounganisha Chama cha *ZPPP* na Chama cha *ZNP* ambacho kilikuwa Hisbu. Baada ya makubaliano ya vyama hivyo ikawa *Afro Shiraz Party* ikashindwa kwa kiti kimoja tu. Lakini cha ajabu vyama viwili vimeungana na Majimbo wamepata mengi zaidi lakini asilimia ya kura ya chama *Afro Shiraz Party* ilikuwa asilimia 54.6. Muungano wa vyama viwili hivyo waliopewa madaraka waitawale nchi ile ilikuwa 55.4. (*Makofi*)

Wao wanasema sasa hivi hakuna demokrasia, sasa je, ilikuwa demokrasia pale? Kukipa vyama viwili ambavyo asilimia ya kura zilikuwa chache na ndio maana kwa maana ile wazee wetu ndiyo wakaamua wajumbe wale 14 ambaye mmojawapo jana amefariki maskini Mwenyezi Mungu, amrehemu. Wakasema hapa mtindo huu utakwenda milele nchi hii ni yetu na sisi tuna haki ya kutawala tunadhalilishwa ndiyo walipoamua tarehe 12 Januari 1964 kupindua. Kwa hiyo, tunaposema Mapinduzi, Mapinduzi yale ni halali tuyakubali sote tulikuwa wanyonge. (*Makofi*)

Hata mimi na wenzangu wale kule mbele hatukuwa hivi leo, tulikuwa dhahiri wanyonge. Wengine Makunduchi wanatoka wale pale, wengine Koani wakibeba nazi kwa punda. Hakuna hata mmoja miongoni mwao na mwetu sisi aliyekuwa angalau anamiliki gari wakati ule kwa sababu tulikuwa tunatawaliwa na *Sultan*, leo utawala umeondoka basi tunapiga kelele, tuungane tupige kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la michezo. Katika jambo ambalo Mheshimiwa Raiss Jakaya Kikwete, ameliona ni suala la michezo. Kwa nini nimesema hivyo, mgogoro wa michezo hasa mchezo wa mpira ulikuwa unadharirisha nchi hii, unadorora kadri ambavyo tulikuwa tunakwenda ilikuwa tunaanguka kimichezo. Lakini amefanya nini, Wizara hii inasema hivi michezo, burudani na Utamaduni, Naibu Waziri ni mtu wa michezo, ukimpa mpira atacheza, akipiga mpira atafunga goli, ukimwambia ongoza mpira ataongoza.

Lakini huyu Waziri, mwenyewe ni mtu wa burudani na Utamaduni Mheshimiwa Mohamed Seif Khatib. Ukimwambia kuimba ataimba, zamani alikuwa mwimbaji huyu, anaimba, burudani zote anaziweza. Kwa hiyo, Wizara hii nina imani kwamba mambo matatu haya yatakwenda vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo vile vile nazungumzia suala la mambo ya Muungano. Nimefurahi kwamba Dr. Hussein Ali Mwinyi, amechaguliwa Waziri wa Mambo ya Muungano. Lakini asubuhi nilipokuwa nikiuliza swali la nyongeza hapa nasikitika namuonea huruma kwa sababu ni mpya bado lakini swali langu hakunijibu. Chuo cha Sayansi *Marine* kiliazimia kujengwa miaka 20 iliyopita mahali ambapo waliamua kukijenga chuo kile kilikuwa Mkokotoni ni maili nyingi sana kutoka

Mjini. Wamejenga nyumba moja pale baadaye wakabadilisha eneo ndiyo wakapeleka Buyu Mkoa wa Kaskazini. Sasa nilichokitaka mimi aniambie Naibu Waziri anijibu, sasa namuachia Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, atafuatilia kwa sababu yeye ni Waziri wa Mambo ya Muungano, lile jumba lilijengwa Mkoa wa Kaskazini kule halina kazi yoyote sasa limekataa kwa sababu chuo kinajengwa Mjini Magharibi kwa hiyo, wapewe Serikali ya Mkoa wa Kaskazini walifanyie kazi lisikae bure likaanza kavuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo napongeza sana Wizara ya Fedha Bara tulipiga kelele kuhusu *BOT* na mwisho miaka miwili iliyopita tukawapa kiwanja na sasa hivi limeshajengwa baada ya miezi sita Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, atakwenda kulifungua. Nawapa hongera sana. (*Makofi*)

Sasa mfano huo huo tunamuomba Waziri wa Mambo ya Muungano Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, ni fedheha kwamba Makamu wa Rais hana Ofisi Zanzibar. Tuliwapa kiwanja wakakikubali wakazungushia uzio wataalam gani hao wamekwenda mahali wameangalia, wamefanya kila kitu wame-*check* mpaka mchanga baadaye wamesema hapafai? Huo si utendaji. Tunaomba sana Waziri anayehusika ahakikishe anapatiwa kiwanja kingine na akisema mimi niko tayari kusimamia wapate kiwanja lakini Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar ijengwe hatuwezi kusema Muungano kama Ofisi ya Makamu wa Rais haipo pale Zanzibar leo akienda kule anakaa wapi? Yeye Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi akienda kule Waziri wa Muungano atakaa wapi? Sasa ninaomba sana asimamie hilo.

La mwisho ni kuhusu maslahi ya Watumishi, nimefurahi sana kwamba katika ukurasa wa 25 kwa hiyo Watumishi wa Serikali kwa kweli mishahara ni midogo sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, bahati mbaya sikuwepo tulikuwa na Kamati ya Miundombinu nikaomba kwamba labda tukimaliza kikao chetu ndiyo nije niungane pamoja na wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikushukuru na nikupongeze kwa kuchaguliwa kwako lakini pia nitumie nafasi hii kukuomba unipelekee salama zangu kwa Mheshimiwa Spika, kwa jinsi mlivyopata kura nyingi. Pia napenda nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutupatia Rais ambaye kwa kweli Watanzania wote wameona kwamba huyu ndiyo kiongozi anayefaa kutuongoza katika kipindi hiki yeye pamoja na Mheshimiwa Makamu wake pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Bahati nzuri mimi wote hawa nawafahamu na bahati nzuri walipojiunga na Chama cha Mapinduzi wakati huo *TANU* mimi nilikuwa nafanya kazi Makao Makuu ya Chama na nilishangaa vijana hawa walikuwa wanafuata nini Makao Makuu. Walikuwa na elimu ya kutosha, ambao tulikuwa na elimu tulikuwa wachache Makao Makuu, kumbe sikujua siri ilianza pole pole.

Wamejengwa ndani ya chama na ndiyo maana nilipoona wanaaomba nafasi hizi sikusita hata kidogo, niliwaunga mkono kwa sababu najua chimbuko lao ni nini, wamelelewa na chama, wamekuzwa na chama, wanakifahamu chama na wanafahamu matatizo ya wananchi. Mimi nawatakia kila la kheri Mwenyezi Mungu awasaidie ili tuondoke katika adha hii. (*Makofi*)

Pili nataka nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuchagua Baraza la Mawaziri, Baraza zuri kabisa. wengi ambao wameingia wameanza kujitahidi kuonyesha kwamba wana uwezo.

Ingawaje siku za kwanza sisi tulipata shida wakati tunaingia kwenye Baraza la Mawaziri, Mheshimiwa Anne Makinda, tulikuwa naye tena kwenye Ofisi ya Mzee Marehemu Sokoine, ilikuwa ukisimama pale ukijibu vibaya pale pale anasimama Mzee Sokoine Mheshimiwa Waziri, usiwadanganye wananchi, anakuambia pale pale jibu vizuri, kama ni hapana ni hapana, *style* yake mzee yule ilikuwa ndiyo hiyo. (*Makofi*)

Nimekuwa nikiwaomba wenzangu pia ambao wako ma-*front benchers* wajitahidi hata kama haiwezekani, tusipakane mafuta Tuambizane ukweli. Tusitoe ahadi ambazo wakati mwingine tunakwenda kuaibika kwenye Majimbo yetu. Unakaa miaka mitano wanasema ulisema hivi na hivi mbona hakuna lolote. Ni vizuri mkatusaidia mkawa wakweli hatutasikitika kama ukweli utakuwa na maelezo yake. Baada ya kusema hayo sasa nataka niunge mkono hoja ambayo iko mbele yetu: "Hotuba ya Rais" na mimi nasema naiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

Lakini niwakumbushe mtu mmoja ambaye mimi nilikuwa namkumbuka sana ametusaidia kwenye kampeni ni Mama Salma Kikwete. Mama Kikwete sehemu zote alizopita kwa kweli ametusaidia. Mimi kwa taarifa yenu kampeni yangu ya mwaka 1995 ya kwanza nilishinda kwa asilimia 80 ya mwaka 2000 nikashinda kwa asilimia 86 ya mwisho 2005 ambayo tumemaliza mwaka jana nilishinda kwa asilimia 93. Nimewagaragaza wapinzani mpaka wakasema afadhari ungepita bila kupingwa. Lakini namshukuru aliyenisaidia alikuja kwenye kampeni tukasaidiana wote kwa pamoja. (*Makofi*)

Sasa nini tunafanya; Wajibu wa chama chochote cha siasa kwanza ni kuandaa sera ambazo zikikubalika basi tushike dola. Baada ya kuandaa sera na kushika dola wajibu wa pili ambao ni muhimu ni kuandaa watu wako watakaosimamia sera yako. Usipokuwa na watu wako sera unaweza kuona nzuri lakini ukashindwa kusimamia utekelezaji. Ndiyo maana nataka nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa hatua hii aliyoichukua ya kuanza kuandaa watu na mimi ningemuomba aandae katika ngazi zote akishamaliza Wakuu wa Mikoa aingie Wakuu wa Wilaya, aingie Wakurugenzi, aingie Taasisi mbalimbali, kwa sababu lazima uwe na watu ambao kwa kweli watakufanyia kazi ambayo unaitaka. Wale ambao wataonekana wanasuasua tusitie shaka wala tusiwaogope waondoke tu. Kama wanasuasua hawaendi kwa kasi anayoitaka yeye mwenyewe asisite afanye kazi yake, ama sivyo baada ya miaka mitano tutashindwa la kusema. Hilo ni ombi langu. (*Makofi*)

La pili, ni kusimamia utekelezaji wa wasimamizi. Wasimamizi wakubwa ni Wabunge hapa. Wasimamizi wakubwa wa sera yenyewe ya Chama cha Mapinduzi ni Wabunge kwa kuwahoji Mawaziri mmefanya nini kutekeleza yale ambayo yamo ndani ya ilani. Mimi la kwanza ambalo nitawauliza kwa sababu katika Ilani ya Uchaguzi imezungumza kwamba kipaumbele cha kwanza kwenye miundombinu ni barabara ya Sumbawanga mpaka Tunduma.

*Number one* utaacha nyingine zote katika ilani ya uchaguzi kama mnayo nakala barabara ya kwanza iliyotajwa ni Tunduma - Sumbawanga. Nipenda kusikia Mawaziri wananiambia wametekeleza namna gani ilani ya uchaguzi ama sivyo kusipokuwa na utaratibu wa utekelezaji tutakwama, tutakuwa tunapiga maneno miaka inakwenda hakuna lolote litakalokuwa linafanyika. Mimi naomba hilo msimamie utekelezaji. Lakini pia nataka nimuombe Rais kuwa katika utaratibu tulionao ni vizuri tukajipanga upya. Kujipanga upya si upande wa vyombo vya Serikali, si upande wa taasisi zake lakini pia na sisi tutaanza kujiangalia ndani ya chama.

Ndani ya chama kujipanga upya maana yake je, wote tuliopo hapa tutakwenda kwa kasi hiyo hiyo ambayo Rais wetu anayo, tutasimami shughuli zote ambazo zimeandikwa katika ilani ya uchaguzi kwa misingi hiyo hiyo tuliyokuwa nayo? Ndio maana nasema kwamba yote hayo lazima yaende sambamba bila kuacha upande mmoja. Asili yetu ya uongozi ni watu. Baba wa Taifa alisema hivyo. Asili yetu wote ya uongozi ni watu wote tumetokana na watu hapa na ndio maana mimi nitashangaa kudhani ya kwamba Wabunge wanaweza kukaa hapa wakawasaliti watu wao. Kwa sababu tumetokana na wao lazima tutawaheshimu, tutawatetea mpaka tuone ya kwamba wanafanikiwa kwenye mambo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuna dhana ambayo iko mbele yetu ya kwamba labda Wabunge wanatetea maslahi yao. Mimi nasema demokrasia adui yake mkubwa ni uoga. Demokrasia yoyote ukitaka isitekelezwe wajibu wake ingiza uoga ndani yake hamtafanya kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio msingi ambao nadhani lazima tuuzingatie na sisi tusimamie haki na kuwatetea wananchi wetu kwa misingi bila kuogopa, hiyo kazi mojawapo tutaifanya najua yapo mengi ambayo tungeweza kuzungumza lakini kwa ajili hali yenyewe hiyo lazima tuangalie. Mimi ningependa kukumbushia mambo matatu ya haraka, kwanza ni ahadi za Serikali kwa miaka karibuni kumi ambayo nimekaa ndani ya Bunge kumekuwa na ahadi nyingi sana ni vizuri tukazirejea, tukazipitia na kuona zile ambazo kwa kweli haziwezekani basi tuambiwe.

Nitawapeni mfano, kwanza barabara ya Sumbawanga – Tunduma ni nimeshaizungumza ambayo tulishazungumza ya kwamba iwekwe barabara ya kuunganisha mikoa ya Ziwa ya Magharibi inayokwenda mpaka Kagera bila wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia suala la maji katika mji wa Sumbawanga nimekuwa kila wakati nazungumza tumeambiwa kuna Benki ya Dunia itakuwa kusaidia, tukaambiwa kuna *BADEA* ambayo ni Benki ya Warubuni lakini mpaka sasa hakuna

lolote linalofanyika. Nini kinajaribu kufanyika? Mwaka jana nilipata nafasi ya kuhudhuria mkutano Durban *South Africa* nikagundua kuna kitabu kimoja ambacho kinaitwa *Lake Victoria Region Water and Sanitation Initiative*.

Hiki ni kitabu ambacho kimetolewa *UN Habitat*, hiki kinaelezea mikakati ya kusaidia miji kwa nchi tatu Kenya, Uganda na Tanzania na dola karibuni milioni 19 zilikuwa zitengwe kwa kusaidia, pia kuanzia miji ya Mwanza, Sengerema, Geita, Biharamulo, Bukoba ni miji ambayo imeandaliwa ya kwamba ilikuwa tangu 2002 iwe ni *Regulation* ya mwaka 2002 ilipitisha, Umoja wa Maitafa walipitisha chini ya mpango *NEPAD. L*akini mpaka sasa hakuna lolote linafanyika. Sasa *speed* tunayokwenda nayo tutakosa mengi, kama tunakwenda na *speed* ya kusuasua wenzetu watatuwahi, Waziri aniambie tumefikia wapi katika suala hili ama sivyo tutakuwa tunachezea tunaandika ma-*document* bila kujua kitu gani kinafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mengi tungeweza kuzungumza lakini kwa kujenga heshima ya muda, naunga hoja mkono. (*Makofi*)

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo na uhai wa kufika hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Mimi nina mambo manne tu katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo hotuba hiyo naikubali moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu Tume ya Uchaguzi ambayo imezungumziwa katika ukurasa wa sita, la pili ni mpasuko ambao umezungumziwa katika ukurasa wa 18, la tatu ni usalama wa raia na utawala bora ambao umezungumziwa katika ukurasa wa 21 na 22 na ya nne ni suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki au shirikisho ambalo limezungumziwa katika ukurasa wa 58 na 59.

Mheshimiwa Naibu Spika, sadaka huanza nyumbani kwa hivyo naanza na mpasuko, Mheshimiwa Rais alisema kwa uchungu mkubwa sana kwamba kuna mpasuko, ana uhakika kwamba kuna mpasuko na mimi nakubaliana nae. Lakini sasa ukisikiliza baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaosema hakuna mpasuko ninasikitika sana na kwa kimila, mila zetu za Tanzania baba anaposema au mzee anaposema na akatokea mtoto akapinga basi mtoto yule humwita nunda na humtia adabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sijui CCM kwa Wabunge hawa wanaokana maneno ya Mheshimiwa Rais sijui mtawachukulia hatua gani, maana yake ndio wazee na wazee wanapokosea au watoto wanapokosea basi wazee wanawajibika kuwapiga bakora kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba kuna mpasuko na nasema haya kwa uhakika na nina mambo mengi sana lakini kwa sababu ya muda nitazungumza mambo matatu au manne. Kwanza mimi napenda niseme nimekuwa katika Baraza la Wawakilishi tokea mwaka 1995 mpaka leo na huko nyuma niliwahi kuwa katika Baraza la Wawakilishi na ni kiongozi wa Upinzani katika Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kusema kwamba mfano mmoja wa Bajeti ya Mawasiliano tuliirudisha mara mbili sisi kwa sababu ya mpasuko huo. Bajeti ya Mawasiliano nina kitabu cha Bajeti ninaweza nikakuletea, ilitoa Bajeti hiyo asilimia 93 kwa shughuli za barabara za Unguja, asilimia saba kwa barabara za Pemba na huko Pemba ndio kwenye vuno au mazao yote ya karafuu, asilimia 90 ya mazao hayo lakini hakuna barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Pemba nikikuchukua katika barabara za Pemba ukirudi hapa itabidi nikodi wale watu wanafanya *massage* kutoka Hong Kong kuja kukufanyia kwa sababu ya barabara mbaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ubovu wa barabara hizo, Wabunge na Wawakilishi wa *CUF* wakadhubutu kununua lami yao wenyewe angalau mule mahali ambapo hapapitiki kuwekwe lami. Nakuhakikishia kwa masikitiko makubwa Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikwenda na vikosi vyake wakapiga risasi matangi ya lami, wakasema lami ile tunywe sisi *CUF*. Sasa hiyo ni hali mbaya ya kusikitisha na mimi siilaumu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nailaumu CCM kwa sababu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliwekwa na CCM. Kwa hiyo, hiyo ndio hali ya CCM wanayofanya Pemba, Mheshimiwa Mbunge wa Gando yupo aliyenunua lami, Mheshimiwa Mwakilishi wa Gando yupo walionunua lami na lami hiyo Serikali ikapiga rasasi lami ikamwagika bure. Sasa hii ni hatari gani ambayo inafanywa na Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, kwa mfano katika Baraza la Mawaziri 14, kuna Waziri mmoja tu kutoka Pemba. Mimi najiuliza hivi kweli CCM hawa walioko wawili Pemba hawawezi kuteuliwa chini ya kifungu cha 66 cha katiba? Kwa sababu Rais anao uwezo wa kumteuwa mtu akamfanya Waziri na hivyo ndivyo walivyofanya kwa kumteuwa kwa mfano Mhshimiwa Adam Mwakanjuki, kwa kumteuwa Asha Abdallah, kwa kumteuwa Ramadhan Abdallah Shaban wote wameteuliwa chini ya kifungu hicho. Kwa nini asiweze kumteuwa angalau mtu mmoja au wawili wakawe Mawaziri kutoka Pemba? Huo ni mpasuko mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sera kwa mfano ya elimu ambayo imepitishwa juzi, sera ya elimu hii ni ubaguzi wa hali ya juu na sisi tulipinga kwa sababu sera ya elimu ile inaonyesha dhahiri kwamba mtoto anayesoma Pemba mpaka afike *form four* au darasa la 12 hana ruhusa ya kuja Unguja asome kule kule, hii ni sera gani ya elimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa baadhi ya Wabunge walizungumza wakasema kwamba *CUF* au sisi ndio tunaanza chokochoko. Ninasikitika sana kwamba hili si la kweli hata kidogo. Nina ushahidi wa kutosha hapa ambapo Serikali ilienda ikaanza

chochoko kwa wananchi wa Pemba; na chokochoko hizo ni baada ya uchaguzi watu walipigwa, watu walinajisiwa, watu walinyang'anywa vitu vyao na walifanyiwa mambo chungu nzima. Hayo yote ni kuwaonyesha ni jinsi gani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na CCM inawafanyia watu wa Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linazidi kuiingia nguvu kwa mfano, katika hoja ambayo aliitoa Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir alisema kwamba watu ndio wanaoanza kuchokoza. Si kweli watu wamekwenda wameonewa, wamepigwa na ushahidi upo na hii sisi tulifanya kwa mfano katika Baraza la Wawakilishi tulitaka kupeleka hoja ili watu hawa wote ambao wanahusika na vitendo hivyo iundwe Tume ichunguze.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasikitika kusema kwamba Baraza la Wawakilishi na Serikali hoja hiyo ilinyamaziwa kimya na haikuletwa katika Baraza wala hatukupewa habari yoyote kwa nini ilikataliwa hoja hiyo, ikiwa aliyefanya vitendo hivyo ni mwananchi wa kawaida au ni *CUF* basi atapata adhabu. Lakini kwa sababu wanaona dhahiri kwamba ni Serikali ni vikosi vya SMZ ndio wakanyamaza kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hiyo baada ya kupeleka ombi la kupeleka hoja hiyo na wakaona ukweli uliopo Serikali au Baraza la Wawakilishi walikaa kimya wakafyata, tunaita kwa Kiswahili wakafyata mkia. Kufyata mkia ni suala zima kwa mfano tunapokuwa na wanyama kama vile paka na mbwa kama utamtokea amefanya kitu na kitu kile kikawa ni kweli basi unapotaka kumpiga mbwa yule au paka yule hulalia mkia wake na kukupembejea kama kwamba anaomba radhi. Kwa hiyo ndio hali ya Serikali inavyofanya katika masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo kwa sababu sina muda nakuja …….

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wa Spika, naomba kifungu 50 (1) ambacho Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anachangia amesema kwamba Serikali ilileta chokochoko ikanajisi, ikafanya mambo ya ajabu ajabu. Ninaomba kauli yake Mheshimiwa aidhibitishe au aifute. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nilivyosikia mimi ni kwamba anasema baada ya uchaguzi kulikuwa na vitendo vya namna hii sikusikia Serikali. (*Makofi*)

Muda ulikuwa umepita kwa hiyo kengele imegonga wakati Mheshimiwa anauliza hoja, kwa hiyo tunaendelea.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia afya njema pamoja na nyie wenzangu tukakutana tena hapa kwa kikao hiki. Pia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwawezesha watu wa Jimbo langu la Mkanyageni kwa kunichagua mimi niwe mwakilishi wao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru wewe pamoja na Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wabunge wenzangu wengine kwa kuchaguliwa. Pia

nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa na kuna sababu nyingi za kuipongeza hotuba hii, ni hotuba ambayo imejaa hekima, imejaa busara na ina falsafa nyingi. Pamoja na kwamba hotuba yake imechukua mengi katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM lakini na mimi nasema hotuba hiyo hiyo pia imechota mengi katika Ilani ya Uchaguzi ya *CUF*, Ilani ya Uchaguzi ya CHADEMA pamoja vyama vingine vya siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana inaungwa mkono, ni kwa sababu hizo kwa sababu italeta maendeleo kwa Watanzania wote na hilo ndilo tunalolitaka sote ikiwa ni mpinzani, ikiwa ni wa chama tawala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ningeomba kuzungumzia suala haki za binadamu, hakuna budi kama msemaji mwenzangu alivyotangulia kuna uvunjifu mkubwa wa haki za binadamu. Matokeo ya kuuwawa watu wasio na hatia, vipigo, kesi za kubuni matokeo ya Mahonda, Tumbatu mjini Magharibi, Pigi, Wete ni ushahidi tosha wa uvunjifu wa haki za binadamu .Yaliyotokea, yaliyotendeka yameonekana Dunia nzima kupitia mitandao iliyojaa leo wala hayahitaji ushahidi mwingine wowote. Yote yamefanywa na vikosi vya *SMZ,* uvunjifu huu wa haki za binadamu ni kinyume kabisa na katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.Roho za binadamu si haki kutolewa hivyo hivyo na katiba yetu inapinga hivyo. Vifungu vya 14,15 na 16 Sheria ya 1984 Na.15 Ibara ndogo ya 6 inazungumzia masuala hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukazungumza kwamba mambo hayo yaliyotendeka labda yamefanywa na vikosi vya Zanzibar. Lakini pia vikosi vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano vimeshiriki pamoja na kwamba siyo sehemu zote lakini vitendo vya kumwagiwa maji machafu ya watu walio msikitini wanaoswali hawana tatizo lolote katika misikiti ya eneo la Nyerere vinadhihirisha uvunjaji huo wa haki za binadamu. Serikali ya Jamhuri haiwezi kukwepa lawama kuhusu uvunjaji huo wa haki za binadamu kwa sababu sheria ya ulinzi *The National Defence Act* ya 1965 inasema wazi na inaeleza dhahiri, kwa hivyo Amiri Jeshi Mkuu ni Rais wa Jamhuri ya Muungano, hivyo Jamhuri ya Muungano kwa upande mmoja haiwezi kukwepa lawama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mfano uliotokea miaka ya 60 katika kijiji cha Kangani Pemba, wakati huo Chama Tawala *ZNP* aliuliwa mtu wao na wao ndio wanaotawala lakini badala ya kupiga watu na waliposhindwa wao upelelezi wakaleta askari kutoka *Scotland Yard* na ukafanywa upelelezi mtu mmoja akatiwa hatiani na muda wote wa matukio ni watu nne tu waliowekwa kizuizini, iweje leo Waafrika wenyewe afanye kosa mtu mmoja au wawili kiadhibiwe kijiji chote na mifano hiyo imetokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais amesema katika hotuba yake kwamba anataka kujenga demokrasia ya kweli. Basi na mimi nashauri tumsaidieni Rais maana sote tunapenda amani na utulivu ya kweli siyo amani na utulivu wa majukwaani. Tumsaidieni kwa uwezo wetu wote na njia moja ya kumsaidi Mheshimiwa Rais ni kuunda Tume, Tume itakayojumuisha Wabunge, Wawakilishi, wataalamu wa sheria na wajumbe wa vyama vyote kuchunguza haya maafa yote na matukio ya daftari la kudumu.

Yachunguzwe matukio ya daftari la kudumu, matokeo ya uchaguzi na vitendo vyote vilivyosababisha uvunjaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mpasuko, napenda kwanza ninukuu ukurasa wa 18 Mheshimiwa Rais amezungumza wazi wazi kwamba, " Nachukua uongozi wa Taifa letu nikiwa nasononeshwa sana na mpasuko wa kisiasa kati ya Unguja na Pemba na pengine kati ya Pemba na sehemu nyingine za Jamhuri ya Muungano, matokeo ya uchaguzi mkuu wa 2005 yametukumbusha tena mpasuko huo."

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo halipingiki lakini inaonekana katika wachangiaji wengine wanasahau. Naomba ninukuu kipengele kimoja kukumbusha tena Mheshimiwa Rais amesema kwamba, "Mpasuko huo ambao ninaamini chanzo chake ni cha kihistoria, lakini historia hiyo ni ya wanadamu na wanadamu hawalazimiki kuwa wafungwa wa historia."

Mheshimiwa Naibu Spika, historia gani hiyo leo tukumbushane miaka hiyo, mimi wazee wangu wote walikuwa CCM labda walikuwa *Afro-Shiraz Party* lakini mimi *CUF* haikunifunga historia ninatizama muelekeo wa leo na imani inavyonipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la mwisho la nishati. Katika ukurasa wa 57 Mheshimiwa Rais amezungumzia umeme wa kudumu, makaa ya mawe ya Mchuchuma na gesi ya Mnazi *Bay* itatusaidia sana kwa mujibu wa hotuba ya Rais na ninakubaliana nao kwamba itatusaidia sana kuleta umeme wa kudumu. Wizara ya Maji na Nishati si Wizara ya Muungano, lakini katika ukurasa wa 128 wa katiba yetu ya Jamhuri kwenye nyongeza ya kwanza suala la gesi na mafuta ni suala la Muungano kwa hivyo hapo utata wa katiba upo. Lakini hata hivyo kwa vile tunailinda na kuitetea katiba ninashauri Unguja na Pemba yako mafuta na huko *Mnazi Bay* iko gesi ningeshauri gesi hiyo kwanza ………..

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. (*Makofi*)

**MHE. MWANNE E. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwa kushukuru wapiga kura wangu Nawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Tabora kwa kuwa na imani kubwa na mimi kunirejesha tena Bungeni kwa vipindi viwili nawashukuru sana na ninaahidi mbele yako nitaendelea kuwapa ushirikiano kama nilioanza tangu mwaka 2000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi alioupata ambao historia yake haijawahi kutokea, nampongeza sana. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na Rais pia kupigiwa kura nyingi sana na Bunge lako Tukufu kwa ushindi alioupata wa asilimia takriban 98. Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza wewe pamoja na Mheshimiwa Spika, kwa ushindi mlioupata muda hautoshi nitakwenda haraka haraka nawapongeza sana. Lakini pia nichukue nafasi ya pekee kuwapongeza wenzangu Wabunge wenzetu na wananchi wa Zanzibar kwa ushindi waliouonyesha na kutuonyesha njia Watanzania Bara hatimaye tukashinda. Kazi

walioifanya ilikuwa ni nzuri sana kura ni za uhakika nampongeza Rais Amani Abeid Karume. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo pia naomba niwapongeze Mawaziri wote walioteuliwa na Manaibu wake, Wakuu wa Mikoa pamoja na Wabunge wenyewe tujipongeze pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo nianze moja kwa moja kwa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais iliyowasilishwa mbele ya Bunge hili Tukufu na Waziri Mkuu. Moja kwa moja nianze kwa kuchangia suala zima la afya, ukurasa wa 43 umeeleza jinsi gani Rais anakaleketwa au ana uchungu na suala zima la afya. Sasa mimi niende moja kwa moja kuhusu Vituo vya Afya na Zahanati zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wanawahamasisha wananchi kujitolea kwa nguvu zao wajenge zahanati wananchi wakajenga zahanati nyingi sana na Vituo vya Afya ni vingi sana. Lakini kwa bahati mbaya sehemu nyingi ingawaje nitazungumzia kidogo kwa upande wa Tabora Wilaya ya Urambo, kuna zahanati ambazo zimejengwa tangu mwaka 2000 zahanati 23.

Mpaka leo wanalala popo, mpaka leo hakuna kazi yoyote inayofanyika wananchi wanateseka sana, wakina mama wajawazito wanafia njiani pamoja na watoto wadogo kwa sababu huduma ziko mbalimbali sana kutoka kituo kimoja na kingine inawezekana tatizo hili ninalolizungumzia pia ni Tanzania nzima kuna matatizo kama haya ya Vituo vya Afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niende haraka haraka ukurasa wa 48 Mheshimiwa Rais amezungumzia katika hotuba yake suala zima la mazingira. Mazingira ni tatizo kubwa sana kwa wananchi wetu.

Kwanza uelewa wa ukataji miti sasa hivi bado haujazingatiwa na watendaji wetu ambao wanasimamia kwenye maeneo hayo kwa kweli wanashindwa kwa sababu umbali waliokuwa nao, Mwenyekiti wa Kijiji hawezi kuzungukia mazingira yote kwa sababu wale wanaokwenda kuomba kuhamia kwenye maeneo yao wanamuomba Mwenyekiti wa Kijiji anawaruhusu lakini bila kuongozana naye au kufuata kwamba huyu anayekwenda anampimia eneo gani.

Kwa hiyo anaruhusiwa kwenda akachague eneo analotaka kwa hiyo anakata miti akishamaliza kukata anaondoka kama hapamfai au hata kama mwaka mmoja atahama.

Kwa hiyo nilikuwa naiomba Serikali ningeishauri ikiwezekana hawa watendaji wapewe nyenzo za kufanyia kazi. Sisi wenyewe Wabunge wa Majimbo, umbali wa Jimbo moja ni kama hapa na Morogoro Jimbo moja, mbunge anatakiwa kwenda kule. Kwa hiyo sasa huyu mtendaji ataweza? Nilikuwa naomba Serikali iangalie jinsi gani ya kuwawezesha hawa watendaji, lakini pia leo asubuhi wakati Mheshimiwa Waziri anajibu swali la nyongeza kuhusu Wilaya kulikuwa na tatizo, amejibu sawa kwamba Serikali haina fedha.

Je, kwa nini Serikali isiongeze Tarafa, ingeongeza ukubwa wa Tarafa ili angalau kama Jimbo moja lina Tarafa mbili basi angeweza kurekebisha zikawa hata Tarafa nne ili wananchi waweze kufikiwa kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nizungumzie suala zima la Mahakama za Mwanzo. Mahakama za Mwanzo hawana vitendea kazi vya kisasa ndio maana wanachelewesha kesi. Mahakama za sasa hivi pia hazina umeme, atafanyaje kazi ili aweze kutoa hukumu inayotakiwa na kutoa nakala kwa haraka? Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie hizi Mahakama kuwawezesha ili angalau waondokane na matamanio lakini kama hawatawezeshwa na kama hawataangaliwa itakuwa ni tatizo kubwa kukemea suala zima la rushwa.

Pia nizungumzie Mfuko wa Serikali wa Sayansi na Teknolojia hususani kwa wanafunzi. Wanafunzi wanashindwa kukopa kwenye mfuko huu kutokana na masharti magumu yaliyokuwepo. Bodi yenyewe haijazingatia masharti ya hati. Hati kwa mwanafunzi wa kijijini kuipata mpaka aje kusoma sio rahisi. Ningeomba na ningeshauri Serikali iwasaidie njia nyingine ya uhakika ili angalau hawa wanafunzi wa kutoka vijijini wasome. Kama ni matatizo ya vijijini hata mjini wako wengine hawana uwezo wa kuweza kuwasomesha. Kwa hiyo, naomba kama tunazingatia suala zima la wanafunzi ili waweze kupata elimu ya juu ni vema Serikali ikaangalia upya suala hili la mikopo. Nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri alivyoweza kutufafanulia hapo juzi lakini pia nimpongeze na nimhakikishie kwamba tutampa ushirikiano ule atakaohitaji sisi Wabunge tumsaidie lakini kwa kurekebisha bodi hili suala la dhamana ya wanafunzi, ni tatizo Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Waziri nadhani unanisikia naomba tuwasaidie hawa vijana maskini wa vijijini ili angalau waweze nao kuingia kwenye mafunzo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda pia kuzungumzia suala dogo tu la makambi ya wazee. Kuna wazee ambao ni wagonjwa wa UKIMWI. Hawa watu wana matatizo wametengwa sasa kwa njia hii hatujui wamefikia wapi. Naomba Wizara ya Kazi iangalie pia haya makundi ya watu maalum hususani walemavu watawasaidia vipi. Hili ni tatizo kubwa kwa sababu wao hawawezi kwenda kuomba mahali popote na hawawezi kupata sauti nyingine zaidi ya Wabunge wao ambao tunawatetea ili kuwe na fungu maalum la hili suala la njaa waweze kusaidiwa kama walemavu kupitia vikundi vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa heshima na taadhima, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa asilimia mia kwa mia, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. SAID JUMA NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nazungumza kwa mara ya kwanza, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Sikonge, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi mkubwa alioupata wa kuongoza nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimpongeze Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa ushindi mkubwa alioupata. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kupata kura nyingi za Waheshimiwa Wabunge na za kishindo. Nimpongeze Mheshimiwa Spika na nikupongeze wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kupata nafasi ya kuongoza Bunge letu kwa kipindi cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikishukuru Chama changu na wananchi wa Jimbo la Sikonge kwa kunirudisha tena Bungeni kwa awamu nyingine ya pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imezungumzia mambo mengi. Kwa ujumla naipongeza. Hotuba hii inatoa dira ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi kwa viongozi wa kuchaguliwa, kwa watendaji wa Serikali na kwa wananchi wote mwelekeo ukiwa wa kutuletea maendeleo sisi wananchi wa Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nijikite kwa mambo machache tu. Kwanza, nataka nizungumzie kidogo suala la kilimo. Naipitiapitia Ilani ya Uchaguzi, yako maelezo mengi yaliyotolewa kama ahadi za Chama chetu lakini kwa ujumla kilimo chetu bado ni duni. Wakulima wengi bado hawajaanza kutumia kanuni bora za kilimo. Lakini inawezekana hawafanyi hivyo kwa makusudi bado yako matatizo. Matatizo ya msingi ambayo kama hatukuyatafutia ufumbuzi bado wananchi wetu wanaweza kuendeleza kulima hivi miaka hadi miaka.

La kwanza, wataalam hawapo vijijini na inawezekana kutokana na uchache wao. Mimi nashangaa sana unakuta Bwana Shamba mmoja ana Kata mbili. Akianza kuwatembelea wakulima mwanzo wa mvua, mwisho wa mvua ndio akafika kijiji cha mwisho. Wakulima wanahitaji wataalam lakini wataalam tulionao kwa kweli ni wachache. Serikali naomba iliangalie hili katika utekelezaji wa Ilani yetu ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile Mabwana Shamba wale wa zamani walikuwa na maeneo yao ya kuonyesha mfano. Unafika unaona shamba la Bwana Shamba au Bibi Shamba amelima kwa mfano wananchi wanafika pale wanaiga. Leo hii naweza kulima vizuri zaidi kuliko Bwana Shamba. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Kweli kabisa. (*Makofi*)

**MHE. SAID JUMA NKUMBA:** Sasa hatutaki Ubwana Shamba wa kusoma vitabuni tunataka Ubwana Shamba wa vitendo shambani na unaweza ukapita ukakagua hata Bwana Shamba yuko amekaa mjini hana shamba hata la mfano. Kwa hiyo, haya ni mambo ya msingi ya kuangalia. Sasa nikizungumza hapa Mabwana Shamba maana yake na sisi viongozi lazima tuwe na mashamba ya mfano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni pembejeo ziko juu sana. Mimi ninaposikia hapa habari ya Serikali kutoa ruzuku ni mchezo. Hivi ruzuku Serikali inatoa ya Sh.3,000? Ruzuku ya pembejeo kwa kweli bado labda kwenye hii Ilani ya Uchaguzi

ya kipindi hiki. Mkulima ananunua mfuko wa mbolea zaidi ya Sh.20,000 maana yake kama anataka kuzalisha vizuri anahitaji mifuko miwili ya mbolea zaidi ya Sh.40,000.

Kwa mwanachi wa kawaida kijijini anazipata wapi fedha hizi na ni kwa ekari moja? Bado dawa za kuulia wadudu hajatafuta bado mbolea ya kupandia hajatafuta bado nguvu kazi ya uzalishaji. Haya yote ni mambo ambayo kwa kweli ni vikwazo vya maendeleo kwa wakulima wetu. Sasa huwezi ukapata ufanisi wa kilimo kama pembejeo bado ziko juu kiasi hiki.

Naiomba Serikali kwa kweli pamoja na maelekezo mazuri ya Mheshimiwa Rais itafute utaratibu wa kupunguza gharama za mbolea aidha kwa kuanzisha viwanda vyetu hapa nchini au kwa kununua mbolea kutoka nchi za nje na kutoa ruzuku kubwa ambayo itawafanya wakulima waweze kununua kwa bei ya chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mazao ya biashara kama tumbaku maana kwetu ukisimama hapa unazungumza halafu husemi tumbaku bado hujaonekana umefanya kazi. Kwa mazao kama tumbuku kwa Mkoa wa Tabora lengo liwe kuwaendeleza wakulima wa mazao haya ya biashara. Leo wakulima wa tumbaku wa Tabora wanalima kwa mikopo. Tumepata janga la ukame lakini pamoja na ukame huu makampuni ya tumbaku yaliyowakopesha wakulima bado yataendelea kuwakata hawa wakulima fedha kwa asilimia mia moja. Huku si kuwaendeleza wakulima ni kuwakandamiza wakulima, ni kuwanyonya wakulima. Ikifika mahali kuna tatizo limejitokeza ambalo mkulima hakulitarajia wala kampuni haikulitarajia tugawane basi hasara hii. Kwa hiyo, hili nalo naliomba sana kwa wakulima wetu hasa wa zao hili la tumbaku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zetu za Mkoa wa Tabora zimesahaulika sana. Wale watu wanaotaka kujifunza udereva ni vizuri ukaanzia kujifunza udereva kwenye maeneo ya Tabora ili ukija huku usipate tatizo lakini ukijifunza kuendesha gari Dar es Salaam ama hapa barabara za Dodoma ukienda kule unaweza ukapata taabu sana unaweza ukanyang’anywa hata leseni. Barabara za kule ni mbaya. Naiomba sana Serikali katika kipindi hiki, tumeahidi lakini kuna barabara ya kutoka Nzega - Tabora – Sikonge – Ipole – Rungwa haipitiki na ndio barabara inayotuunganisha na wenzetu wa Tarafa ya Kiwele na wenzetu wa Mkoa wa Mbeya. Barabara toka Ipole – Koga – Mpanda haipitiki. Barabara ya kutoka Itigi – Tabora – Urambo – Kaliua- Kigoma, haipaitiki. (*Makofi*)

Sasa niwaombe sana Mheshimiwa wa Miundombinu tena bahati nzuri Mheshimiwa aliyepita alikuwa mtu wa takwimu wa barabara na Mheshimiwa Mramba mtu wa takwimu, tusaidiane hapa barabara zetu zitengenezwe. Kama hatuwezi kutengeneza barabara Mkoa wa Tabora utabaki kisiwani haufunguki. Tunataka tutembee na sisi mpaka Ukerewe tufike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ilitengewa fedha ya kutoka Ipole – Rungwa, mkandarasi mmoja anaitwa *Badri East Africa* akafanya kazi chini ya kiwango akafutiwa mkataba. Toka afutiwe mkataba mpaka leo Serikali imekaa kimya wananchi hili imekuwa ni kero kubwa sana. Naiomba Serikali ifuatilie ili kuhakikisha kwamba

anapatikana kandarasi mwingine aweze kutusaidia kumaliza tatizo hili la barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la njaa. Jambo hili ni janga la nchi nzima. Hakuna mahali palipo salama kwenye tatizo hili la njaa. Mimi binafasi nampongeza sana Mheshimiwa Kikwete na Serikali yote pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ambayo sasa hivi wanaifanya ya kuhakikisha Watanzania hawapati tatizo na adha kubwa kwa ajili ya kuwapalekea chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa natoa tahadhari. Kunapotekea matatizo au majanga ya namna hii kuna watu hupitia majanga haya kujinufaisha.

**MBUNGE FULANI:** Haswa!

**MHE. SAID JUMA NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi jioni hii ili nichangie hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile hii ni mara yangu ya mwazo, sina budi niwatolee shukrani wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Muyuni, Unguja kwa uamuzi wao wa kunichagua tena kuja hapa mbele ya Bunge letu hili Tukufu ili na mimi nipate kushiriki katika michango mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hayo, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Kikwete, Mheshimiwa Rais Karume, Makamu wa Rais Dr. Shein, pamoja na Mheshimiwa Spika na wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa kwa wakati huu ili kuja kuliongoza Taifa hili la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyokuwa mbele yetu hapa ni hoja ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini jambo la kusikitisha ni kwamba hotuba hii imekuwa sasa ni kivuli na chaka la baadhi ya wenzetu kuja hapa kujilabu kwa njia ambazo hazina msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo ambalo wajumbe wenzetu hapa wamelizungumzia. Ni kitu cha kushangaza sana kwamba leo mtu anayeitwa kiongozi, mzaliwa wa Zanzibar, Unguja na Pemba na anakuja mbele ya Bunge hili Tukufu na kusema kwamba eti Zanzibar hakuna maendeleo na Kisiwa cha Pemba kimetupwa, hivi hapa ukweli uko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sana ndugu zetu hawa waliokuwa na *concept* hizi wakae wazingatie. Waangalie historia. Zanzibar imetawaliwa kwa miaka na miaka na miaka nenda na utawala wa mwisho wa Zanzibar ulikuwa ni mtiririko wa utawala wa Kisultani. Hebu tuangalie katika utawala wote huu wa Masultani waliopita ni Sultani gani alijenga angalau kibanda tu katika kisiwa cha Pemba. Akaamua tu kwamba

leo mimi nimekwenda Pemba nikifika nikapumzike katika nyumba ya Pemba, ni yupi? Alikuwa akifika kwenye meli akawaone wananchi wake halafu anarudi analala kwenye meli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mapinduzi haya leo kisiwa cha Pemba kinang'ara, kisiwa cha Pemba kina viongozi wa kila pembe. Hawa hawa watu wa kisiwa cha Pemba wamefikia viwango vya juu kabisa na katika kufikia pale tuliona jinsi gani walituongoza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo mtu anakuja mbele ya Bunge hili Tukufu anasikitika na kusema kwamba eti Rais wa Zanzibar hamchagui kiongozi kutoka Pemba. Sasa leo unamchagua kiongozi kwa madhumuni gani, si aje akusaidie, ikiwa kama mtu hayuko tayari kukusaidia, hamwendi sambamba unamchagua wa nini? Lazima kuwe na mantiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningewashauri tu ndugu zangu hawa waliokuwa na malalamiko haya, wajaribu, wakubali hali halisi ilivyo. Leo tumemaliza uchaguzi juzi tu na wanatangaza ulimwengu mzima kwamba hawaitambui Serikali ya Zanzibar. Sasa unategemea mtu humtambui aje akuchague? Atakusaidia nini? Hakusaidii hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya siasa ya Unguja na Pemba ni hali ya kihistoria. Nafikiri wenzetu pengine hapa Tanzania Bara mlikuwa kidogo hamyajui, nashukuru sana kwamba sasa hivi mnaanza kuelewa. Kule Pemba toka enzi tunazotoka kulikuwa na usemi mmoja wanasema "Waarabu wa Pemba wanajuana kwa vilemba na Pemba peremba ukienda na joho utarudi na kilemba". Huu ni usemi toka mimi sijazaliwa. Kwa hiyo hii *attitude* ya ulalamishi ni ya kihistoria. Tuitazame penye uwezekano tufanye kila linalowezekana ili kuweza kuyatatua lakini siwezi nikasema hapa kwamba Wapemba wanaonewa kwa tofauti ya Unguja na Pemba kwa sababu wao hapewi fursa, hawapewi kila nafasi, sio kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, kuna mjumbe mmoja alisimama hapa akasema kwamba eti Pemba hakuna barabara nzuri. Jamani hii ni kweli na eti lami inapigwa risasi na Askari wa Jeshi la Zanzibar. Hivi kuna Serikali gani itoe hela yake inunue lami halafu ipoteze. Hata hivyo leo hebu watu waondoke waende Pemba, mimi natoka Unguja lakini nalia wivu kwa barabara zilizoko Pemba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningewaomba sana wenzangu hawa waipitie Sera ya Chama cha Mapinduzi waone inasema nini zaidi ya hizo barabara zilizotengenezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kuna barabara ngapi ambazo ziko kwenye mtandao wa kutaka kutengenezwa. Tuachilie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna malalamiko kusema kwamba wanaonewa, Visiwani Majeshi yanaingia kwenye vijiji na kuwapiga watu. Jamani hebu kama kweli tunazungumza ukweli mbele ya Bunge hili hebu tutafute nini chanzo na sababu za hayo

kutokea. Wamesahau kwamba kuna kijana mmoja kule Zanzibar ambaye alikuwa anaitwa marehemu Chande Salehe Sadala.

Kijana huyu alikuwa anatoka Jimbo la Magogoni, sehemu ya Mwera. Kijana huyu walimchinja kinyama hawa hawa wanaosema hivi. Wakatiwa mikononi mwa sheria watu sita kwa ushahidi kamili wa Serikali na hawa wote sasa hivi kutokana na siasa na utawala bora na haki hizo wanazosema za kibinadamu wako nje. Jamani hii haki ya kibinadamu iwe kwa wa Pemba tu wa Unguja hawana haki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tuwe na muda sana wa kuichangia hotuba hii lakini kutokana na hali halisi ilivyo tunashindwa kuingia ndani ya hotuba kwa sababu naona wenzetu hawako tayari kuichangia hotuba ila ni kujaribu kutafuta njia na suluhisho la matatizo na kujitetea kusikokuwa na maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu.

Kwanza kabisa naomba nitoe pongezi za dhati, lakini sitazitoa kwa urefu ule unaostahili. Naomba tu mnielewe kwamba kwa sababu ya muda nimpongeze Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na wengine wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nitoe shukrani za dhati kwa wananchi wa Masasi kwa kunichagua kwa kipindi cha pili kwa kura nyingi kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejifunza jambo moja kwamba unaporudia kipindi cha pili au cha tatu panakuwa na kazi sana wewe kukubaliwa na wananchi lakini nashukuru hayo nimeyafanya kwa kishindo, nashukuru Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais ni dira na mtazamo mpya wenye ari, nguvu na kasi mpya kwa ajili ya maendeleo yetu wote Watanzania. Mengi aliyoyasema ni ahadi na alisema kwamba atahakikisha kwamba hawaangushi wananchi na kwa kupitia Bunge hili sisi tunaojadili hotuba yake tu namhakikishia kwamba hatutamwangusha Rais, na wala sisi Wabunge hatutawaangusha wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza maoni na mapendekezo mengi kutoka kwa Wabunge wenzangu kwa kweli mimi nimeridhika na michango mingi iliyotolewa. Lakini labda nichukue kipindi hiki tu kuibua mambo mbalimbali yanayohusu Mikoa ya Kusini au *Mtwara Corridor* ambayo naona mengi bado hayajafika mezani.

Kwanza kabisa, nataka kusema kwa dhati wakati umefika wa kuendeleza Mikoa ya Kusini, na tuhakikishe kwamba Awamu hii ya Nne ndio inakuja kuleta maendeleo

haya. Awamu zilizopita zimejitahidi kujenga barabara Dar es Salaam – Kibiti – Lindi – Mingoyo.

Wengi tulikuwa tumetegemea kwamba ile barabara ingekuwa imekamilika mwezi Juni mwaka huu. Lakini nasikitika kusema na kwa bahati mbaya wenyewe wahusika siwaoni humu ndani lakini nataka kuwaeleza kwamba tafadhalini Waziri na Naibu Waziri ebu fungeni safari muende Lindi kwa barabara ili muone je hii barabara kweli itakamilika ifikapo mwezi Desemba mwaka huu? Jawabu itakuwa haiwezekani. Ukienda sehemu ya Nangurukuru – Lindi – Mingoyo kwa kweli Serikali iko haja ya kusema na kuwaeleza wananchi je, ahadi yake ya kumaliza barabara hii tarehe 30/12 kweli itawezekana na kama haiwezekani, kulikoni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pale yupo Mkandarasi Mwarabu wa Kuwait anakwenda taratibu, taratibu utafikiri ngamia jangwani. Kwa hiyo, katika eneo hili hapapitiki hata kidogo na wakati huu kama mvua ikija ya kutosha ile barabara itajifunga. Ndio maana nasema Mawaziri hebu nendeni mkaone. Je, ile ahadi itakamilika? Jamani chonde, kamilisheni ujenzi ili tusije tukamwaibisha Rais wetu kwani ameshawaahidi watu wa Kusini kwamba barabara ya lami mpaka Mwanza mwezi Desemba mwenendo ama *speed* ya ujenzi inbakatisha tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nataka kuchangia ni kwamba kwa bahati nzuri sasa imekwishaanza kuonekana kuwa Kusini ni Mikoa tajiri kuliko Mikoa yote Tanzania na nitawaeleza. Kuna mabonde ya ajabu ya kulima ambayo hayajaguswa. Ukitoka Ruvuma, fika Matandu, uende Lukuledi, mabonde mazuri tu unaweza kulima kila zao. Lakini wapi teknolojia ya kulima, hakuna, wapi kilimo cha umwagiliaji, hakuna. Sisi tunashangaa fedha zinatumika katika mito, vijito, mifereji midogo midogo vinavyomwagilia wakati wa tu wakati maji yako mengi unaweza kutumia mwaka mzima. Wizara ya Kilimo, chonde hebu vamieni Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, suala la umeme. Hivi sasa tumeshaanza kuwaonyesha kwamba umeme hatuwezi kutegemea maji ya Mtera na Kidatu tu si tumeona sasa yanakauka. Hivi mnategemea nini sasa, si Songosongo? Songosongo inaleta gesi hapa na ni tegemeo kubwa katika kuzalisha umeme hata jana Mheshimiwa Rais amesema tutanunua majenereta zaidi ili kuhakikisha umeme unakuwa mwingi. Sasa umeme ule unatoka wapi? Songosongo, Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachosema sisi ile ya Songosongo tumewapeni huko Dar es Salaam lakini ile gesi ya *Mnazi Bay* ambayo ndilo tegemeo la Kusini. Mredi wake unakwenda taratibu mno. Sisi tulitegemea mpaka mwezi Mei mwaka huu tutakuwa na umeme wa gesi lakini mpaka sasa bado.

Sasa hebu tuelezeni huko *front-desk* haya mambo yatakamilika lini na umeme utakwenda lini Tandahimba, Masasi? Tunataka kuona unakwenda lini Tunduru na Songea. Sisi hatujui kama ni kampuni ya Canada ya *ATOMAS* au *TANESCO* ndiyo watakaosambaza umeme vijijini lakini nakuambieni gesi ipo nyingi na kwa mujibu wa utafiti imeonekana kuna *1 trillion cubic metres* ni nyingi mno unaweza kutumika kwa

miaka 100 ijayo. Ndiyo maana nawaambieni kwa kweli Kusini kitakuwa kitovu kikubwa cha maendeleo. umeme hapo, mabonde hayo, korosho eeh! Kila kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie utalii kwa kweli sasa hivi kuna maeneo makubwa ya Seluu, Msangesi, Fukwe za Mtwara na Lindi, Kilwa ambako kuna maeneo ya Kale watalii ndiyo wanataka sana kuja na niwaelezeni utalii umezidi sana katika miaka hii ya karibuni lakini sasa kinachotuangusha ni *Air Tanzania* sasa hivi iko *Intensive Care Unit* yaani iko hoi hata wiki hii katika shughuli za urembo wa *Miss Utalii,* sijui nani atakayewapeleka Arusha na Ngorongoro kwa sababu hali ya ndege yetu iko hoi hebu Wizara yetu ya Miundombinu saidia hapo ili kuhakikisha kwamba utalii unafanikiwa nchini.

Kwa kuwa kengele imeshagonga naomba tu kusema kwamba Kusini, Kusini, Kusini, ndiyo tegemeo kubwa la uchumi wa Tanzania kwa miaka ijayo.

Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, alitakiwa kusema yeye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii. Kwa hiyo namuita Mheshimiwa Haji Juma Sereweji halafu ajiandae Mheshimiwa Keenja halafu ajiande Mheshimiwa Dr. Wanyacha.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu ili niwe mmojawapo wa kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema kweli hii hotuba ni nzuri na ninaipongeza na vile vile naipongeza hasa kwa alivyotusomea, kama unatokea utasema hasomi lakini alikuwa anasoma na yale aliyoyaeleza kwa ufasaha ambayo alikuwa hayasomi moja kwa moja tulipotazama ndani ya kitabu hicho yote yamo kwa hilo tunamsifu.

Lakini vilevile nimpe pongezi Rais wa Jamhuri ya Muungano pamoja na Makamu wake kwa kupata ushindi wa kishindo, nimpe pongezi Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa kupata ushindi wa kishindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpe pongezi Spika wa Bunge pamoja na wewe kwa kukalia kiti hicho kwa ushindi mkubwa, lakini nisiwasahau wananchi wangu wapiga kura wa Jimbo la Mwanakwerekwe kwa kunichagua kwa ushindi huu. Nimefurahi kwamba kila chumba nilichoingia siku ya hesabu Mimi na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete tulikuwa tunaongoza, jambo ambalo liliwafanya Wapinzani wote waondoke na kukimbia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba utusamehe leo Wazanzibar wote, na hii ni mojawapo imo katika hotuba ya Rais. Watanzania Bara mnauliza Zanzibar kuna nini lakini tunachowaambieni ni kwamba kuna Chama cha *CUF* kinachotaka kutawala kwa mabavu na hawana ubavu. Kuna viongozi wa juu wa Chama cha *CUF* wanatoka Tanzania Bara wakija Zanzibar wakisimama juu ya majukwaa wanahubiri maneno ya kuwachochea wafuasi wao na baada ya kumaliza tu wafuasi hao huwa wanaingia mitaani na kuanza fujo, kuwapiga wanamaskani wa Chama cha Mapinduzi, kuwapiga watu wasio

na hatia sasa polisi kama wanachukua mkondo wa kuzuia mambo maovu hayo hapo *CUF* wanalalamika ati kuna Haki za Binadamu, natumai hakuna dola hata moja itakayokaa kuna vitendo vichafu kama vile wanyamaze tu hamna na kama hoja yao kubwa kwamba haki za binadamu iletwe kwenye Demokrasia halafu wafanye fujo. Ng'o! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema kweli wallah! *CUF* waushukuru Muungano, washukuru sera za Chama cha Mapinduzi za amani na utulivu ambazo ndizo tunazokwenda nazo na Chama cha Mapinduzi kama Chama cha Mapinduzi hatujathubutu kuondoka na kufanya fujo au kuwafanyia fujo lakini kama tutafanya hivyo tunahakikisha *CUF* wa Pemba haki, Unguja hakai hata mmoja na hatujafikia hivyo na hatutofikia hivyo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninavyosema kwamba Zanzibar, Unguja na Pemba, Pemba wako watu wazuri tu ambao wanachama wa Chama cha Mapinduzi lakini vilevile hawatakiwi na *CUF* wanafukuzwa wale walio wa Chama cha Mapinduzi ambao wana jamii ya Kipemba wanawafukuza wakifa hawawaziki. Mbona hawayasemi na hayo? Wayaseme na hayo vile vile. Kunako daftari la wapiga kura ndani ya Jimbo langu Ndugu Chande wamemuua kwa kuwa alikuwa wakala na wakamzika halafu wakapiga tuta wakapanda mhogo juu yake Mungu akawafedhehi wakaonekana na wakakamatwa na simu ya marehemu watendaji wa vitendo hivyo.

Lakini vilevile wamemuua kijana mbichi kabisa askari wa KMKM Pemba Mungu akawafedhehi kwa muda wa siku 14 hakuoza akaonekana, baada ya kuonekana tu wakasema lahaulah! kumbe Mpemba Mwenzetu. Tunakwenda wapi? Halafu wanakaa hapa wanasema ooh! Sijui tunachokozwa, tarehe 28/10/2005 kunako kampeni za mwisho mwisho kabisa Chama cha Mapinduzi kilifanya kampeni yake Kaskazini, Unguja na wao wakaenda sehemu za Paje Kusini lakini *CUF* walivunja mkutano wao mapema kila gari walichukua mawe, makonokono, virungu na kila kitu na wakawapiga Ndugu wa Chama cha Mapinduzi kiasi cha watu 50 walijeruhiwa. Chama cha Mapinduzi tufanye nini? Polisi wafanye nini? Kweli dola kama dola ikae tu? Lakini vilevile kuna usemi usemao kwamba kiongozi yeyote asiyedhibiti maasi, uhalifu naye anashiriki, kwa hiyo Jamhuri ya Muungano walidhibiti hawataki kushiriki kwenye maasi hayo ndiyo maana dola ikachukua mkondo wake. (*Makofi*)

Hapa nimeletewa historia ya kiajabu kabisa, Mheshimiwa mmoja wa upinzani wa CUF anasema kwamba 1960 eti ZNP walikuwa wameshatawala, 1960 ZNP walikuwa bado hawajatawala na ndiyo maana askari wakachukuliwa kutoka Scotland kuja kufanya upelelezi kwa sababu mfalme alikuwa chini ya himaya ya Askari Jeshi la Uingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa ni kwamba ningependelea viongozi Bungeni wakija waseme ukweli wasithubutu kusema maneno ya kupotosha kwa ufahamu wangu nitasema hivi kwamba tumeambiwa Pemba hakuna Mkuu wa Mkoa hata mmoja mzaliwa wa Pemba lakini yuko Ndugu yetu Dadi Faki Dadi amezaliwa Pemba Wingwi lakini kuna Ndugu yetu Mwajuma yeye ni Mkuu wa Wilaya Mkoani halafu kuna Ndugu

Jabu Khamis Mkuu wa Wilaya Chake halafu kuna Ndugu Isa Ali Isa Mkuu wa Wilaya ya Wete halafu kuna Ndugu yetu Hasnuu ameteuliwa na Rais awe Mwakilishi wa Balaza la Wawakilishi Zanzibar. Vile vile kuna askari wetu mmoja anaitwa Ndugu Ayoub aliyekuwa Kamanda Mkuu wa Vikosi Pemba ambaye walimpiga kisu alikuwa Mpemba na kazi ilikuwa Pemba. (*Makofi*)

La mwisho ninalolisema *RPC* pamoja na Kamishna kwa Katiba yetu hatoki Zanzibar, hatoki Morogoro wala hatoki Kigoma anatoka kwenye Jamhuri ya Muungano na yule ni kikosi cha Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano kwa hiyo hata atoke Pemba tutajua yeye anatoka katika Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Mungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo labda wakati umekwisha niseme naiunga mkono Hotuba hii mia kwa mia .

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii na pili kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza na mimi nijiunge na wenzangu kuanza na shukrani na pongezi.

Kwanza nimpongeze Rais wa Jamhuri Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Makamu wa Rais kwa ushindi wa kishindo walioupata. Naomba nimpongeze pia Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Aman Abeid Karume kwa ushindi alioupata na wanasema dalili njema huonekana mapema alitusaidia kuonyesha hali ingekuwaje katika uchaguzi mkuu uliopita. (*Makofi*)

Naomba niungane na Mheshimiwa Paul Kimiti kumshukuru sana Mama Salma Kikwete na mgombea urais na mwenza wake kwa jinsi walivyotuombea kura kwa wapiga kura na wapuga kura kweli wakasikia wakatupa kura nyingi sana.

Nachukua nafasi hii kuwapongeza Wabunge wenzangu wote waliopita na kuingia katika Bunge hili kwa njia mbalimbali hongereni sana kazi ilikuwa ngumu lakini mliimudu basi tuanze kujianda na kwamba 2010.

Nawapongeza wenzetu waliopata uwaziri, Naibu Waziri, Ukuu wa Mikoa na Ukatibu Mkuu kwa nafasi hizo walizopewa na ninaomba niwahakikishie kwamba Wabunge watawapa ushirikiano pale watakapouhitaji na kwa viwango watakavyohitaji na wao watupe ushirikiano kule majimboni ili mambo yaende vizuri itakapofika mwaka 2010.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii niwashukuru sana sana wananchi wangu wa jimbo la Ubunge, walinipigia kura 93,700 na ushee nyingi sana na ile *stadium* tunayoijenga haiwezi kuwaweka wote walionipigia kura, nawashukuru sana. Nilishinda kwenye kila Kata na karibu kwenye vituo vyote nawashukuru sana kwa imani waliyonipa na ninawahakikishia kwamba kazi imeshaanza tutashirikiana kuhakikisha kwamba tunaondoa kero zinazotusumbua na kupata maendeleo yale tunayoyahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye hotuba. Hii hotuba ni nzuri sana kila mtu anaikubali hata wapinzani wetu hata wale wasiotupenda wanakubali kwamba hii ni hotuba kabambe kabisa. Lakini uzuri wa hotuba hii itakuwa katika utekelezaji wake imeainisha kila jambo tunalotakiwa kulifanya, kila kero na imetoa dawa ya kutibu kila tatizo lililopo katika nchi hii. Rais amenishangaza kweli anavyoielewa nchi hii, hongera sana kwa hotuba yako nzuri sana.

Sasa tuungane basi tuache haya mambo ya ugonvi tuungane sasa tuwatumikie wananchi wetu kwa kufuata hii dira iliyowekwa na hii hotuba ya Rais, kama tukifanya hivyo kwamba 2010 wananchi watatuhukumu tena kuona ni nani aliyefanya vizuri na ni nani ambaye hakufanya vizuri. Katika hili naomba tuungane kwa sababu hatutofautiani katika kukubaliana kwamba hii ni hotuba nzuri.

Lakini Rais anasisitiza kwamba kila kero iandaliwe mipango endelevu ya kuitekeleza na hili naomba sana Serikali irudi sasa kuangalia sera, mikakati na mipango ya kutekeleza mikakati ambayo ilikwisha kuandaliwa katika awamu ya tatu irekebishe ilingane ilingane na hii Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya ambayo tunakwenda nayo sasa hivi. Kwa hiyo ningeomba hili lifanyiwe kazi haraka na mapema kabisa na kwa malengo hayo ya kuweka mipango ambayo ni endelevu maana kuna mambo mengi sana ambayo tumewahi kufanya ambayo yalifanyika mara moja halafu baada ya hapo hakuna.

Kuna sehemu matrekta yalipelekwa yalipokufa watu walitafuta *scrap vet* sasa hivi hakuna, wananchi wamerudi tena kwenye jembe hayo siyo maendeleo endelevu, maendeleo endelevu ni yale ambayo yanaonekana Bariadi ambako wanalima kwa matrekta na majembe ya kukokotwa na ng’ombe sehemu kama Singida, Iramba hasa kwa Mzee Msindai ambako wanalima asilimia zaidi ya 90 ya kilimo chao wanatumia maksai na matrekta, kijiji cha Hembahemba hapa Pandambili ambako mwaka jana peke yake walinunua matrekta 29 kuongezea mamia ya matrekta waliyokuwa nayo. Bila kushirikisha wananchi katika mipango tunayoandaa uendelevu tunaoutarajia hautakuwepo na pale ambapo wananchi wameshiriki kwa kweli kumekuwepo maendeleo mazuri sana. Naomba niliachie hapo nategemea wamenisikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi hii sasa hivi tuna *crisis* ya maji, tuna dharura kubwa sana ya maji na wataalamu wananitisha wananiambia kutokana na joto linaloongezeka duniani ziwa Victoria linaweza likakauka, wananiambia kwamba kina cha maji ya hayo maziwa makubwa kimeshuka katika kipindi hiki kina kimeshuka kwa hiyo maji yanapungua katika vile vianzio vya maji, sisi wa Dar es Salaam tunashtuka sana kwa sababu hata sasa kule Jimboni maji hakuna kwa hiyo ukituambia Mto Ruvu utakauka tunakochukua maji basi ni tishio kubwa kabisa.

Mheshimiwa Rais analizungumzia suala hili la uhifadhi wa mazingira kwamba litapewa umuhimu wa juu sana lakini naomba na sisi wote tulipe umuhimu wa juu kabisa. Ule upandaji wa miti siku ya kupanda miti Januari haifai kwa mikoa mingi ya nchi hii kwa hiyo kila mkoa ujiwekee siku ya kupanda miti ya mkoa ambayo itaoana na mazingira katika maeneo yake pia Milima ya Uluguru ya Morogoro tunaomba sana

ipandwe miti na ihifadhiwe ili kulinda chanzo hiki cha maji kinacholisha Jiji hili kubwa kuliko yote katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makao Makuu ya Wizara ya Maji yako Ubungo kwenye Jimbo langu, na Jimbo langu ndilo Jimbo lililikosa maji kuliko Majimbo mengine yote Dar es Salam, nimeshazungumza na Waziri ameniahidi kwamba atalivalia njuga na mimi nitahakikisha kwamba kwa kweli utalibebea mkoba mpaka maji yapatikane kule Jimboni na nimewaahidi wananchi kwamba moja ya mambo nitakayofuatilia kwa nguvu zangu zote ni suala hili la maji maana linahatarisha maisha ya akina mama wanaovuka mabarabara makubwa na ndoo cha maji kichwani, watoto wetu wanaovuka kwenda kufuata maji na kipindupindu sasa kimekuwa ugonjwa wa kudumu.

Mheshimiwa Rais anatuambia kwenye ukurasa wa 42 kwamba hii kero ya maji ndiyo kero *number one* na mimi nakubaliana naye, kwa hiyo Dar es Salaam tutafutiwe kianzio cha maji cha uhakika. Haya maji yanayopita na sisi tunachota mwaka kama huu wa ukame tuna hatari ya kuathirika vibaya sana watu wa Dar es Salaam. Kwa hiyo tunaomba Serikali ilitazame suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo ningetaka niligusie ni ajira ya vijana na uwezeshaji wa wafanyabiashara ndogondogo. Mwaka wa 1997 tulifanya sensa Dar es Salaam tukakuta tulikuwa na wafanyabiashara ndogondogo na vijana wasiokuwa na kazi zaidi ya 800,000, zaidi ya wakazi wa baadhi ya mikoa katika nchi hii walikuwa wameajiriwa katika biashara ndogondogo ama walikuwa hawana kazi.

Sasa tumeahidi kwamba tutahakikisha kwamba vijana hawa wanapatiwa ajira na wanawezeshwa kufanya shughuli zao kwa uhakika, naomba hiyo kazi ianze mapema na kwa Dar es Salaam tulishaanza. Tulianza wakati ule kwa kuorodhesha vijana wale na kuweka mipango ya kuwahudumia, naomba kazi hii irudie tena ili tuwatambue hawa na tutambue uwezo wao na vipaji na ujuzi walio nao ili tuangalie jinsi ya kuweza kuwasaidia. Naomba pia tuandae mpango wa kuwapatia mafunzo wale wanaohitaji mafunzo ya biashara, viwanda vidogovidogo na shughuli wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ni mfupi sana naomba hilo nalo niliachie hapo lakini nitaendelea kwa kweli kwa nguvu zangu zote kuhakikisha kwamba haya mambo tuliyoahidi yanatekelezwa, mikopo ile tuliyoiahidi kwa akina mama na ubora wa maisha kwa sisi sote unakwenda vizuri zaidi.

Elimu ya Sekondari. Tuliambiwa unaanza mpango wa MES ambao haujaanza, sisi wa Dar es Salaam tuko nyuma sana kwa Sekondari, tuko nyuma kwelikweli na kwa hiyo kuna mipango ambayo tumeamua kuchukua kwa dharura lakini tunaomba hivi fedha za MES zipatikane mapema zitusaidie kutupa nguvu ya kukamilisha mipango hii. Naipongeza sana ile mikoa inayosimama hapa na kuzungumza kwamba Wilaya ina Sekondari 29, ina sekondari kama 40, sisi katika Jimbo langu kuna Sekondari tatu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja Mkono naomba yatekelezwe. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Serengeti walionipa tena kura na kurudi mara ya pili katika hili Bunge.

Uchaguzi ulikuwa mgumu lakini kwa kweli wengi walisema nirudi na nimerudi na ninaahidi kwamba nitawatumikia kikamilifu na kutetea wananchi kama nilivyotetea kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika na wewe pia kwa kuchaguliwa kwa kura za kishindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura za kishindo na kuwa Rais wa awamu ya nne. Nichukue nafasi nimpongeze Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu na Rais wetu. Niwapongeze Mawaziri ambao wameteuliwa, Wakuu wa Mikoa na Makatibu Wakuu walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wetu kuongoza katika awamu hii ya nne.

Nichukue nafasi hii niwapongeze sana Wabunge wenzangu, kazi ilikuwa nzito na Mwenyezi Mungu amesaidia tumerudi kazi yetu iliyobaki ni kuwatumikia wananchi wetu waliotuchagua kwa moyo mmoja na ili tuweze kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kusema kwamba naunga mkono hoja.

Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna alivyotoa ile hotuba humu ndani ilifurahisha sana yeye hakusoma alikuwa akienda *point* kwa *point* anaelezea kwa kirefu kwa hiyo ilionyesha ni mtu mwenye uwezo mkubwa kwanza anajua matatizo ya nchi hiyo ilionyesha kabisa alivyoitoa ile hotuba, ilionyesha anafahamu matatizo na kwa kweli Mungu akitujalia basi tumepata Rais wa karne ya 21, ni bahati sana kupata Rais wa namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika mengi Mheshimiwa Rais aliyasema lakini kuna mambo ambayo ni lazima tuyazingatie ili tuendelee, kwanza ni lazima tuitikie ule wito wake wa Kasi Mpya , Nguvu Mpya na Ari Mpya huo siyo wimbo ni lazima muelewe Rais anasema nini. Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya wimbo anatuambia Watanzania amkeni tufanye kazi tuendeleze Taifa letu, tusimwachie yeye kwamba yeye anaweza kuendeleza hili Taifa. Sasa yeye ni kiongozi na sisi tumsaidie Wabunge, Wananchi, Mawaziri amkeni tujenge Taifa letu. Karne ya 21 kinachotiliwa mkakzo ni uchumi basi mambo mengine ya siasa nchi zilishapata uhuru watu tunajitawala hakuna tatizo tukilegalega kiuchumi tumekwisha. Mimi juzi nilikuwa Spain nilikwenda nchi nyingi tu lakini nikawa najiuliza hivi Mbingu wanayoisema huenda hizi nchi kule kwetu ni motoni na hapa ndiyo Mbinguni wanayoisema wenzetu wanaishi kweli bwana lakini sisi karne ya 21 ukashangaa unapopita unakuta bado tunaishi nyumba za nyasi, maji hatuna. Kwa hiyo,

Ndugu zangu ili tu-*catch up* lazima tufanye kazi kweli kweli na saa tunazofanya kazi sisi hapa Tanzania ni saa kama sita zinatakiwa ziongezwe watu tufanye kazi tuzalishe, uchumi ukuwe, vijana wapewe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu ambavyo tunatakiwa tuhakikishe kwamba vinafanyika ili tuweze kupata maendeleo, cha kwanza ni elimu. Sasa hivi tunapeleka asilimia kama 20 au 27 *Secondary School* sasa hivi karne ya 21 elimu ya darasa la 7 haijatosha mtu kusema amesoma tunataka watoto wote wafike *form four*, mtoto wa darasa la saba hawezi kufungua *internet* hata ile kufungua *computer* hajui hivi hii karne ya 21 kama hujui kufungua *computer* kweli una kisomo?

Kwa hiyo, tunataka elimu hakuna nchi duniani inayoitwa *Developed Country* wakati watu wake hawakusoma hata hizi nchi za kiarabu zenye mafuta mengi ni *Developing Country* tatizo pale ni watu hawana kisomo cha kutosha. Tunataka Tanzania tutoe *high quality education*, isiwe watu wanakwenda shuleni utashangaa kuna mwalimu mmoja au walimu wawili Sekondari hivi kweli unaamini na yako madarasa mpaka *form four* pale unaamini hiyo ni elimu inatolewa huko? Kwa hiyo, ni lazima tulitilie maanani na elimu tukishaipata watu watajua namna ya kuji-*package* na ku- *corp* na huu utandawazi.

Kingine ni kilimo. nchi yetu 80% wananchi wanategemea kilimo ukiangalia *budget* hata 1% haiendi kwenye kilimo. Sasa kama hii Sekta ndiyo inaajiri watu wengi hata asilimia 1% ya *budget* hawapewi utaendeleaje? Ninajua sasa watu wanasema tukanunue matrekta watu walimie, hiyo siyo *strategy* ya kuendeleza kilimo kitu cha kwanza nchi igawanywe kwenye *ecological zone*. Kama Dodoma ni lazima tujue ni zao gani linaweza kukua hapa, kule Same kila mwaka nikipita mahindi yanakufa na watu wanaendelea kulima kwa hiyo kinachotakiwa ni *very immediate* kama mawese na mawese mimi nimefanya utafiti Botswana na Namibia nchi za jangwa ambazo *varieties* zake ukizipanda ugali wake ni sawa sawa na mahindi lakini hapa tunakuwa na *varieties* ambazo siyo nzuri kwa hiyo watu wanakataa ugali wa *pile millets*

Lingine ili kilimo kiendelee ni lazima wataalamu watoke kule Temeke waende vijijini, ma-*degree* hote yamejaa Temeke, sasa kama wataalam wanakaa Temeke hawaendi vijijini wale wataendeleaje? Huko *district* kuna watu wamemaliza hata na *degree* lakini ukienda hata baiskeli hana. Kwa hiyo mkulima hajui apande lini, hajui atumie mbegu gani, hana mtu wa kumwelekeza lakini ili ufanikiwe unatakwa *divide your country* katika *ecological zone* ukiisha maliza ujue ni zao gani la kupanda pale utafute *varieties* ambazo zinatakiwa kuwa pale na hiyo inachukua kazi kweli kama viazi mringo unachukua *15 years* kupata *a good variety* halafu ukiisha maliza ni lazima tuhakikishe kwamba tuzibe milima hii tunayoiona *South Africa* imefanya hivyo, unatengeneza *man made lakes* maziwa yaliyotengenezwa yale maziwa ndiyo utakayotumia maji katika umwagiliaji bila umwagiliaji tunatwanga maji kwenye kinu. Hizi hela kama za MIKUKUTA nyingi zikiwepo zikawekwa mabwawa tukawa nayo makubwa ya kumwagilia wananchi wakaanza kulima tutapata faida kubwa sana tunaomba sana.

Baada ya hapo mbegu ziwepo siku hizi unasikia kwenye redio mbegu zinatoka Kenya, zinatangazwa mbegu za kitali zinatoka Kenya tulime hivi wataalam wetu wamekwenda wapi? Huwezi ukatumia mbegu iliyotengenezwa Kenya kupanda Tanzania. Mimi ni mtaalamu kazi yangu ndiyo hiyo niliyoisomea. Ukosefu tu wa kutafiti *the right variety* kwenye *right environment* umekwisha na watu wananunua pale Arusha mbegu wanakwenda kupanda kule Kondoa na ile mbegu ni ya Nyanda za Juu. Kwa hiyo, akiishapeleka pale kazi imekwisha hatapata chochote. Lakini *to fit your variety to the right environment*, *right soil and right rainfall*. Kama Mwalimu Nyerere alivyosema kilimo kimeanguka, wataalam wa kilimo hawaendi vijijini na hiyo ndiyo wanatakiwa kuwaelekeza watu.

Lingine ni rushwa, rushwa ni lazima ipigwe vita kwa nguvu zote kwa Kasi Mpya, Nguvu Mpya na Ari Mpya angalia Kenya ilivyokwisha. Ukicheza na rushwa daraja ambalo unatumia milioni 3 unaambiwa milioni 50 tutafika wapi, tukitumia hizi hela zetu kwa uangalifu zinatosha. Rushwa ipigwe vita. *(Makofi)*

Lingine ni utawala bora, bwana bila utawala bora hakuna huko vijijini kuna miunguwatu wanasumbua watu, tuhakikishe wameshughulikiwa haraka Mimi nimeona kule kwangu watu wamepigwa, wakanyang'anywa mali, wakati nafanya kampeni. Mtu anakwenda anapiga watu, tena wazee, anawanyang'anya mali mambo yamekwisha. Tukiendelea na mchezo huu bila kuwa na utawala bora hatuwezi kufika kokote.

Kuna kitu kingine ambacho kinanikera. Sasa hivi wataalam tunao wa kompyuta, halafu wanachukua miaka miwili ndio mahesabu yanaletwa hapa Bungeni. Katika *UN is one month*, sasa Tanzania tufanye *per six months*. Mtu aliiba hela, miaka miwili alishaondoka hata ukienda pale humkuti, unaleta hapa Bungeni unamdanganya nani? Mchezo wa kuleta mahesabu miaka miwili hapa ukome mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka miwili ni mingi wakati tuna wataalam wa kompyuta, zipo tunataka mahesabu angalau *per six months* tujue nani ameiba na Rais amesema huko kwa Wakuu, sio sisi Wabunge ndio tunaanza kusema mtu aliiba. Ni kiongozi huko huko anatakiwa aiambie Serikali, huyu ameiba ama ameita Polisi anamkamata. Kwa hiyo, tunaomba sana Taifa hili ni letu na tusipoliangalia litaangamia, tusiwaonee haya wahalifu na hakuna msamaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilishangaa, nilikaa nje miaka tisa, nilipokuja mtu anakuja kuniambia amekosea, ananiambia msamaha, umeiba hela za watu unaniambia hela hizi ni za shirika sio zangu, kama ungeniibia zangu mimi. Kwa hiyo, tunaomba tuwe *tough*. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Pili, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi za kishindo. Nampongeza pia Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchaguzi na kushinda kwa kishindo.

Lakini pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri na Wakuu wa Mikoa kwa uteuzi waliopewa, ni imani yetu kwamba watatufanyia kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza na habari ya njaa. Singida ni moja ya eneo ambalo lina njaa kubwa. Ile dhana ya kwamba baadhi ya Vijiji vina neema na Vijiji vingine havina neema na naona ile dhana imepitwa na wakati, sasa Vijiji vyote vinahitaji chakula na kwa sababu hiyo nina tatizo na *figures* ambazo zimeletwa kupitia ofisi ya Waziri Mkuu.

Katika Wilaya ya Singida Vijijini imeonyeshwa pale kwamba sisi tunahitaji tani chache ukilinganisha na Wilaya ya Manyoni na Wilaya ya Iramba. Singida Vijijini ndio wenye watu wengi zaidi kuliko Manyoni na Iramba lakini hapa *figures* zilizokuwa hapa zinaonyesha kwamba sisi watu wa Singida Vijijini ambao ndio wengi zaidi tunahitaji tani chache.

Tunaomba wahusika wa Ofisi ya Waziri Mkuu waziangalie upya *figures* hizo na mimi nitakuwa tayari kushirikiana nao baada ya kurudi Jimboni tuone *figure* sahihi zinapatikana. Njaa hii itupe funzo la kwamba tusitegemee mvua peke yake katika kupata chakula, lazima tufike mahali sasa tuangalie na maeneo mengine.

Tumeimba mara nyingi habari ya umwagiliaji, lakini hakuna kitu, tumezungumza habari ya uvunaji wa maji lakini hakuna kitu. Hayo mambo mawili kama tukiyakazania, kilimo cha umwagiliaji na watu wakafundishwa namna ya kuvuna maji mimi nadhani tunaweza tukanufaika, tukatumia vitu hivyo kwa ajili ya kilimo badala ya kutegemea mvua peke yake na majira sasa yamebadilika na hali ya hewa imebadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Singida kuna baadhi ya maeneo ya umwagiliaji, nilibainisha nikamkabidhi Naibu Waziri wa Kilimo aliyepita lakini mpaka sasa hakuna kitu. Lakini vile vile kuna *scheme* ya umwagiliaji Mang'onyi ambayo Wizara ya Kilimo walikuwa wanaishughulikia. Nayo imedemadema sasa huu ni mwaka wa tatu hakuna mafanikio.

Naomba Wizara ya Kilimo iangalie *scheme* ya Mang'onyi. Sisi ambao tunapata mvua mara moja kwa mwaka, nadhani tuna haja ya kusaidiwa pale ambapo umwagiliaji unastahili kuwepo na pale ambapo mipango mbalimbali ya uvunaji maji inavyoweza kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni suala la utawala bora. Serikali kama Serikali ni kubwa. Wizara zipo nyingi lakini katika suala la utawala bora yapo maeneo yakifanya kazi vizuri sifa itapatikana kwa Rais wetu na Serikali nzima.

Lakini yapo maeneo machache yakifanya vibaya haki isipotendeka sura ya Serikali yetu itaharibika kwa mfano, kama Mahakamani haki itakuwa haitendeki, kama Polisi haki itakuwa haitendeki, katika eneo la ardhi haki itakuwa haitendeki, upande wa

Hazina mirathi ambayo inalalamikiwa na watu wote haki haitendeki, mahospitalini kina mama, watoto na watu mbalimbali hawapati matibabu mpaka wazungumze vizuri na maeneo mengi kama ya shule na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maeneo ni machache lakini ni nyeti kwa sababu ya *interaction* ya moja kwa moja kati ya mwananchi na yule mhusika kwa niaba ya Serikali. Sasa pamoja na kwamba Serikali nzima lazima ifanye kazi vizuri lakini kama haya maeneo yatasimamiwa vizuri, yatafanya kazi vizuri, haya yanaweza yakatoa picha nzuri kwamba hii Serikali ya Awamu ya Nne inafanya kazi vizuri na kama maeneo haya yakafanya vibaya yatapaka matope Serikali yote hata kama wengine hawana hatia. Nawaomba sana Mawaziri waliohusika na maeneo haya wajaribu kuangalia maeneo haya ili kusudi sifa yetu ya Serikali isiharibike.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upande wa maji mimi nashukuru sana sisi Singida tuliingizwa katika mpango wa Benki ya Dunia. Namshukuru Mheshimiwa Lowassa alipokuwa Waziri wa Maji na naishukuru Serikali, lakini mradi wa Maji wa Benki ya Dunia toka mwaka 2002 mpaka leo hakuna hata kisima kimoja kilichochimbwa, ni urasimu tu. 2002, 2003, 2004, na 2005 wananchi wamechanga hela chungu nzima wanatuuliza kila siku mmetwambia tuchange pesa, tumechanga maji yako wapi, vipi tukae na mradi ambao hauna *effect* kwa muda wa miaka mitatu au minne.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anayehusika na huu mradi kwa kweli utaonekana haufai kama hatua za haraka hazitachukuliwa na kuwapatia wananchi maji. Wananchi wanataka maji na hawataki maneno na ahadi nyingi ambazo hazina sababu. Lakini vile vile mimi nashauri suala la maji sasa liwekewe *program* kamili, program maalum kama ilivyo MMES kwa elimu, kama ilivyo MMEM kwa elimu na sasa maji yawe na program maalum, kila Kijiji kiwekewe mkakati wa kupata maji, maji ni tatizo ukiacha umaskini na balaa la njaa lililopo sasa hivi *the next issue* ambayo ni tatizo kwa wananchi ni maji. Kwa hiyo naomba Serikali iweke program maalum ili kila Kijiji kiweze kupata maji, hapo tutakuwa tunapata afueni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni afya. Hospitali ya Mkoa ya Singida haina hata Daktari mmoja bingwa. Tumepiga kelele hapa, mimi nimeuliza swali, Mheshimiwa Chilolo akauliza swali, Mheshimiwa Msindai akauliza swali, tumeahidiwa ahadi chungu nzima lakini mpaka leo hata Daktari mmoja bingwa hakuna.

Akinamama wanapata matatizo makubwa pale ambapo wanataka Daktari bingwa, watoto wanapata matatizo makubwa pale ambapo wanataka Daktari bingwa. Sasa watu wanahusisha vifo vinavyotokea kwamba ni sababu hatuna Daktari bingwa. Kifo ni kifo Mwenyezi Mungu muda wako aliokupangia ukimalizika basi lazima ufe, lakini kama yapo mazingira ambayo yanaonyesha kuchangia, basi watu wanaamini hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo imani ya wananchi sasa ni kwamba Mkoa wa Singida Serikali haiujali na wala haiwajali watu wanaokufa na watoto wanaokufa. Itakuwaje Serikali ya Mkoa mzima wa Singida haina hata Daktari mmoja bingwa!!

Ni jambo la kusikitisha. Tuliahidiwa habari ya Madaktari kutoka Cuba, wamekuja wamekaa miezi miwili, mitatu hawapo, wametoweka na hatuelezwi kwa nini wale Madaktari wameondoka ili mradi sasa Mkoa mzima wa Singida hauna Daktari bingwa na wale wa Cuba wameondoka. Niambiwe kwanza kwa nini Madaktari wale wameondoka lakini pia niambiwe hatua gani za haraka zinachukuliwa ili kutupatia Madaktari bingwa katika Mkoa wa Singida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la ajira sisi tulionadi sera za CCM tumelipigia kelele hili na limechangia katika kutupatia kura. Suala la ajira kwa vijana kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais lazima lipewe kipaumbele. Mimi nashauri maeneo yafuatayo yatiliwe mkazo tutapata ajira. Moja, kwanza sheria ya ajira yenyewe itazamwe upya. Mimi nina wasiwasi sheria ina upungufu kiasi kwamba inaruhusu wapishi, ma-*cashier* kutoka China, India na kwingineko kuja kufanya kazi ya upishi, eti kwa sababu chakula cha Kichina hatuwezi kupika, nani kasema hayo?

Chakula cha Kiswahili ndio kigumu kupika lakini kwa sababu ya *loophole* zilizopo katika Sheria ya Ajira ndio maana Wachina wanafanya hiyo kazi. Lakini sasa hivi yapo madai huko Dar es Salaam kwamba Wachina sasa wanafanya kazi ya vijana wetu hawa Wamachinga wanatembeza kila kitu kwa nini? Tunalalamika ajira hakuna tunaruhusu wageni wanafanya kazi mpaka ya Umachinga hivi kweli sisi tuko wapi. Naomba hii sheria kama ina matatizo iangaliwe upya na kwa kweli tuzibe mianya ambayo inawafanya wenzetu kutoka nje waje wachukue ajira badala ya vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba tuwekeze katika mashamba makubwa, tuwakaribishe wawekezaji katika mashamba makubwa, mashamba hayo makubwa kama ya mpunga na kadhalika yatatusaidia kutoa ajira kwa vijana wetu huko Vijiji na tutapunguza tatizo la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile India wananufaika sana kwa viwanda vidogo vidogo. India ni wengi sana kuliko watu wote, lakini tatizo la ajira kule sio kubwa sana kama lilivyo hapa kwetu. Hapa kwetu maembe yanaoza, machungwa yanaoza, mananasi yanaoza.

Kama tukifanya utaratibu wa kuwa na viwanda vidogo vidogo katika maeneo kama ya kule Tanga, Morogoro, Singida na kadhalika mimi nina hakika vijana wetu watapata ajira. Sasa naomba tupeleke *delegation* kule India tukajifunze wenzetu Wahindi wamewezaje kuwa na viwanda vidogo vidogo lakini sisi tunashindwa. Tulifanye hili ili kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa ahadi ya ajira aliyoitoa. Moja ya eneo ni viwanda vidogo vidogo vya juisi ya machungwa, mananasi, maembe na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunasema ajira hakuna, lakini zipo nafasi wazi mashuleni, walimu hakuna, zipo nafasi wazi mahospitalini, madaktarini hakuna na manesi hakuna, huku tunasema kwamba tuna tatizo la ajira. Vijana wetu wanahitimu chungu nzima mashuleni, kwenye vyuo na kadhalika tunaji-*contradict* kwa nini? Tunasema ajira hakuna lakini hatujazi nafasi zilizo wazi, urasimu Serikalini tuuondoe,

Menejimenti ya Utumishi waondoe urasimu, vijana wetu waajiriwe. Akishatoka Daktari kule Muhimbili aende kufanya kazi, akitoka mwalimu kwenye vyuo vyetu vya ualimu waende kufanya kazi. Tuachane na urasimu ambao hauna sababu, unaweza ukatuharibia mambo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niongelee kuhusu mikopo kwa wananchi walio Vijijini. Vijijini mabenki hayataki kutoa mikopo kwa wananchi waliopo Vijijini. Naomba mabenki yatoe mikopo pia kwa wananchi walio Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge saa ya kuahirisha kikao imefika, ningependa kusema yafuatayo. Kwanza kabisa kesho inaelekea tutakuwa na kazi nyingi, asubuhi saa mbili na nusu watu muwahi kwa ajili ya kuji-*register* kuna semina moja ambayo itahusu watu wote. Baada ya hiyo semina ya watu wote Wabunge wanachama wa CCM wataendelea na mkutano wao wa Uchaguzi.

Kwa hiyo, baada ya semina hiyo halafu tutakuwa na kikao cha Chama kwa ajili ya uchaguzi. Sasa nimepewa nitangaze hapa na Waziri wa Nchi, TAMISEMI anasema hivi Waheshimiwa Wenyeviti wa Waheshimiwa Wabunge katika Mikoa mnaalikwa nyumbani kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu leo tarehe 10 Februari, 2006 saa mbili na nusu usiku. Waheshimiwa Wenyeviti wa Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa kama wapo viongozi wa namna hiyo. Nadhani kuna Mikoa ambayo imechagua tayari Wenyeviti wao katika Mikoa yao, sasa hawa ndio wanaoalikwa.

Baada ya kusema hivyo, naomba kusema orodha tuliyonayo ya kuchangia siku ya Jumatatu itatosha. Kwa hiyo, wote walioko kwenye orodha ile watapata nafasi ya kuchangia kabla hatujaitakia Serikali ianze kujibu hoja zetu nadhani Jumanne. Kwa hiyo, nawatakieni *weekend* njema, naahirisha kikao mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01.42 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu Tarehe 13 Februari, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*